**BUNGE LA TANZANIA**

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Saba - Tarehe 17 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UHUSIANO NA URATIBU:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora) Pamoja na (Uratibu na Mahusiano) kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/ 2014.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MHESHIMIWA KULIKOYELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA, URATIBU NA MAHUSIANO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora) Pamoja na (Uratibu na Mahusiano) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 52

### Tatizo la Maji Mji Mdogo wa Tinde

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Tinde umekuwa kwa kasi sana lakini unakabiliwa na ukosefu wa maji ya uhakika.

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ili kuondoa tatizo hilo la maji huku wakiwa wanasubiri mpango wa mradi wa Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tinde unakuwa kwa kasi sana na hivyo huduma za maji hazitoshelezi mahitaji kulingana na ongezeko la idadi ya watu. Kwa sasa wananchi wa Tinde wanapata huduma za maji kutoka katika visima vifupi 24 vilivyojengwa kwenye vitongoji vinavyozunguka Mji wa Tinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 39.0 kwa ajili ya kusambaza maji katika baadhi ya maeneo ya Mji huo kwa kutumia maji ya kisima kirefu kilichopo katika eneo la Sekondari ya Wasichana ya Tinde ambacho kina uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 6 kwa saa. Kwa sasa taratibu za kununua mabomba na pampu ya kusukuma maji zinaendelea.

Serikali kupitia Wizara ya Maji, ilishatangaza zabuni ya kumpata mtalaam Mshauri (*consultant*)atakayefanya kazi ya upimaji na usanifu wa mradi mkubwa wa maji kutoka Kahama kwenda Miji ya Kagongwa, Isaka, Tinde, Igunga na Tabora ambapo chanzo ni maji ya Ziwa Victoria. Watalaam washauri *consultants* walishawasilisha Wizarani zabuni zao *Technical and Financial Proposals* tangu tarehe 3 Aprili, 2013. Kinachoendela ni uchambuzi wa taarifa hizo ili kumpata Mkandarasi atakayefanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango wa muda mrefu wa Serikali wa kutoa maji Kahama ambayo chanzo ni Ziwa Viktoria, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imetakiwa kuhamasisha wananchi kuwa na utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua ili kupunguza uhaba wa maji unaotokana na ongezeko la idadi ya watu katika Mji huo. *(Makofi)*

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri kiasi fulani ya Naibu Waziri, naomba kupingana na taarifa yake ya kusema kwamba Mji Mdogo wa Tinde una visima 24. Mimi ninatoka Kitongoji cha Tinde Mji Mdogo wa Tinde, kisima kinachohudumia watu wa Tinde ni kisima kimoja tu na siyo 24 kama alivyosema hapa. Ninaomba kumkumbusha Naibu Waziri kwamba aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji Mheihimiwa Lwenge alishafika katika kisima kile akashuhudia adha kubwa wanayoipata wananchi wa Tinde kwa kuwa na foleni kubwa ya kusubiria maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa uchambuzi huu wa taarifa ya maji ya Ziwa Victoria nimekuwa nikiusikia toka mwaka 2011 na taarifa zake zinakuwa bado hazijakamailika, naomba nielezwe ni lini kazi hii itaanza?

Swalli la pili; kwa kuwa, Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Gerson Lwenge alipofika katika kisima kile alitoa ahadi ya kujenga tenki katika kisima cha Mwakisu ili kiweze kuhudumia watu wengi zaidi kwa muda mfupi kuliko foleni aliyoikuta pale.

Je, ni lini ahadi hiyo itatimizwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa majibu ya nyongeza kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini mradi huu wa kutoa maji Ziwa Victoria na kupeleka katika vijiji vya Kagongwa, Isaka na Tinde na vile vile kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Nzega, Igunga na Tabora na kwamba umekuwa ukisikia mara kwa mara lakini hautekelezwi, ni kwamba tayari mchakato wa utekelezaji wa mradi huu umeanza na sasa hivi tunavyoongea kama alivyojibu Naibu Waziri katika swali la msingi ni kwamba zabuni ambazo

zimewasilishwa tarehe 3 Aprili, 2013 zinachambuliwa na uchambuzi ule utachukua takribani miezi miwili na baada ya uchambuzi ndiyo upembuzi yakinifu utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo tunategemea upembuzi yakinifu utaanza kwenye mwezi wa Saba na utachukua miezi sita. Baada ya hapo ndiyo itatolewa zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi. Hii ni kwa miradi yote miwili ya kupeleka maji Tabora na kupeleka kule Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwamba kwanini inachelewa hii inatokana na ufinyu wa Bajeti. Kwa hiyo, tumekuwa tukitekeleza kulingana na fedha ambazo tumekuwa tunatengewa. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba mradi huu sasa utatekelezwa kwa kasi kubwa na katika Bajeti hii tutaleta maombi ya fedha za kutekeleza mradi huu tunaomba mtupitishie.

Kuhusu suala la ahadi ya Naibu Waziri alipokwenda kule na akaahidi suala la tenki tutalifuatilia na tutatekeleza kama ilivyokuwa imeahidiwa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hiki ni kipindi changu cha tatu nipo hapa Bungeni na tatizo la maji vijijini, vijiji vyote vya Tanzania ambayo ni asilimia 80 limekuwa ni tatizo kubwa na ni tatizo ambalo Serikali haijaonesha mikakati dhahiri ya kutatua tatizo hili.

Je, Serikali leo inaweza ikawaambia Watanzania wote wanaoishi Vijijini ina mkakati gani wa kuwafanya nao waondokane na maisha ya hatarini?

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru, hata Kongwa hilo ndilo tatizo namba moja Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kujibu swali hili la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tatizo la maji vijijini nchini kote ni kubwa sana, hivi sasa upatikanaji

wa maji vijijini ni watu asilimia 58 peke yake. Hii ina maana kwamba asilimia 42 ya watu ambao wanakaa vijijini wana matatizo ya maji. Katika mkakati wa Serikali wa *Big Result Now* yaani (Matokeo Makubwa Sasa) Serikali imepanga kutekeleza mradi wa maji Vijijini kwa haraka, kwa kuupa kipaumbele, na baadaye kuutengea fedha ili uweze kutekelezwa kwa haraka na kufikia asilimia 70 mwaka 2015. Hata hivyo, katika Bajeti ambayo ipo mbele yetu bado kuna changamoto kubwa katika kufanya jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa swali hilo umepita kitambo. Naomba nitambue uwepo katika ukumbi wa Bunge, Mbunge wa Njombe Kusini, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, katika Kiti chake. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi naomba nijibu kwa ujumla kuhusu suala la maji. Tatizo la maji sasa hivi ni tatizo la kidunia kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Ni ukweli usiopingika zamani maji yalikuwa mengi kwa sababu kulikuwa na vyanzo vingi kila kijiji kilikuwa na chanzo chake. Kwa hiyo, pamoja na mikakati aliyosema Waziri wa Maji, lakini sisi Wabunge tusaidie kuwaelimisha wananchi vile vyanzo vyetu vya asili ni lazima tuvirudishe. Kwa sababu hata hilo Ziwa Victoria tunalolitegemea asili yake maji yanaenda mto Nile. Sasa tunavyozidi kuvuna kuna siku kiasi cha maji kitapungua na wala hakitakidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba turudishe vyanzo vyetu vya asili vya maji. *(Makofi)*

Na. 53

**Huduma za Benki Katika Mji wa Laela**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Laela unakua kwa kasi sana na kuna shughuli nyingi za kibiashara zinazohitaji huduma za kibenki:-

Je, ni lini Serikali itawashawishi taasisi za kifedha kuanzisha matawi yao katika Mji huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waizri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Mallocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi kupata huduma za kibenki karibu na maeneo yao. Serikali pia inatambua kuwa, huduma hizo za kibenki kwa wananchi lazima ziwe za faida kwa pande zote yaani kwa mabenki na pia wateja (wananchi).

Kwa kutambua hilo Serikali inaendelea kuhakikisha kuweka mazingira bora na salama ya kiuchumi ili kuwezesha sekta binafsi kuanzisha mabenki na kutoa huduma bora za kibenki kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sera ya sasa ya huduma za mabenki wameshimiwa Wabunge wanaweza kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha wananchi wajiunge na kuanzisha Benki za Jamii *(Community Banks)* zinazozingatia mazingira ya mahali husika pamoja na kuzihamsisha benki zilizopo nchini kufungua matawi katika maeneo hayo. Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa suala hili, imewasiliana na Benki ya *NMB* ambao wamekubali kwenda Laela kuangalia kutathimini mazingira ya kibiashara kabla ya kufungua tawi mahali hapo. Suala hili litawekwa katika mpango kazi wa *NMB* wa mwaka ujao wa fedha. Serikali kupitia Benki Kuu, imeweka sheria na taratibu za kusaidia juhudi za wananchi katika kuanzisha mabenki au taasisi za fedha katika maeneo yao.

Aidha, Serikali inayo Sera ya Taifa inayolenga kuhamasisha uanzishwaji wa mabenki kwa ajili ya wateja wadogo *(National Microfinance Policy)*, sera hii inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha na Waheshimiwa wengine watawahamasisha wananchi katika maeneo yao kuunda taasisi za fedha zitakazowasaidia wananchi katika maeneo hayo. Aidha, Serikali pamoja na Benki Kuu ipo tayari kutoa ushauri wa kitalaam wa namna ya kuanzisha taasisi za fedha kwa wananchi wa Mji wa Laela na Miji mingine nchini yenye mahitaji ya namna hiyo pindi watakapokuwa tayari. *(Makofi)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa ufafanuzi na majibu yake mazuri, lakini ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; uanzishwaji wa *Community Banks* ni mpango wa baadaye na yapo mahitaji ya wananchi katika maeneo mbalimbali yanayohitaji huduma hiyo.

Je**,** kwanini Serikali isitumie hata utaratibu wa *mobile* benki ili kutoa huduma katika maeneo mbalimbali?

Swali la Pili; Mkoa wa Rukwa unaongoza katika Kilimo, lakini wakulima na wafanyabiashara wanailalamikia Serikali kwa riba kubwa inayotozwa na taasisi hizo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali tayari imeshawasiliana na *NMB particularly*, kwa ajili ya kwenda kufanya tathmini katika Mji wa Laela kuona kwamba inalipa sasa kuweka tawi pale la *NMB.* Kama tutafuatilia kuhusiana na *Mobile Banks* Serikali haitoi huduma za kibenki kama yenyewe lakini kupitia Benki Kuu inayo *policy* vile vile ya kutumia *Mobile Banking.*

Utaona kwamba sasa hivi benki zingine sasa hivi zinatumia *Mobile Banking*, lakini kuna *services* zingine ambazo wananchi vile vile wanatakiwa wazitumie. Kwa mfano sasa hivi Benki Kuu *(BoT)* tayari imeshatoa agizo kwa mabenki kuanza sasa kutumia *agency* kwa ajili ya kupata huduma za

kibenki kwa wananchi. Kwa hivyo hili tunalichukua *NMB* tayari wameshasema kwamba wanakwenda kufanya *assessment* lakini vile vile tutawashajihisha benki zingine ziweze kutoa huduma zao karibu na wananchi kwa kutumia, *not necessary* kuweka *physical structure* ya benki pale, lakini kwa kutumia *agencies* na kutumia *Mobile Banking*.Hili tunalichukua na ninaamini kwamba hata mabenki wameshalisikia hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riba kubwa hili siyo tatizo la Miji hiyo, riba kubwa ni tatizo la mabenki yote kuwatoza wananchi. Hili nalo linafanyiwa kazi. Kuna *effects* nyingi kutokana na hili, kwanza riba kubwa inatokana na mabenki wao wenyewe zile fedha wanazozipata wanazipata kwa riba kubwa. Kwa hivyo wanapokopesha na wao wanataka wapate faida nao wanaongeza riba.

Lakini vile vile tumeona changamoto kwamba Watanzania wengi sana tukubali hatuna pahali ambapo ni *static*, tunazunguka sana. Kwa hivyo hata mabenki inakuwa *very risk* kumkopoesha mtu kwa sababu kawaida inakuwa huwezi kumpata sehemu alipo. Kwa hivyo kwa kutambua hilo sasa Serikali ndiyo tumeanzisha mradi wa *NIDA* ambao angalau kwenye kitambulisho chako kuna *details* za makazi na *details* za vitu vingine ambapo benki inaweza ikakupata.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kuna mambo mengi, kuna changamoto nyingi kutokana na hili. Lakini hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na mabenki pia inajitahidi kuhakikisha kwamba hata hizi riba zinaondoka kwa kuweka *Economic Infrastructure* kubwa ya kuwawezesha wananchi kupata *access to bank* na vile vile benki kuwakopesha katika *affordable rates. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, Wizara ya Maji swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum kutoka Solwa, matatizo ya maji kule Tinde yanajirudia.

Na. 54

**Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza:-

Katika awamu ya pili ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Vijiji vyote vilivyo ndani ya umbali wa Km 12 kutoka bomba kuu, ni Sera na Mpango ulioko Serikalini, lakini mpaka sasa hakuna maelezo yoyote juu ya utekelezaji wa mradi huo:-

(a) Je, Serikali, inasema nini juu ya utekelezaji na kukamilisha mradi huo?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya mradi huo katika Mwaka wa Fedha 2012/2013?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu *(a)* na *(b)* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatekeleza kwa awamu mpango wa kupeleka maji kwenye vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu la kusafirisha maji kutoka Ziwa Victoria. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, Serikali, imeunganisha jumla ya Vijiji 39 vilivyopo umbali wa Kilometa tano (5) kutoka bomba kuu. Wananchi wa vijiji hivyo, wanapata huduma ya maji tangu mwezi Februari 2009. Katika awamu ya pili ya utekelezaji Serikali, imeongeza wigo ambapo vijiji vyote vilivyopo umbali wa kilometa 12 kutoka kwenye bomba kuu vitaunganishwa.

JUmla ya vijiji 100 vimeainishwa kama ifuatavyo: Wilaya ya Misungwi vijiji 14, Kwimba vijiji 22, Shinyanga vijiji 46 na Kahama vijiji 18. Serikali imeanza utekelezaji katika vijiji vya Nyang'homango, Isesa, Igenge na Mbalika, ambavyo vipo karibu na kituo cha kuzalisha maji cha Ihelele.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 400 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa maji kutoka Ziwa Viktoria. Hadi mwezi Machi 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi milioni 154. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili na nishukuru tu kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika majibu yake amesema Wilaya ya Shinyanga Vijijini, tuna vijiji 46 katika awamu ya pili, lakini hivi ninavyoongea mpaka sasa hivi hakuna hatua yoyote inayofanyika katika utekelezaji wa awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sielewi. Naomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri, anieleze kama kuna fedha, fedha zilizopangwa ni shilingi ngapi? Utekelezaji wake ukoje na lini tunaweza tukapata huu mradi ukakamilika kwa ajili ya wananchi wa Shinyanga Vijijini, kwa maana ya Jimbo la Solwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Katika miradi ya *World Bank,* unajua kabisa kuna adha kubwa sana ya ucheleweshaji wa kupata fedha. Bahati nzuri sana sisi katika Jimbo la Solwa, tumepata mradi huo tunautekeleza katika Kata ya Didia na Kata ya Mshepo, kwa sasa. Baada ya hapo tutakwenda Kata ya Ilola na Remidadi

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, aseme ni kwa nini sasa mikataba ambayo iko Wizarani kwake, kuidhinisha kumpata Mshauri Mwelekezi, imechelewa sana kutolewa ili na sisi tumpe Mkandarasi atekeleze mradi wa maji wa *World Bank* katika Kata ya Didia na Mshepo? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi kujibu swali la rafiki nyangu, Mheshimiwa Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimetembelea eneo la vijiji hivyo ambavyo vimetajwa, kilometa 12 kutoka pande zote za bomba kuu. Na katika mwaka wa Fedha 2013/2014, tumepanga kuanza utekelezaji wa kuvipatia maji vijiji hivyo. Na tumapanga kwamba, shilingi bilioni 4 zitumike kupitia Mamlaka ya Kashwasa, ili kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika Bajeti tuliyowasilisha mwaka jana, tuliazimia kutekeleza vijiji 5 katika vijiji 10 ambavyo vimepangwa katika kila Halmashauri. Serikali, imejitahidi kwa nguvu zote kuanza utekelezaji wa vijiji hivyo, ikiwa ni pamoja na vijiji hivyo alivyovitaja rafiki yangu, Mbunge wa Solwa.

Hivi karibuni tumepeleka fedha za ziada, ili vijiji vile vya kwanza viweze kukamilika. Tumeazimia kwamba, katika Bajeti inayokuja, tutamaliza vijiji vile vitano vilivyobaki katika Halmashauri zote Tanzania nzima. *(Makofi)*

Na. 55

**Mapato yatokanayo na Uwanja wa Taifa Dar es Salaam**

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Serikali imeelekeza Taasisi zote za umma na binafsi zikiwemo Halmashauri za Miji, Majiji, Manispaa na kadhalika, kuchangia jamii zinazozizunguka ili kuendeleza mashirikiano yao na jamii hizo. Manispaa ya Temeke, ambayo ndiyo mwenyeji wa Uwanja wa Taifa Dar-es-Salaam, hainufaiki na mapato yatokanayo na uwanja huo.

(a) Je, Serikali, inatoa kauli gani?

(b) Je, tangu uwanja huo uanze kutumika, Serikali, imepata kiasi gani na kati ya hicho, Manispaa ya Temeke imepata kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Temeke, hunufaika kutokana na mapato yatokanayo na matumizi ya Uwanja wa Taifa, ambayo huingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mapato hayo yanatokana na 18% ambayo ni Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* inayokatwa kwa kila mchezo unaochezwa na kupelekwa *TRA* na pia gawio la 15% ambazo hukatwa kama ada ya matumizi ya uwanja. Mapato yote haya hutumiwa na Serikali, katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wa Tanzania, ikiwa ni pamoja na wa Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mapato hayo, matukio yote yanayofanyika Uwanja wa Taifa, huwanufaisha wananchi na Manispaa ya Temeke kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa fursa kwa wafanyabiashara ndogondogo wa eneo hilo kutoa huduma mbalimbali za kibiashara ambazo huwaingizia kipato. Aidha, kutokana na kodi mbalimbali zinazotozwa kwa huduma hizo kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Uwanja wa Taifa uanze kutumika mwezi Agosti, 2007 hadi kufikia mwezi Februari, 2013, makusanyo yanayopitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambayo ni 15% ya mapato baada ya kutoa *VAT,* ni 1,533,697,666.92/=. *(Makofi)*

Aidha, mapato yanayokusanywa kupitia Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* huwasilishwa *TRA* na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini *(TFF).*

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, nasikitika sana kwa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, Manispaa ya Temeke, hatupati kitu chochote. Niliwahi kuwauliza Wakurugenzi waliopita na waliopo, hatupati chochote ni masikitiko makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili. Kiasi cha pesa kilichotajwa kwamba, kimekusanywa kuanzia mwaka 2007 hadi sasa ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na mechi ambazo zinafanyika Uwanja wa Taifa. Hapa kuna mianya mingi sana ya ufisadi ambayo inafanyika kulingana na mazingira yaliyopo. Hata gazeti la jana la Nipashe, limeonesha ni namna gani fedha inaporwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mechi ya *Leopards* ya Afrika Kusini, iliyofanyika katika Uwanja wa Taifa, pesa iliporwa kwa sababu wana mtindo wa kubeba pesa kwenye begi wanapeleka *TFF,* pesa nyingi namna hiyo, kwa nini ibebwe mkononi? Tunataka kujua, tunaomba na *CAG* afanye ukaguzi; hapa pana ufisadi, naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu Maswali mawili ya Mheshimiwa Mturano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, fedha zote, yaani maduhuli ya Serikali, yanayopitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, hupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini pili, *VAT* nayo hupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, fedha hizi zote zinatumika katika Mfuko Mkuu wa Serikali na Watanzania wote wakiwepo wa Temeke.

Kwa hiyo, ni kwamba, Temeke wanapata, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali, ambayo hayo ndio sehemu ya mapato ambayo tukikaa hapa katika Bajeti tunaangalia kwamba, mapato yatatokana na nini, ikiwemo hilo na kugawanya hizo fedha kwa Watanzania wote, wakiwepo wenzetu wa Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwanza nataka niseme tu kwamba, kwa takwimu tulizo nazo ni kwamba, upo uwazi wa mapato yanayotokana na Uwanja wa Taifa na kwa asilimia ambayo Serikali inapata na kwa asilimia ambayo *TFF* wanawasilisha *VAT.*

Mheshimiwa naibu Spika, baada ya makato, kwa maana ya *VAT* matumizi na kile kinachobaki kupeleka *TRA.* Sasa mimi sitaki sana kufanyia kazi habari za magazeti kwamba, kuna ufisadi.

Lakini nataka niseme tu kwamba, jambo hilo kama lipo, sisi Serikali, tutaendelea kufuatilia, lakini pia Serikali, imejipanga zaidi kudhibiti mapato zaidi. Tutaweka vifaa vya kuweza kukagua tiketi kwa maana ya kisasa zaidi badala ya hizi tiketi za kawaida, ambayo itatusaidia katika kudhibiti mapato. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsantesana. Tunajua kwamba, Serikali, ina dhamira ya dhati ya kuibua vipaji kupitia michezo, lakini huwezi ukaibua vipaji kama viwanja havipo katika hali nzuri, hasa viwanja ambavyo vipo katika ngazi ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inakarabati viwanja vya Wilaya, ikiwepo kiwanja cha Saba Saba Wilayani Bunda na hasa ukizingatia *Ester Cup* inaendelea sasa hivi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, nakubaliana na yeye kwamba, moja ya changamoto katika michezo yetu ni miundombinu, vikiwepo viwanja. Nakubaliana na yeye kabisa kwamba, Serikali kupitia Halmashauri mbali mbali na Manispaa, tushirikiane kwa pamoja na wadau mbalimbali kuviendeleza viwanja hivi, ili tuwe na miundombinu mizuri ambayo itaendeleza michezo yetu hapa nchini. *(Makofi)*

Na. 56

**Makato ya Asilimia Mbili (2%) Kwa Walimu Wote Nchini**

**MHE. LUHAGA J. MPINA (K.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Walimu wote nchini, wamekuwa wanakatwa 2% kwenye mishahara yao.

(a) Je, tangu mwaka 2005 – 2011 kupitia makato hayo ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa?

(b) Je, jengo la *"Mwalimu House"* pamoja na majengo mengine katika Mikoa ya Mtwara, Kigoma na Mbeya, yanapangishwa kwa shilingi ngapi kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi, kiasi kilichochangwa na wanachama kutoka mwaka 2005 hadi 2011 ni shilingi bilioni 81,278,071,321.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Jengo la *"Mwalimu House"* lilikamilika mwaka 2007 na ndipo lilipoanza kupangishwa. Hadi kufikia mwaka 2011 jengo hilo lilikuwa limepata jumla ya shilingi milioni 920 kama mapato ya kodi ya pango hilo kutoka kwa wapangaji. Aidha, fedha hizo zilipelekwa kwenye mifuko ya *SACCOS* za Walimu Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jengo la *CWT* katika Mkoa wa Mtwara, linatumika kama Ofisi na kuna mpangaji mmoja tu ambaye, hulipa kiasi cha shilingi milioni nne (4,000,000/=) kwa mwaka tangu mwaka 2011. Jengo la *CWT* Mkoa wa Kigoma, halijapangishwa bali linatumika kwa shughuli za Ofisi za Chama. Aidha, jengo la *CWT* Mkoa wa Mbeya, linaendelea kujengwa na hivyo, halijapangishwa bado. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, mfanyakazi yeyote yule ni lazima aridhie makato ya uanachama wake katika Taasisi anayoingia. Na kwa kuwa, *CWT* Mwalimu mara tu anapoajiriwa hapo hapo hutakiwa kukatwa hiyo 2%.

Je, hiyo ni njia halali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Walimu hawa ambao ni wanachama wakubwa wanaochangia asilimia mbili (2%) ya mshahara wao, wanapewa fursa ya kupata taarifa ya mapato na matumizi ya fedha zao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza kwamba, Walimu ama wanachama ni kawaida ya kuridhia makato yao kwenye mishahara yao na hivyo *CWT* au Hazina, wanakata asilimia mbili Walimu kwenye mishahara yao. Je, Walimu hawa wanakuwa wameridhia?

Jibu hili ni nkwamba, baadhi ya Walimu wanakuwa wameridhia na baadhi ya Walimu wanakuwa hawajaridhia. Suala hilo Serikali, imeshaliona na tayari Waziri wa Kazi na Ajira, alishalitolea ufafanuzi hata kwenye vyombo vya habari.

Sasa hivi tutaomba ushirikiano tu na Wizara ya Fedha, iweze kuhuisha taarifa hizi za Walimu wote wanachama nchini, ili angalao 2% hii inapokatwa kwa Walimu, Walimu wote wanakuwa wameridhia.

Kwanza wanakuwa wamekubali kuwa wanachama na baadaye barua ya pili inakuja kama fomu, ili Walimu waweze kuridhia makato hayo. Suala hilo nadhani linaendelea kufanyika kwenye Ofisi ya Hazina na Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato na matumizi kwenye chama cha *CWT,* siwezi kuwasemea sana, lakini utaratibu ni kwamba, mapato ya fedha hizi yanakwenda huko kwenye *SACCOS* za Wilaya na Mikoa.

Sasa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi, ndiye mwenye dhamana ya kuangalia mapato na matumizi pamoja na Wizara ya Kazi. Nilichukue hilo, tutashirikiana na Waziri wa Kazi na yeye yupo hapa ananisikia, ili tuweze kuona namna wanavyosomeana mapato na matumizi kwenye matawi yao.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mishahara, posho na stahili nyingine za Walimu wapya, zimekuwa zikichelewa sana kuwafikia, jambo linalowasababishia usumbufu mkubwa sana kama ilivyo sasa katika katika Jimbo la Rombo. Walimu walioajiriwa mwaka huu, mpaka sasa hivi wanahangaika kupata posho zao na mishahara yao.

Je, Serikali, ina tamko gani kuhusu jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho na mishahara kuchelewa kwa baadhi ya Halmashauri, ikiwemo Rombo, suala hili ni kweli, hata mimi Napata *message* nyingi za Walimu, lakini ufafanuzi tu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alipokuwa anatangaza ajira kwa Walimu, alitoa maelezo kwamba, Walimu wote hawa wakaripoti kati ya tarehe 1 Machi, 2013 na tarehe 9 Machi, 2013.

Walimu watakaokwenda kuripoti baada ya hizo tarehe maana yake watapambana na mkumbo huu wa kucheleweshewa posho pamoja na mishahara kwa sababu, unakuta pale Halmashauri, Afisa Utumishi anakuwa ameshapeleka zile taarifa kule Hazina na hivyo, inaweza ikasababisha ucheleweshaji wa suala kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa namshauri Mheshimiwa Mbunge wa Rombo, akiona Walimu wengine ambao labda walicheleweshwa lakini waliripoti *before* tarehe 9 Machi, 2013 kwa hilo tuwasiliane.

Lakini wale wote unaokuta wamechelewshwa, basi ni wale ambao waliripoti baada ya tarehe 9 Machi, 2013 tarehe za kuripoti kama alivyotangaza Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ilitokea kwamba, baadhi ya Walimu hawakuwa *interested* kuendelea kuwa Wanachama wa Chama cha Walimu, hasa wale wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambao walilazimika kukishitaki Chama cha Walimu Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ile ikawa imetoa *rulling* kwamba, Walimu wale kweli, wanastahili kutokuwa wanachama wa Chama cha Walimu, ambacho ni hiki cha sasa.

Je, Serikali, iko tayari kuweza kuwasaidia Walimu hawa kujiondoa kwenye Chama cha Walimu kwa kuwa, wameona kwamba, hakina tija?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Machali, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Walimu wa Kigoma Ujiji pamoja na Kasulu, wanataka kujitoa kwenye Chama cha *CWT,* lakini baadaye walipeleka kesi hii Mahakamani.

Mheshimiwa, hatuwezi kuanza kutoa majibu ya Kimahakama hapa, kesi hii bado haijaamuliwa. Lakini suala hili hata Wizarani tunalifahamu, hata *TAMISEMI* wanalifahamu, lakini hatuwezi kuongelea zaidi mambo nya Mahakamani, lakini ni kweli suala hili lipo kule Kigoma. *(Makofi)*

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu naomba kufanya marekebisho kidogo kwenye mstari wa pili kutoka chini isomeke Shule za Sekondari za kiwango cha *A-level.* Baada ya masahihisho hayo naomba sasa swali langu Namba 57 lipate majibu.

Na. 57

**Upungufu wa Sekondari za A-level, VETA Morogoro Vijijini**

**MHE. DKT. LUCY S. SAWERE** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini inakabiliwa na ukosefu mkubwa wa shule za Sekondari za *A-level* na chuo cha Ufundi *VETA:-*

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Sekondari za *A-level* katika Halmashauri ya Morogoro?

(b) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kujenga chuo cha Ufundi *VETA* katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili shule iweze kupata kibali cha kuanzisha mikondo ya Kidato cha tano na sita inatakiwa kutimiza vigezo muhimu kama vifuatavyo:

Vyumba vya madarasa na thamani za kutosha, mabweni ya kutosheleza wanafunzi wa kidato cha tano na sita, maabara tatu zenye vifaa kwa shule inayofundisha masomo hayo, vyoo vya kutosheleza watumishi na wanafunzi wote kwa jinsia zao, jiko, bwalo, vitabu vya kiada vya masomo husika, walimu wa kutosha kwa masomo husika na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini kuteua shule moja kati ya shule za *O-level* zilizopo katika Wilaya hiyo, shule inayokusudiwa kuanzisha mikondo ya Kidato cha Tano na Sita na kukamilisha vigezo vilivyotajwa. Baada ya kukamilisha vigezo hivyo Serikali itatuma wakaguzi wa shule wa kanda ili kubaini kiwango cha ukamilifu wa miundo inayotakiwa ndipo shule itapata kibali kwa mikondo ya *A-level*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zenye Kidato cha Tano na Sita ni za kitaifa na hivyo hupokea wanafunzi kutoka nchi nzima kulingana na taasisi yaani *combinations* za masomo zilizopo kwenye shule husika. Hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wanafunzi wote watakaofaulu kuendelea na masomo ya kidato cha Tano katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini hawatakosa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Wilaya ya Morogoro Vijijini haina chuo cha Ufundi stadi yaani *VETA.* Kwa kutambua hilo Serikali imeiweka Wilaya hiyo kuwa ni miongoni mwa Wilaya 28 za kujengewa vyuo vya *VETA* kwa awamu ya kwanza ambapo tayari nyanja zitakazofundishwa umeshafanyika tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Morogoro Vijijini kwa sasa kutumia vyuo vya Ufundi stadi vilivyopo karibu vya Morogoro, Kihonda, Dakawa na Mikumi kupata huduma za mafunzo wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kutafuta fedha za ujenzi wa vyuo vya Ufundi stadi katika Wilaya zilizobainishwa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. LUCY S. SAWERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika Wilaya ya Morogoro Vijijini kuna shule kadhaa ambazo zinakidhi viwango alivyoviainisha Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa bahati mbaya kuna vigezo vichache tu ambavyo kufuatana na hali yetu ya kiuchumi tumeshindwa kuvitekeleza kama kujenga maabara za nyongeza.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuisaidia Halmashauri hii kuongeza angalau hata maabara kwenye shule moja ili tuweze na sisi kupata Kidato cha Tano cha Sita katika Wilaya yetu?

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wameshafanya utambuzi wa stadi ambazo zinahitajika kufundishwa katika Wilaya 28, Halmashauri ya Morogoro ikiwemo.

Je, Serikali sasa kwa sababu kuna vijana wengi ambao wamemaliza darasa la saba na wengi sana ambao wamemaliza kidato cha nne na hawakupata fursa ya kuendelea na masomo au kupata nafasi kwenye vyuo vingine.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa angalau kujenga chuo kimoja katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na wanaanza kujenga lini hicho chuo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mbunge wa Morogoro Mashariki, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetangulia kusema kwenye jibu langu la msingi kwamba ili shule iwe na vigezo vya kusajiliwa kupata mikondo ya Kidato cha Tano lazima

ikamilishe vigezo nilivyovitaja na Mheshimiwa Mbunge hapa kwanza nimshukuru anasema baadhi ya shule kule kwake tayari zimekamilisha vigezo hivyo na bado kuna mapungufu madogo madogo kama maabara na kadhalika.

Mimi nilikuwa namwomba tu Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake pale, wananchi waweze kukamilisha mapungufu hayo ama sivyo ningemshauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu tumebaini au tumetambua shule 264 ambazo kila Halmashauri tumeteua shule 2 kwamba zitakuwa *functional schools* na tayari fedha hizo ziko kwenye Halmashauri na tayari mambo yanakwenda huko. Sasa inategemeana katika Wilaya hiyo kama miongoni mwa shule mtakuwa mmeteua ikawa ni hiyo basi itapendeza zaidi na mimi ningekushawishi ukafanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chuo cha *VETA* kama nilivyosema kwamba Serikali inaendelea kuandika maandiko mbamlimbali kuomba fedha kwa wahisani ili tuweze kukamilisha vyuo hivi 28. Lakini mpaka sasa tayari majadiliano yanaendelea kati ya Serikali na *ADB* kuangalia upatikanaji wa fedha kiasi cha dola za Kimarekani milioni 4.7 ili zitakazotumika kujenga vyuo hivi vya Ufundi vya Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kwa kuwa Vyuo vya *VETA* vimeonyesha kuwa vina umuhimu mkubwa sana kwa kuweza kuwasomesha au kutoa mafunzo kwa vijana wengi wa Kitanzania na vyuo hivi kwa kuwa vinatoa mafunzo mengine ambayo yanahitaji vifaa vya hali ya juu na ambavyo vinatumia gharama kubwa na pia watumishi au walimu ambao wanahitaji mishahara na mazingira ya kufundishia bora.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuongeza ruzuku au ruzuku ya *Skill Development Levy* ili kuweza kuviendesha vyuo vilivyopo vya *VETA* na hata vile vingine vinavyoanzishwa sasa hivi katika Wilaya hizo 28?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mtinda, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa hivi vyuo vya *VETA* kwa vijana wetu na kama nilivyosema katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) tumedhamiria kujenga chuo kimoja angalau kila Wilaya na mwaka huu mwaka uliopita kwenye Bajeti kwamba tulitenga Wilaya tano (5) kuweza kujengewa vyuo hivyo na tayari mpango huo unaendelea kwenye Wilaya za Kilindi, Chunya, Ukerewe, Ludewa na Namtumbo. Lakini sasa kama nilivyosema kwamba ni kutokana na ufinyu wa Bajeti mpaka sasa hatujaweza kukamilisha Wilaya zote 28 kwa pamoja.

Lakini katika azma ya kutekeleza mpango wa ujenzi wa vyuo hivyo Serikali imeamua sasa kukarabati vyuo 25. Vile vyuo vya Maendeleo *FTCs* vyuo 25 na tayari mwaka huu wanafunzi wameanza angalau wanafunzi 50 wameanza kuingia katika Halmashauri 25 ambavyo naweza nikavitaja hapa lakini kwa sababu ya muda Mheshimiwa Mbunge naweza nikakupatia baadaye jedwali hili uweze kulisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ya *SDL* naomba nilichukue hilo tukaweze kuangalia kama kuna uwezekano wa kuiongeza ama kubaki pale pale. Ni suala ambalo limekaa kibajeti zaidi. *(Makofi)*

Na. 58

**Kuboresha huduma za Mahakama Tunduru**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Je, Serikali itaboresha lini huduma za Mahakama katika Wilaya ya Tunduru kwa kujenga majengo na kutoa vifaa na wataalam ili chombo hiki kifanye kazi kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Ramo M. Makani, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuboresha huduma za mahakama nchi nzima kwa kujenga majengo ya kisasa, kutoa vifaa na wataalam ili chombo hiki muhimu kiweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali imekuwa ikijenga majengo ya mahakama kwa ngazi zote pale Bajeti inaporuhusu.

Kwa kupitia mfuko wa Mahakama, Mahakama zote nchini ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Wilaya ya Tunduru zitaendelea kupata mgao wa fedha za matumizi na vitendea kazi na kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Mahakama imeomba kibali cha kuajiri watumishi 593 hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi ajira hizo zitakapokamilika Mahakama ya Wilaya ya Tunduru itapewa kipaumbele. *(Makofi)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Awali ya yote niipongeze Serikali kwa kuja na mpango huo na niipongeze Serikali pia kwa kutamka wazi kwamba wakati wa kutekeleza mpango wa muda mrefu wataipa kipaumbele Wilaya ya Tunduru. Naamini wanafanya hivyo au mpango huo unakusudiwa kufanyika hivyo kwa sababu za kijiografia za pale mahali ambapo Tunduru ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati tunasubiri utekelezaji wa mpango wa muda mrefu nilikuwa naomba kuuliza kama ifuatavyo kuhusiana na mipango ya muda mfupi na muda wa kati. Wilaya ya Tunduru inazo mahakama za mwanzo 9 miongoni mwao ziko ambazo zipo umbali wa kilomita 150 kutoka moja kwenda nyingine na barabara na miundombinu ambayo haifai kabisa na haipitiki hivyo kusababisha haki za watu wengi sana washtakiwa na hata washtaki kuchelewa na hatimaye kuashiria kuzikosa kabisa.

Je, Serikali iko tayari sasa kutekeleza mipango ya muda mfupi na kuipatia angalau gari kwa sababu kwa sasa Mahakama ya Wilaya haina gari kabisa inayo *RAV 4* iliyochakaa kabisa ya mwaka 2005. Kwa hiyo je, Serikali iko tayari sasa kupeleka gari kwa ajili ya kuhudumia Mahakama za Mwanzo za Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kufuatia marekebisho ya sheria ya kuwaruhusu Mahakimu wahitimu wa Shahada ya kwanza kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo tulipata bahati ya kupata Mahakimu wanne ambao wangeweza kupunguza tatizo hili angalau kwa muda huu wa haraka lakini mpaka sasa bado utekelezaji wake haujaanza.

Je, Serikali itatekeleza lini mapendekezo yale ya Sheria au upitishaji ule wa Sheria ili Mahakimu hawa wanne waweze kusaidia kupunguza *gap* iliyopo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhandisi Ramo M. Makani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ameelezea kwamba wana shida ya gari kwamba lililopo limechakaa na wangependa kuomba Mahakama iweze kuwapatia gari. Tumepanga kununua magari kiasi lakini tukishapata Bajeti mkitupitishia tutaangalia na tutaipa kipaumbele Mahakama ya Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili kuhusiana na Mahakimu Wakazi wanne waliopangiwa katika Wilaya ya Tunduru na kwamba ni lini sasa wataanza kazi. Tayari barua zao zimeshaandikwa na saa yoyote kutoka hivi sasa wataripoti katika Wilaya hiyo ya Tunduru. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru Mahakama imekuwa inaomba bilioni moja tu kila mwaka kwa ajili ya ujenzi lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi lakini fedha za sherehe bilioni moja inatoka kila mwaka kwa ajili ya sherehe, kuandaa mazishi na kadhalika. Kwa nini Serikali isiwe *committed* kuwapatia Mahakama hii bilioni moja kwa ajili ya kujenga majengo yao nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali ambaye amehoji ni kwa nini Mahakama inashindwa kupewa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga Mahakama zake na kwamba tunaweza kupata katika Serikali bilioni moja kwa ajili ya mazishi. Ukiangalia kila Wizara, kila taasisi na yenyewe inastahili kupata Bajeti na hata mazishi pia na yenyewe ni muhimu na hatuwezi kuepuka katika maisha yetu katika jamii. Kama Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria. Lakini kwa kushirikiana na Mahakama tumekuwa tukijitahidi kujenga hoja na hata ukiangalia katika Bajeti hii inayokuja tuna nyongeza ya takribani 28.2% na endapo Wabunge itawapendeza ikiongezeka tutashukuru. *(Makofi)*

Na. 59

**Kiwanda cha Transfoma cha TANELEC**

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA** aliuliza:-

Kiwanda cha *TANELEC* kutengeneza *Transfoma* za Tanelec kilileta sifa kubwa Tanzania kwa kuwa bidhaa zake ziliweza kuuzwa hata nchi jirani:-

Je, kiwanda hicho bado kinaendelea na uzalishaji huo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhamed I. Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *TANELEC* hapo awali kilikuwa kikitengeneza *Transfoma,* majiko na vifaa vingine vya umeme. Baada ya kubinafsishwa na kupewa mwekezaji mwingine kiwanda hicho kiliendelea kutengeneza mashine za transfoma ambapo hadi hivi sasa bado kinaendelea na uzalishaji kama ifuatavyo: Mwaka 2,010 *transfoma* 1,389, mwaka 2011 *transfoma* 2,886 na mwaka 2012 kimezalisha *transfoma 2,173.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hivi sasa kiwanda hiki kinaendelea kuuza bidhaa zake katika nchi 10 za Afrika Mashiriki na kati zikiwemo Kenya, Uganda, Tanzania, Malawi na Zambia.

**MHE. MUHAMMAD I. SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Kiwanda hiki kilikuwa na ufanisi mkubwa sana wa kutengeneza hizi bidhaa ni sababu zipi zilizosababisha au kupelekea hadi kiwanda hiki kubinafsishwa na ni kampuni gani iliyopewa, suala la kwanza.

Suala la pili kwa kuwa nchi tajwa kumi, ikiwemo Tanzania ndizo zinazouziwa bidhaa hizi ni sababu zipi zinazopelekea Serikali hii kununua *transfoma* kutoka nchi za nje badala ya kununua *transfoma* zinazotengenezwa hapa nchini Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa viwanda na biashara napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni sabau gani ambazo zilisababisha kiwanda hiki kiweze kubinafsishwa. Kama ninavyokumbuka kwamba mwaka 1995 sehemu kubwa ya viwanda ambavyo vilikuwa ni kero au vilikuwa vinaendeshwa kwa kusuasua viliweza kufanyiwa sheria ya kurekebisha Mashirika ya Umma na miongoni mwa viwanda ambavyo vilihusika ni kiwanda hiki cha *Tanelec.*

Kwa kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hapo nyuma kilikuwa kinafanya vizuri sana lakini miaka ilivyokuwa inaendelea kutoka 1995 mpaka 2007 kiwanda hiki kilionyesha kusuasua. Kwa hiyo, yule Mwekezaji aliyekuwepo wakati huo ambaye Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua jina lake ni kwamba aliyekuwepo wakati huo kutoka wakati kiwanda hiki kinarekebishwa na kama shirika la Umma ambayo haikuweza kuweka hali zao vizuri alikuwa ni Bwana Aseya Brown Bova au *ABB Limited* ambaye alikuwa anatoka Zurich Switzerland. Ilipofika mwaka 2007 kwa sababu hii ya kusuasua aliweza kukiuza kiwanda hiki kwa muuzaji mwingine ambaye ni *Trans Century* kutoka Kenya.

Kusema kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, kilikuwa kinafanya vizuri hapo mwanzo, lakini baada ya kusuasua kililega lega na ndiyo maana kikaweza kubinafisishwa.

Lakini naomba niwaombe Watanzania wote kwa ujumla na wananchi kwa ujumla kupitia Bunge lako Tukufu kwamba tujenge tabia ya kununua bidhaa zetu sisi wenyewe hapa nchini, ambazo zinatengenezwa hapa nchini.

Sehemu kubwa ya watu, ikiwemo *TANESCO* ambaye ni mbia mkubwa katika kiwanda hiki, naye vilevile anaagiza bidhaa kutoka nje. *Transformer* kutoka nje na wanachi vilevile na mashirika, na ofisi zetu, tujenge tabia ya kununua bidhaa zetu ambazo zinazalishwa hapa nchini na nina imani kwamba ubora wa kutosha, kwa sababu *TBS* wanakagua bidhaa hizi.

Kwa hiyo, niwaombe sana kupitia Bunge hili kwamba, wananchi pamoja na *TANESCO* ambaye ni mbia mkubwa kwamba, tununue bidhaa zetu za ndani. Wizara yangu inahamasisha sana suala hili, kwamba watu tununue bidhaa zetu za ndani. Tuna kauli mbiu ambayo Wizara yangu inatumia kwamba, nunua bidhaa za Tanzania na Jenga Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda kama mtakavyoona saa zetu, naomba tulitendee haki swali mwisho la Wizara ya Uchukuzi la Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mbunge wa Mbulu.

Na. 60

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Manyara**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sera ya Uchukuzi ya mwaka 2003, Serikali iliahidi kujenga uwanja wa Ndege Mkoani Manyara mwaka 2003 katika eneo la Magugu ili kutoa huduma za usafiri wa Ndege kwa wananchi wa Babati, Mbulu na Katesh.

Je, Serikali itatimiza lini ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli serikali iliahidi kujenga Kiwanja kipya cha Ndege katika Mkoa wa Manyara, katika eneo la Ngungungu. Kwa mujibu wa sera ya Uchukuzi ya mwaka 2003, kila Mkoa unastahili kuwa na kiwanja cha Ndege cha Daraja la *3 (c),* chenye uwezo wa kuhudumia ndege za abiria zenye kubeba abiria 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa eneo hilo ni la serikali, tulikubaliana kuwa uongozi wa Mkoa uanze mchakato wa kuandaa ramani ya mipango Miji (*Town Plan Drawing*) ambayo itaainisha eneo ambalo kitajengwa kiwanja cha ndege. Baada ya kukamilisha ramani hiyo, waiwasilishe kwenye vikao vya ushauri vya Mkoa *(RCC)* kuomba kibali cha Serikali kuidhinisha matumizi yake na miradi mbalimbali ya maendeleo ianze kutekelezwa kulingana na ramani ya Mipango Miji ukiwemo mradi wa ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uwezo wa Serikali kujenga viwanja vya ndege kila Mkoa kwa mara moja ni mdogo. Aidha, Wizara inazingatia ushauri wa Bunge kwamba tuandae miradi ambayo Serikali itakuwa na uwezo wa kuitekeleza katika kila Bajeti. Kinachofanyika sasa ni kutekeleza miradi hii kwa awamu. Mfano kwa sasa miradi ya viwanja vya ndege inayoendelea ni katika viwanja vya Kigoma, Bukoba, Tabora, Mafia, Songwe na Mwanza.

Kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, viwanja vya ndege wa Sumbawanga, Shinyanga na Mtwara vitatekelezwa kwa fedha za mikopo toka benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank (EIB*). Aidha, miradi ya viwanja vya ndege iliyopo katika hatua za awali za utekelezaji ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa viwanja vya ndege 10. Viwanja hivyo ni Iringa, Njombe, Songea, Mtwara, Tanga, Kilwa Masoko, Lindi, Musoma, Singida na Lake Manyara (Karatu). Miradi hii itatekelezwa kupitia *Program* ya kuboresha sekta ya Uchukuzi yaani *Transport Sector Support Programme (TSSP)* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, swali la nyongeza kabisa leo!

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali pamoja na Hospitali ya Haidom inatumia uwanja Haidom kwa muda mrefu sasa na Uwanja huu hauna Taa usiku na hauna Moramu.

Je, kwa mpango wa kushirikiana na watu binafsi yaani *PPP,* serikali ina mpango gani wa kusaidia uwanja huo uweze kutumika kwa kupokea viongozi kama ambavyo inafanyika sasa hivi pamoja na kusafirisha wagonjwa au kupokea wagonjwa usiku?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba viwanja vingi vya Wilayani na maeneo mengine kwa sasa bado havina Taa kiasi cha kuviwezesha kutumika wakati wa usiku. Tunafahamu umuhimu wa hivi Viwanja, na pale inapowezekana kuvipatia huduma hiyo ya Taa ili viweze kutumika usiku, serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, haitasita kufanya hivyo. Suala la kukiwekea Moramu ili kiweze kuwa bora zaidi tunalichukua na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, na maswali ya leo yameisha. Naomba nitoe matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa kamati ya Bunge Katiba Sheria na utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana, anaomba kamati hiyo ikutane ukumbi 219, gorofa la pili Jengo la utawala, wajumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala saa saba mchana ukumbi 219, Jengo la utawala. Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge la Bajeti anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane saa tano asubuhi hii Ukumbi wa Msekwa C. Kamati ya Bajeti, Msekwa C saa tano asubuhi. Kamati ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, anaomba wajumbe wa Kamati wakutane saa saba na robo, Ukumbi 231, Jengo la utawala. Katibu tuendelee!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mwongozo wa Spika!

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora Pamoja na Uratibu na Mahusino**

*(Majadiriano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola ni hao! Tuanze na Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, chini ya Kanuni ya 68(7), wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anajibu swali Namba 56 la Mheshimiwa Richard M. Ndassa, juu ya kuwepo malalamiko ambao wanakatwa asilimia mbili ya mishahara yao bila kuwa wanachama wa *CWT.*

Mheshimiwa Spika, ni Bunge hili mwaka 2004, lilitunga sheria Namba 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini, (*The Employment and Labour Relations Act*) Kifungu 72, Bunge hili, likasema Chama chochote cha Wafanyakazi katika nchi hii, ambacho kimesajiliwa, kikiwa na wanachama zaidi ya 50% ya wanachama wake, *automatically* wale ambao siyo wanachama, watatozwa ada isiyozidi asilimia ile ambayo wanachama wanalipa, kwa ajili ya huduma ya uwakala.

Sheria ilitungwa ili walimu wakifanya majadiliano ya mishahara yao, ambao siyo wananchama watafaidika kutokana na mshahara utakao patikana au kama wanajadiliana kuhusiana na madeni. Sasa leo Waziri anawaminisha Watanzania kwamba walimu hawa wanaonewa, hawajaingia kwenye uanachama, hamwoni kwamba ni kulihalilisha Bunge, linatunga sheria halafu leo,

tunasema walimu wanaonewa. Sasa naomba mwongozo wako kama ni sahihi Waziri kuwambia Walimu kwamba wanaonewa ili hali Bunge hili lilitunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**TAARIFA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nadhani tumesha kuelewa. Sasa Machali unachofanya ni kipya kabisa, sijui kama miongozo nayo ina taarifa! Endelea Mheshimiwa Machali taarifa hiyo!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, kwamba ni kweli hiyo sheria ya Mahusiano Kazini yaani, (*The Employament and Labour Relations Acts, 2004*) inatamka hivyo. Lakini Sheria kubwa na muhimu ambayo inaongoza nchi yetu ni Katiba ya Jamhuri ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania na ndiyo Sheria mama.

Kwa mujibu wa Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kifungu kidogo cha kwanza, kinaweka bayana kwamba, Mtu yeyote hawezi kulazimishwa kwamba ashirikiane na nani. Kifungu kidogo cha (4) kinasema itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na Chama chochote au Shirika lolote. Hii ni kwa mujibu wa Katiba, sasa kinachofanywa leo hii katika Chama cha Walimu.

Mwalimu anaajiriwa halafu analazimishwa kuingia kwenye uanachama, jambo ambalo ni kinyume hata kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Walimu. Nafikiri kifungu kidogo cha (7) au (8) ambacho kina *state* kinasema:- Mtu akukubaliwa uanachama ataorodheshwa katika daftari la kudumu na hivyo kuwa mwanachama wa chama cha Walimu. Tafsiri yake ni nini? Ina maana kuwa mtu amefanya

*application*. Kwa hiyo, hii sheria ya mahusiano kazini, ya mwaka 2004, ina *contradict* na *Constitution* ambayo ndiyo sheria mama. Hapo ndiyo maana walimu wa Manispaa Kigoma Ujiji, Waliamua kukipeleka Chama cha Walimu mahakamani, ili wajiondoe. Nilikuwa naomba eneo hilo kama halielewi!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, muongozo wangu katika hili upo moja kwa moja kwa sababu tupo katika kipindi cha Bajeti za Wizara mbalimbali, wakati wa Wizara ya Elimu itakapofikia mjadara wake hapa, litakuwa ni moja ya jambo ambalo limetolewa ufafanuzi. Mheshimiwa Halima J. Mdee!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi natumia kanuni hiyo hiyo ya 68(7) kuomba Mwongozo wako, lakini vilevile ninarejea, Kanuni ya 99, Kanuni ya 100. Kanuni ya 101 (4) Kanuni ya 103 (2). Hoja yangu hasa, inahusiana na ufanisi wa uendeshaji bora shughuli za Bunge. Nazungumza hili kwa sababu imetokea jana na inaweza ikaendelea kama tusipochukua maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba, kipindi pekee ambacho Wabunge wanakuwa na fursa ya kuhoji kuhusu masuala ya kisera, ambao Mawaziri hawajapatia majibu ni wakati wa Kamati ya Matumizi. Sasa tumeona Kamati ya Matumizi imatengewa dakika 25 peke yake, kwa mantiki ya kuhoji suala la sera. Sasa tafsiri yake ni kwamba Mawaziri wakati wanajibu, mwakijua kabisa fursa pekee ya kuhoji sera wanatakiwa watu 5 na kwa mgawanyo ambao tumeugawa, kutokana na *proportionality* na mabadilisho ya Kanuni tuliyoyafanya, matokeo yake ni kwamba, hoja za msingi zinatakiwa zijadiliwe na watu ama 3 kutoka Chama cha Mapindizu ama mmoja (1) kutoka CHADEMA au Mmoja (1) kutoka *CUF* sasa matokeo yake ni

nini? Matokeo yake ni kwamba Mawaziri wanajibu hoja, kiwepesi ama kwa kupotosha. Wakijua kabisa hakuna hoja ya kusimama kupingana nao.

Kama ilivyotokea jana kwa Waziri Mkuu. Sasa mimi nilikuwa nataka Mwongozo wako, kwa sababu nafasi pekee ya kuhoji ni katika Kamati ya Matumizi, ndiyo tunaweza tukaondoa shilingi ambayo imeruhusiwa Kikanuni lakini jana umetuambia unahoji dakika 5, ukijibiwa vitu vya hovyo hovyo, fursa ya kutoa shilingi haipo, Mawaziri wanafanya kama wanavyotaka.

Sasa mimi nataka Mwongozo wako. Busara ya kiti chako, hasa ukizingatia kwamba, Kanuni zipo na vipengele vya Kanuni vinaweza vikatenguliwa kwa maslahi ya nchi. Unaonaje kiti chako kwa kushauriana na Kamati husika kitoe maelekezo sahihi ili basi Bunge letu litendee haki, wananchi kwa kukaa hapa na kujadili mambo ya msingi na siyo kufanya sanaa. Kwa sababu tunacho kifanya hapa ni mchezo wa kuigiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima J. Mdee na hilo nalo nilitolee mwongonzo moja kwa moja, halihitaji kusubiri. Kwamba, ni matokeo ya maelekezo ya Kamati ya Kanuni na yote hayo yako ndani ya Kanuni. Kwamba muda ule wa wakati wa Kamati ya Matumizi wa kuhoji masuala ya sera kwa Waziri, kufanya kwa uwiano, ule ambao mmedai kwa muda wote kwa usawa. Kwa hiyo, usawa huo, ukatenga dakika 25, kwa ajili ya zoezi hilo la sera.

Katika usawa huo huo mmegawa nafasi hizo kwa Wabunge watano kwa dakika tano tano. Kwa wastani wa kwamba, wataongea Wabunge, ama watatu wa CCM,

mmoja wa CUF, mmoja wa CHADEMA na kama kutakuwepo wa *TLP, UDP* na *NCCR - Mageuzi,* basi wanaweza kuchukua nafasi moja wapo katika zile tatu za CCM. Kwa hiyo, CCM ikawa na mbili na vile vyama vingine vikawa na moja.

CHADEMA moja na *CUF* moja. Sasa hili lilitokana na hoja zenu ninyi wenyewe za kutaka mgawano sawa kwa kila jambo hapa ndani. Lakini niseme kwamba Kamati ya Kanuni ni wajumbe ambao wako humu ndani, wamesikia, watalichukua, watazidi kuangalia namna bora zaidi ya kulifanya jambo hili kwa sababu liko kwenye Kanuni, ni vigumu sana kwa kiti kufanya kinyume na kile kitu ambacho kiko kwenye Kanuni kwa hivi sasa. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahasante sana. Bunge letu linatizamwa na wananchi Tanzania nzima, mijini na vijijini.

Pia linasikilizwa na wananchi Tanzania nzima, Mjini na Vijijini. Sasa nimepokea ujumbe kutoka kwa wananchi wakilalamika matumizi ya Lugha ndani ya Bunge letu, wakati wanajibu maswali, wanachanganya Kingereza na Kiswahili. Jambo ambalo baadhi ya Wananchi wanashindwa kufuatilia.

Sasa naomba Mwongozo wa kiti chako, nikitambua kwamba lugha ya hapa Bungeni ni Kingereza na Kiswahili, lakini katika kujibu maswali ambayo tunahitaji wananchi wapate majibu kwa ufasaha ni nini kifanyike? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hilo pia Mheshimiwa Joseph R. Selasini nilipokee, ni ushauri wa jumla. Kwa kweli, katika matumizi ya Lugha, katika Bunge letu. Kingereza kinaruhusiwa na Kiswahili kinaruhusiwa. Ndiyo maana tunapata miswada hapa imeandikwa kwa Kingereza. Lakini kwa kadiri iwezekanavyo, tujitahidi, Waheshimiwa wote wala siyo Mawaziri peke yake, kutumia lugha ya Kiswahili kadiri inavyowezekana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo ninaomba niwape ufafanuzi kidogo kuhusu shughuli yetu ya leo ambayo kama mtaangalia *Order Paper* yetu ya leo na Katibu ameshatusomea hapa, kuhusiana na hoja za Serikali. Ni kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisa Makadirio ya Matumizi ya ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Uratibu na Mahusian, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Sasa tumepangiwa siku mbili za shughuli hii, katika siku hizi mbili, leo siku ya kwanza tutakuwa na Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Celina O. Kombani na Mheshimiwa Stephen M. Wasira, ambao watawasilisha hotuba zao kila mmoja kwa kadiri ya Kanuni labda kama watabakiza dakika kwa ajili ya meza, lakini wanayo saa moja moja kila mmoja wao.

Wenyeviti wa Kamati wawili watawasilisha hapa hotuba zao. Kwa hiyo, kila Mwenyekiti ana nusu saa, kwa hiyo watachukua saa moja kamili. Wasemaji wa Upinzani watakaowasilisha hapa mbele ni wawili pia na kila mmoja ana nusu saa. Kwa hiyo, naomba uwelewa wenu na ushirikiano wenu katika zoezi zima.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Celina O. Kombani, yeye wamegawana na Mheshimiwa Waziri Stephen M. Wasira muda wao kwa dakika 75 kwa 45. Mheshimiwa Celina O. Kombani! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Tume ya Mipango (Fungu 66) na Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 9), Bunge lako sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2012/13. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala; pia ninampongeza Mheshimiwa William Mganga Ngeleja (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote walioteuliwa katika Kamati hiyo. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa kwenye Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu katika zoezi lililofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2012/13 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/14, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu. Chini ya uongozi wake, Serikali

imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa Wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake, yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na Washirika wa Maendeleo kuona umuhimu wa kuendelea kuiunga mkono Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Billal, kwa uongozi wake bora. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Hotuba yake aliyoitoa kwenye Bunge lako Tukufu wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2013/14 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na imeonesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2013/14. Ningependa pia kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb), kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha katika Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nampongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu; Mheshimiwa Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora; na Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum, kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Aidha, nawashukuru Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bwana Peter Alanambula Ilomo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu;

Bwana HAB Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bibi Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais; Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake, ambao wamefanya kazi kubwa katika kuwezesha hotuba hii kukamilika kwa wakati. Nawashukuru pia Wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa pole kwako binafsi, Bunge lako pamoja na jamaa na familia ya Mbunge aliyefariki dunia wakati wa Vikao vya Kamati ya Mambo ya Nje vya kujadili Bajeti za Wizara, Marehemu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani. Aidha, natoa pole kwa Watanzania wenzangu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki, yakiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 Jijini Dar es Salaam na machimbo ya changarawe Mkoani Arusha. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuzishukuru Nchi na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio tuliyopata. Hivyo, nachukua nafasi hii kuzishukuru Nchi hizo na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ifuatavyo: Australia, China, Indonesia, Finland, Brazil, India, Italia, Japan (*JICA*), Korea ya Kusini (*KOICA*), Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza (*DFID*), Ujerumani (*GTZ*), Uswisi, Marekani (*USAID*), Ireland, Israel, Canada (*CIDA*), Denmark (*DANIDA*), Norway (*NORAD*), Sweden (*SIDA*), Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan *(Japanese Social Development Fund), UNDP* na *OPEC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu itazungumzia

maeneo matatu ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2012/13; Mpango wa Utekelezaji wa mwaka 2013/14 na Maombi ya Fedha kwa mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2012/13, umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kazi zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake, katika mwaka 2012/13, Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, ilitengewa jumla ya Shilingi 9,146,327,000 (Fungu 20) na Shilingi 217,100,430,000 (Fungu 30), kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 50,382,037,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2013 Shilingi 6,729, 551,638 (Fungu 20) na Shilingi 176,832, 510,433 (Fungu 30) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya Shilingi 42,185, 855,677 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu, imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2012 hadi Machi, 2013, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe wasikivu tumsikilize Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2012 hadi Machi, 2013, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma kwa Rais na familia yake zilitolewa;

(ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo

mbalimbali kama vile Uchumi, Siasa, Jamii, Sheria, Mahusiano ya Kimataifa zilitolewa;

(iii) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo Nyaraka 70 zilichambuliwa, mikutano 17 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*IMTC*) ilifanyika na Nyaraka 45 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 16 ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na Nyaraka 36 zilifanyiwa uamuzi. Mikutano sita ya Kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika na ajenda 13 zilijadiliwa. Mikutano minne ya Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo Miswada minne ilichambuliwa.

(iv) Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Pili ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ilikamilika mwezi Septemba, 2012. Matokeo ya tathmini hiyo ni kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika Sekta ya Umma. Aidha, matokeo haya yatatumika katika maandalizi ya Mpango wa Awamu ya Tatu *(NACSAP III);*

(v) Mafunzo ya Utawala Bora na njia za kupambana na Rushwa kwa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi 48 Ikulu, Mawakili wa Serikali 60 na Wajumbe 80 wa Kamati za Uadilifu kutoka Wizara zote, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali yalifanyika;

(vi) Katika Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(Open Government Partnership*), Serikali kupitia Wakala ya Serikali Mtandao imekamilisha uanzishwaji wa Tovuti ya Wananchi (*Citizen Portal*) itakayotoa taarifa kwa Wananchi kuhusu namna ya kupata huduma mbalimbali zitolewazo na Serikali na Taasisi zake;

(vii) Taarifa za nusu mwaka za utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi katika Sekta za Afya, Maji na Elimu zimetolewa na kuonesha utekelezaji mzuri wa mpango katika Sekta hizo. Aidha, Mpango huo umewekwa kwenye Tovuti kwa ajili ya rejea kwa Wananchi ambayo ni *www.opengov.go.tz.;*

(viii) Rufaa 45 za Watumishi wa Umma zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais kwa uamuzi. Aidha, malalamiko 120 ya Watumishi wa Umma na Wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Rais au Katibu Mkuu Kiongozi. Vilevile, mkutano wa kueleweshana kuhusu usimamizi na utawala wa masuala ya Utumishi wa Umma ulifanyika ambapo Watendaji na Mawakili 40 wa Serikali walishiriki;

(ix) Taarifa jumuishi ya utekelezaji wa Programu za Maboresho kwa mwaka 2011/12 na taarifa tatu za robo mwaka za utekelezaji wa Programu nane za Maboresho zilichambuliwa kwa utekelezaji. Taarifa zimeonesha kuwa utekelezaji kwa ujumla umekuwa wa wastani;

(x) Vikao vinne vya Maboresho vilivyoshirikisha Makatibu Wakuu, Waratibu wa Programu za Maboresho katika Wizara na Washirika wa Maendeleo vilifanyika na vilijadili maendeleo na changamoto katika utekelezaji wa maboresho. Baadhi ya changamoto ni pamoja na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha na kupungua kwa misaada ya Washirika wa Maendeleo na hivyo kuathiri utekelezaji wa maboresho yaliyokusudiwa;

(xi) Tathmini ya kitaifa ya utekelezaji wa maboresho itakayobainisha mafanikio na fursa zilizopo kwa lengo la kujenga misingi ya maboresho yatakayokabiliana na changamoto za sasa na baadaye inaendelea. Tathmini hii inatarajia kukamilika mwezi Mei, 2013 na itatumika katika kuandaa mkakati ujao wa Maboresho;

(xii) Mkakati wa kupambana na kuenea kwa Virusi vya UKIMWI na UKIMWI mahali pa kazi uliandaliwa;

(xiii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa na *TASAF* na MKURABITA ulifanyika katika Mikoa ya Simiyu, Geita, Mwanza, Njombe, Mbeya, Singida na Morogoro. Aidha, uratibu wa Awamu ya Tatu ya *TASAF* ulifanyika na kukamilika;

(xiv) Mikutano mitatu ya kuelimishana kuhusu kuheshimiana na kuvumiliana katika imani za kidini kwa lengo la kudumisha amani ya nchi ilifanyika baina ya Serikali na Viongozi wa Dini mbalimbali katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza;

(xv) Mikutano miwili baina ya Serikali na Viongozi wa Dini mbalimbali katika Mikoa ya Geita na Mwanza ilifanyika kwa lengo la kupata suluhisho katika mgogoro wa uchinjaji wanyama. Serikali bado inaendelea na jitihada za usuluhishi wa mgogoro huu ili kuona namna bora ya kuumaliza;

(xvi) Kazi ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano Ikulu imeanza ambapo ujenzi wa msingi umekamilika. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2013; na

(xvii) Ukarabati mkubwa wa Ikulu Ndogo ya Tanga umefanyika na kukamilika. Aidha, matengenezo ya kawaida ya Jengo la Ikulu na makazi ya Rais yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura Namba 329, jukumu kubwa la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni kuelimisha umma juu ya rushwa na athari zake katika jamii na mbinu za kupambana na rushwa nchini, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya kisheria na kuishauri Serikali namna bora ya kuziba mianya ya rushwa. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Tuhuma 2,936 zilichunguzwa ambapo tuhuma 516 uchunguzi wake ulikamilika na majalada 218 yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuomba kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Majalada 165 yalipata kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka na kesi zilifunguliwa mahakamani zikiwemo 18 zilizotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kesi nane zilizohusu Maliasili na

kesi saba zilizohusiana na uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo;

(ii) Majalada manne yaliyohusu tuhuma za rushwa kubwa *(Grand Corruption)* yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Majalada yote manne yamepata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani;

(iii) Kesi 578 ziliendeshwa mahakamani, kati ya kesi hizo kesi 495 zinaendelea kusikilizwa mahakamani na kesi 79 zilitolewa maamuzi. Aidha, kesi 33 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuadhibiwa, kesi 5 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali na kesi 41 watuhumiwa wake waliachiwa huru;

(iv) Kupitia vyanzo mbalimbali vya taarifa, kiasi cha Shilingi 4,313,723,189.55 kiliokolewa zikiwemo Shilingi 3,881,036,644.00 za malipo ya walimu yasiyo halali kutoka katika Halmashauri mbalimbali nchini na kiasi kilichobaki cha Shilingi 432, 686,545.55 zilitokana na chunguzi mbalimbali zilizofanyika;

(v) Tafiti tatu zenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti zimefanyika katika maeneo ya usimamizi wa bidhaa ambazo ni chumvi ili kubaini uwepo wa madini joto. Aidha, tafiti pia zilifanyika katika bidhaa za petroli na gesi na utoaji huduma katika Bandari ya Dar es Salaam;

(vi) Warsha 20 za wadau za kujadili matokeo ya tafiti mbalimbali na kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa zilifanyika;

(vii) Kazi 110 za udhibiti wa haraka (*quick-wins*) wa malalamiko ya wananchi zilifanyika na kazi 11 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo zimefanyika katika Sekta za Elimu, Kilimo, Siasa, Bima, Fedha, Kazi, Habari, Maji, Mifugo, Ardhi, Afya, Maliasili na Utalii, Mahakama, Ujenzi, Ushirika na Masoko na Sekta Binafsi. Maeneo mengine yaliyohusishwa ni Polisi, *TANROADS* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(viii) Elimu kuhusu rushwa na athari zake ilitolewa kupitia njia mbalimbali za uelimishaji ikiwemo semina 1,675, mijadala ya wazi 137, midahalo 40, kazi mradi 201, ufunguzi wa Klabu 56 za Wapinga Rushwa, uimarishaji wa klabu 1120, vipindi vya radio 150, vipindi tisa vya televisheni, mikutano 522 ya hadhara, maonesho 61, makala 89, matangazo 321 ya redio na televisheni, mikutano 14 na waandishi wa habari, taarifa 50 kwa vyombo vya habari, shughuli 37 za kijamii na machapisho 121,068;

(ix) Wajumbe 50 wa Kamati za Maadili za Idara na Wakala tisa (*TACAIDS*, *MSD*, *PSPTB, TCRI, TPS, TAWIRI, TTCL, RITA* na *TPA*) walishiriki mafunzo juu ya matumizi ya nyenzo zitakazowezesha katika kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili katika sehemu zao za kazi;

(x) Wajumbe 55 wa Kamati za Maadili kutoka katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara, Kigoma, Simiyu na Shinyanga walishiriki mafunzo juu ya matumizi ya nyenzo zitakazowezesha katika kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili katika Serikali za Mitaa wanazofanya kazi. Aidha, mafunzo ya Wakuu wa TAKUKURU kutoka Wilaya zilizopo Mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Morogoro, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Lindi, Mtwara Ruvuma na Iringa yalifanyika;

(xi) Wajumbe 121 kutoka katika Mashirika 95 ya Kidini walishiriki mafunzo juu ya matumizi ya nyenzo zitakazowezesha katika kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili, wajibu na umuhimu wa mashirika ya dini katika mapambano dhidi ya rushwa. Wajumbe walitoka Mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Mbeya, Rukwa, Ruvuma na Katavi;

(xii) Kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma lilifanyika kongamano ambalo wadau 121 walihudhuria. Lengo la kongamano hili lilikuwa kuimarisha na kusisitiza umma umuhimu wa maadili ambayo ni nguzo

muhimu ya mapambano dhidi ya rushwa na kuelewesha umma madhara na athari za rushwa;

(xiii) Maadhimisho ya Siku ya Maadili katika ngazi ya Kitaifa yalifanyika kuanzia tarehe 5 hadi 10 Desemba, 2012. Washiriki 1,128 walitembelea mabanda ya maonesho wakati wa maadhimisho hayo;

(xiv) Vijana waliendelea kujengwa kimaadili kupitia Klabu za wapinga rushwa zinazofunguliwa na kuimarishwa kupitia semina, elimu ya uraia, midahalo, bonanza na Kazi Mradi. Kongamano la vijana na walimu walezi zaidi ya 330 kutoka Klabu za wapinga rushwa Shule za Sekondari Mkoa wa Dar es Salaam lilifanyika Februari, 2013; na

(xv) Ujenzi wa Ofisi katika Mikoa ya Ruvuma na Tabora pamoja na Wilaya za Kasulu na Newala uko katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Mbeya na Mara umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kubwa la Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini. Kwa sasa MKURABITA uko katika Awamu ya Tatu ya utekelezaji ambapo katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 imepitiwa upya ili kubainisha na kuoanisha marekebisho yanayohitajika kwa kuzingatia maboresho yaliyopendekezwa na MKURABITA. Kikao cha wadau kinaandaliwa kwa ajili ya kupata maoni yao juu ya maboresho yaliyoainishwa. Aidha, kuhusu maboresho ya biashara, kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Makampuni juu ya uanzishaji wa kampuni ya mwanahisa mmoja yenye dhima ya ukomo zimeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara;

(ii) Kujenga uwezo kuhusu urasimishaji wa ardhi

vijijini kwenye Halmashauri tatu za Wilaya Tanzania Bara (Misungwi, Uyui na Ngara) katika vijiji viwili kila Wilaya na Zanzibar katika Shehia za Chokocho na Nungwi. Jumla ya mashamba 5,330 yalipimwa. Hati za Hakimilki za Kimila 3,336 ziliandaliwa na taratibu za uhakiki na usajili zinafanyika. Kwa upande wa Zanzibar mashamba 2,250 yamehakikiwa na kati ya hayo, mashamba 1,600 yamepimwa. Urasimishaji utaendelea katika Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Tandahimba na Kiteto kuanzia Aprili, 2013. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Juni, 2013;

(iii) Maafisa 32 kutoka Halmashauri za Wilaya za Uyui, Misungwi na Ngara; Maafisa 24 wa Kata na Maafisa 77 wa Vijiji walipatiwa mafunzo juu ya Sheria za Ardhi na Urasimishaji. Vilevile, vifaa kumi vya upimaji *(hand held GPS - Global Positioning System),* kompyuta mbili, printa moja, Kamera mbili na *laminating mashine* moja viligawiwa katika Halmashauri za Wilaya hizo. Sambamba na utoaji wa vifaa, maabara za kutengeneza Hati za Hakimilki za Kimila *(GIS – Geographical Information System laboratory)* katika kila Halmashauri zimeanzishwa ili kurahisisha kazi ya kutengeneza Hati hizo;

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji 19 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe vimefanyiwa urasimishaji wa mashamba ya chai. Mashamba 1,891 yalihakikiwa na kupimwa na hati 1,579 zilikamilika. Aidha, kazi ya upimaji wa mashamba ya chai katika Halmashauri za Wilaya ya Njombe na Mufindi inaendelea na jumla ya mashamba 7,540 yamepimwa na Hati za Hakimilki za Kimila 6,530 zimeandaliwa tayari kwa uhakiki na usajili na hatimaye kutolewa kwa wamiliki;

(v) Kazi ya ufuatiliaji wa uandaaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila katika Halmashauri 15 za Wilaya ilifanyika sambamba na ujenzi wa masjala. Jumla ya Hati 10,183 za Hakimilki za Kimila ziliandaliwa na kati ya hizo 9,191 zilichapishwa na kazi ya uhakiki usajili na utoaji wa hati hizo kwa wamiliki inaendelea katika Halmashauri za Wilaya husika. Halmashauri hizo ni Masasi, Mkuranga, Meru, Mwanga, Moshi,

Geita, Kasulu, Muleba, Kahama, Sikonge, Mbarali, Sumbawanga, Mbinga, Rufiji na Bunda;

(vi) Kazi ya utayarishaji na utoaji wa Hati Miliki mijini inaendelea katika eneo la Maporomoko ya Mji wa Tunduma Halmashauri ya Wilaya ya Momba na eneo la Kimara Baruti Manispaa ya Kinondoni. Ramani za Mipango Miji zimetayarishwa na kuidhinishwa tayari kwa ajili ya uandaaji wa hati;

(vii) Urasimishaji wa Ardhi Mijini umeanza katika maeneo ya Mwangata A na B, Kyodombi A na B na Isoka A katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ambapo jumla ya viwanja 702 vimepimwa. Aidha, urasimishaji ardhi mijini umefanyika katika eneo la Welezo Mjini Zanzibar na jumla ya viwanja 2,500 vimepimwa. Urasimishaji unatarajiwa kuendelea katika Halmashauri za Miji ya Babati na Manispaa ya Moshi kuanzia Aprili, 2013;

(viii) Urasimishaji wa biashara umefanyika katika Jiji la Mbeya na katika Manispaa ya Morogoro. Katika Jiji la Mbeya, mafunzo yametolewa kwa wafanyabiashara 790, kati yao waliosajili majina ya biashara *BRELA* ni 250; waliofungua akaunti benki 200; na waliopata leseni za biashara kutoka Manispaa ya Mbeya ni 768. Katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro jumla ya wafanyabiashara 780 walipata mafunzo na wafanyabiashara 240 walisajili majina ya biashara. Mchakato wa utoaji leseni unaendelea;

(ix) Ujenzi na ukarabati wa Masjala za ardhi za vijiji uliendelea katika vijiji vya Wilaya mbalimbali nchini na ujenzi uko katika hatua mbalimbali. Vijiji vinavyohusika na ujenzi huu vimo katika Halmashauri za Wilaya za Moshi, Mwanga, Meru, Nachingwea na Mpwapwa;

(x) Kazi ya kuratibu uimarishaji wa mifumo ya Kitaasisi inaendelea ikijumuisha mchakato wa kuanzisha Chombo cha Kitaifa cha Urasimishaji wa Rasilimali Ardhi na Biashara nchini pamoja na taratibu za Kurahisisha Mifumo ya

Kodi na Utunzaji wa kumbukumbu kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati;

(xi) Utaratibu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Urasimishaji katika ngazi ya Wilaya unaendelea. Hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kukabiliana na tatizo la ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya urasimishaji. Mpango huu umeanza kwa majaribio katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ambako jumla ya Shilingi 25,000,000 zilizochangwa na Wananchi katika eneo la Idundilanga zimetumika katika urasimishaji wa ardhi katika eneo la Kambarage; na

(xii) Katika jitihada za kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano MKURABITA imeendesha kikao cha wadau Tanzania Bara na Visiwani kwa ajili ya kuendelea kuwahabarisha wadau juu ya shughuli zinazoendelea. Wadau walitoa maoni mbalimbali likiwemo lile la uanzishwaji wa Chombo cha Kitaifa kitakachosimamia shughuli zote za urasimishaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* unatarajiwa kukamilika Juni, 2013. Kutokana na kukamilika kwa awamu hii, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, imetayarisha Awamu ya Tatu ya *TASAF* ambayo utekelezaji wake ulianza mwezi Agosti, 2012 na itatekelezwa katika kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 ni kama ifuatavyo:-

(i) Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 15 Agosti, 2012 Mjini Dodoma;

(ii) Miradi mipya ya jamii 484 yenye thamani ya Shilingi bilioni 20.0 ilitekelezwa kutoka Halmashauri zote za Tanzania Bara, Unguja na Pemba, ikiwa ni jitihada za

kuboresha huduma za jamii na kuongeza kipato cha walengwa katika maeneo ya utekelezaji wa miradi;

(iii) Mpango wa Jamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Masikini umeendelea katika Halmashauri za majaribio za Bagamoyo, Chamwino na Kibaha. Jumla ya walengwa 28,691 wamenufaika na mpango huu na jumla ya Shilingi bilioni 3.21 zimehawilishwa kwa walengwa;

(iv) Maandalizi ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kukusanya takwimu za awali kwa ajili ya tathmini ya Awamu ya Tatu ya *TASAF* yapo katika hatua za mwisho ambapo Mshauri Mwelekezi ataanza kazi kabla ya Juni, 2013;

(v) Mafunzo ya kujenga uwezo wa ujasiriamali kwa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza yaliendelea kutolewa kwa Vikundi 1,778 vyenye wanachama 22,712 katika Halmashauri za Wilaya 44 zikiwemo Unguja na Pemba kwa lengo la kuviimarisha ili shughuli zake ziwe zinafanyika kwa ufanisi zaidi;

(vi) Mifumo ya taarifa za uendeshaji iliboreshwa kwa kufanya marekebisho na kujenga mifumo mipya inayoendana na mahitaji ya Awamu ya Tatu. Mchakato wa kuwapata Washauri Waelekezi unaendelea na mifumo hiyo itakamilika ifikapo Agosti, 2013. Mifumo hiyo itajikita zaidi katika matumizi ya Kompyuta ili kutunza kumbukumbu za kaya maskini na shughuli za utekelezaji wa Mpango kwa ujumla;

(vii) Wananchi walijengewa uelewa kuhusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa Miradi kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwa ni pamoja na mikutano katika ngazi ya jamii, warsha kwa Viongozi katika ngazi za Halmashauri na Mikoa ambazo zilihudhuriwa na Wakurugenzi na Wenyeviti wa Halmashauri, Maafisa Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Idara na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(viii) Vipindi 64 vya televisheni na vipindi 20 vya redio ambavyo vililenga katika kutoa elimu kuhusu utekelezaji

wa miradi ya jamii na Mpango wa *TASAF* Awamu ya Tatu vilirushwa hewani;

(ix) Mkakati wa Mawasiliano umeandaliwa ambao unatoa dira ya shughuli za upashanaji habari ili kuwezesha jamii kuufahamu vizuri Mpango huu na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa shughuli zake;

(x) Ukaguzi wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Jamii kwa kila robo mwaka ulifanyika ili kujiridhisha na matumizi ya fedha na ubora wa Miradi inayotekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya sekta husika. Matokeo ya ukaguzi huu yalisaidia kuboresha usimamizi wa fedha na ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa ujumla;

(xi) Tathmini tano zilifanyika ili kubaini hatua zilizofikiwa katika kuondoa umaskini kwa walengwa. Matokeo ya tathmini hizo yanaonesha kuwepo kwa manufaa chanya kwa walengwa na jamii kwa ujumla; kwa mfano, katika baadhi ya vijiji hakuna watoto kutoka kaya za walengwa wenye utapiamlo mkali. Aidha, huduma za jamii zimeboreshwa na kipato cha walengwa kimeongezeka. Kwa ujumla, matokeo ya tathmini iliyopima kiwango cha kuridhika na huduma zitolewazo na *TASAF* yameonesha kuridhika kwa zaidi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uongozi ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 274 la mwaka 2010, kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalam wa hali ya juu *(Centre of Excellency)* cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Lengo kuu ni kuimarisha uwezo wa Viongozi kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza *(Emerging Leaders)* wakiwemo wanasiasa, Watumishi wa Serikali na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kozi nne za muda mfupi zilifanyika ili kuwapa viongozi ujuzi na mbinu mpya kwa nia ya kuwajengea uwezo na weledi katika utendaji wao, kama viongozi wa mabadiliko. Kozi hizo ni: Kuzungumza Katika Hadhara kwa Naibu Mawaziri 16 wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kuandika Hotuba na Kutoa Taarifa kwa Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi 58; Menejimenti Inayozingatia Matokeo kwa Makatibu Tawala wa Wilaya 55; Uongozi Katika Bodi za Mashirika ya Umma kwa Wakurugenzi na Wenyeviti wa Bodi za Mashirika ya Umma 27.

(ii) Semina Elekezi kwa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya 24 wa Mkoa wa Pwani ilifanyika Julai, 2012. Semina ililenga kuleta uelewa wa pamoja kwa Viongozi wa Mkoa wa Pwani ili kukuza utendaji wa ushirikiano;

(iii) Utafiti juu ya Tathmini ya Hali ya Utawala Bora katika Taasisi za Umma Tanzania umefanyika na kukamilika. Utafiti huo umeonesha kuna upungufu katika eneo la utawala bora hususan kwenye sheria na mifumo iliyopo ya kiutawala;

(iv) Vipindi vitano vya Mahojiano vilifanyika na kurushwa kwenye Televisheni ya Taifa kwa nia ya kujifunza na kubadilishana mawazo kutokana na uzoefu wa Viongozi waliopita na waliopo kama mfano wa kuigwa na Viongozi wanaochipukia. Viongozi hao ni Rais Mstaafu wa Finland - Mheshimiwa Martti Ahtisaari, Rais Mstaafu wa Ireland - Mheshimiwa Mary Robinson na Rais Mstaafu wa Namibia - Mheshimiwa Sam Nujoma, Rais Mstaafu wa Afrika ya Kusini - Mheshimiwa Thabo Mbeki na Rais Mstaafu wa Ghana - Mheshimiwa John Kufuor;

(v) Mikutano mitatu ya majadiliano kuhusu Utawala Bora katika Mashirika ya Umma; Uongozi wa Kimkakati kwa Afrika Mpya; na Ubia wa Mafanikio Kati ya Sekta ya Umma na Sekta ya Binafsi ilifanyika kwa lengo la kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu; na

(vi) Machapisho matano yameandaliwa kuhusu

Usimamizi Makini wa Chaguzi katika Bara la Afrika; Usimamizi Bora wa Maliasili Barani Afrika; Tathmini ya Hali ya Utawala Bora katika Taasisi za Umma Tanzania; Ubia wa Mafanikio Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; na Athari za Kimazingira Zitokanazo na Maendeleo ya Sekta ya Nishati Tanzania. Lengo la machapisho hayo ni kusambaza taarifa na maarifa yaliyopatikana kutokana na tafiti na majadiliano.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF)* ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfuko ulitoa mafunzo kwa wateja wa mikopo ya nyumba na Wajasiriamali wa Kibaha, Morogoro na Turiani. Mafunzo hayo yalihusu utunzaji wa kumbukumbu na mbinu za kukuza mitaji; na

(ii) Mfuko uliendesha mafunzo kwa wafanyakazi wake ili kuwajengea uwezo na kuwaandaa kwa muundo mpya. Mafunzo hayo yalihusu taratibu mpya za kutoa mikopo, mbinu za kupata vikundi bora vya Wajasiriamali, huduma kwa wateja na utunzaji kumbukumbu na uandaaji ripoti kwa kutumia mfumo mpya wa *CRDB Finance Solution.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake ili kutekeleza majukumu yake, ilitengewa Shilingi 42,431,553,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu haya. Kati ya fedha hizi, Shilingi 20,021,986,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 22,409,567,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2013 kiasi cha Shilingi 17,390,524,650 za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya Shilingi 19,779,504,000 zimepokelewa na kutumika. Kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika ni sawa na asilimia 88 ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa, Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na kwamba, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa Wananchi wanapotoa huduma mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeendelea kusimamia ajira katika Utumishi wa Umma ambapo vibali vya kuajiri watumishi wapya 31,246 kati ya nafasi za watumishi wapya 56,746 vimetolewa. Katika mwaka wa fedha 2012/13, walimu 19,430 waliajiriwa kati ya walimu 28,746 waliokuwepo katika kibali kilichotolewa na Ofisi hii. Vibali vya ajira mbadala 576 vimetolewa. Aidha, utaratibu wa kuwapandisha vyeo Watumishi wa Umma unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo pamoja na Taasisi na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa, imeendelea kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wake ambapo jumla ya Watumishi wa Umma 2,085 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 13 zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Kurithishana Madaraka na zimeanza utekelezaji wake. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 15 zimewezeshwa kuandaa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na Mipango ya Mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha masilahi ya Watumishi wa Umma kwa kuzingatia Sera ya Malipo ya Mshahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010) na ukuaji wa uchumi na ongezeko la Pato la Taifa.

Katika mwaka wa fedha 2012/13 kima cha chini cha mshahara kwa Watumishi wa Umma kimeongezeka kutoka Shilingi 150,000 (2011/12) hadi Shilingi 170,000 kwa mwezi. Ongezeko hilo ni asilimia 13.3. Aidha, hatua mbalimbali za kuboresha masilahi ya watumishi zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya uwiano wa mishahara kati ya watumishi wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma, kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa 33 zilizobainishwa kuwa na mazingira magumu ya kazi kuhusu kuandaa miongozo ya utoaji wa Motisha kwa watumishi wao. Hadi sasa Halmashauri za Wilaya 29 kati ya 33 zimewasilisha Miongozo ya Utoaji Motisha kwa watumishi wake wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu. Lengo la Serikali ni kupunguza na hatimaye kuondoa hali inayosababisha ugumu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu ya vyombo vya usafiri na samani za nyumbani kwa watumishi wa umma pamoja na kuandaa utaratibu wa kuwauzia nyumba watumishi kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambapo Wanachama wa Mifuko hiyo watalipa kidogokidogo. Mifuko hii ni pamoja na *PSPF* ambayo tayari imejenga nyumba 641 katika Mikoa ya Dar es Salaam (491), Morogoro (25), Mtwara (50), Shinyanga (50) na Tabora (25). Pia Watumishi wa Umma wameendelea kudhaminiwa na Serikali kupata mikopo katika Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma. Hadi kufikia Machi, 2013 jumla ya madai ya Watumishi wa Umma 11,820 kati ya watumishi 52,039 wamelipwa malimbikizo ya Mishahara na kiasi cha Shilingi 12,603,190,843 kimetumika. Malipo ya malimbikizo ya watumishi 27,245 yenye thamani ya Shilingi 16,089,986,605 yalikuwa yameshahakikiwa na yanasubiri kufanyiwa malipo kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 12,974 yenye thamani ya Shilingi 12,588,847,207 yalikuwa kwenye hatua ya uhakiki kabla ya kuingizwa katika mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Umma wameendelea kushirikishwa katika masuala yanayowahusu kupitia Mikutano ya Mabaraza ya Wafanyakazi sehemu za kazi, Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma, Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta katika Utumishi wa Umma na Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi kwa kuhuisha mifumo, miundo na taratibu za utendaji kazi kwa lengo la kuimarisha utendaji unaojali matokeo, ufanisi na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma 150 kutoka katika Wizara 15 kuhusu Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini, kuandaa mwongozo wa kuratibu na kuwianisha matumizi na shughuli zote za Teknolojia, Habari na Mawasiliano Serikalini na kuusambaza kwa wadau ambao ni Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, Miundo na Mgawanyo wa majukumu ya Wizara tano za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imehuishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha utunzaji, uhifadhi na udhibiti wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuweka mifumo na kutoa mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 23 kutoka Tanzania Bara na Wizara tano za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha kutunza kumbukumbu Tuli kilichopo Dodoma umekamilika. Kituo hicho kimeongeza uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka kutoka makasha 200,000 hadi 700,000 ambayo ni ongezeko la asilimia 250. Kituo hiki pia kina uwezo wa kutumia mifumo ya kielektroni katika kuhifadhi kumbukumbu zinazozalishwa na mifumo hiyo. Ufuatiliaji na tathmini ya utunzaji wa kumbukumbu umefanyika katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 27 katika mikoa mitano ambayo ni Njombe, Morogoro, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Maadili

umefanyika katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 15, ambazo ni: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Tume ya Utumishi wa Umma; Sekretarieti ya Ajira; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Maji; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Kazi na Ajira; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wakala ya Usajili wa Leseni za Biashara; na Mamlaka ya Chakula na Dawa. Matokeo ya ufuatiliaji huo yalionesha kuwa kati ya Mashauri ya Kinidhamu 38 yaliyojitokeza katika kipindi cha Julai - Novemba, 2012, Mashauri 34 yalishughulikiwa na kuhitimishwa. Pia tathmini ya kiwango cha matumizi ya mifumo ya kimenejimenti iliyowekwa katika Taasisi za umma 18 ilifanyika. Mifumo hiyo ni Mipango Mkakati, Upimaji wa Wazi wa Utendaji wa Kazi, Mikataba ya Huduma kwa Wateja, Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko na Ufuatiliaji na Tathmini. Matokeo ya tathmini hii yanaonesha kuwa kiwango cha matumizi ya mifumo katika Taasisi hizo ni asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Taarifa za Kitumishi na Mishahara Serikalini *(HCMIS)* uliimarishwa na kuboreshwa zaidi kwa kuwekea taratibu za kiutumishi 14 (zikiwemo taratibu za kushughulikia malimbikizo ya mishahara, uhamisho, ukomo wa utumishi na marekebisho ya taarifa za mtumishi) na kutoa mafunzo ya utumiaji wa taratibu hizo kwa Maafisa Rasilimaliwatu 1,047.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya kutoa usaidizi wa Kitaalam wa Mfumo wa *HCMIS* kwa Maafisa Rasilimaliwatu waliopo katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalitolewa kwa Maafisa TEHAMA 293 waliopo katika Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2013, Ofisi za Sekretarieti za Mikoa 21 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 116 ziliwezeshwa kutumia Mtandao wa Mawasiliano wa ndani wa TAMISEMI katika kufanyia kazi Mfumo wa *HCMIS* na hivyo

kuondoa kero ya awali ya kutokuwa na mawasiliano iliyokuwa ikisababishwa na mawasiliano duni ya intaneti.

Mheshimiwa Spika, Ofisi iliendelea kusimamia maandalizi ya Miradi ya Serikali Mtandao kupitia Mradi wa *Regional Communication Infrastructure Programme (RCIP),* ambapo Miradi minane inafadhiliwa.

Mheshimiwa Spika, Viongozi Wastaafu wa Kitaifa tisa na wajane watano wa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa waliendelea kupatiwa huduma kwa mujibu wa Sheria. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na uchambuzi wa athari za mazingira kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa (Mwl. Julius K. Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma (*TPSC*), kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu vyema majukumu yao na kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko katika Utumishi wa Umma pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti katika nyanja mbalimbali. Pia, kutoa mafunzo ya kitaaluma katika ngazi za cheti na stashahada.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Chuo cha Utumishi wa Umma kiliandaa na kuendesha kozi 50 kati ya 84. Kozi 18 zilikuwa za muda mfupi na kozi 32 za mafunzo ya muda mrefu. Washiriki 19,816 walijengewa uwezo wa kiutendaji. Kati ya washiriki hawa, 14,111 wamepata mafunzo ya muda mrefu na 5,705 wamepata mafunzo ya muda mfupi. Kati ya washiriki wote, Watumishi wa Umma walikuwa 8,245 na 11,571 walitoka katika Taasisi Binafsi na Umma wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wake 157 kati ya 186 waliopo. Watumishi 54 wanachukua kozi za muda mrefu ambapo kati yao sita wanachukua Shahada ya Uzamivu, 20 Shahada ya Uzamili, 27 Shahada ya Kwanza na Stashahada mtumishi

mmoja. Watumishi 103 waliobaki, walijengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mfupi na warsha.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimetoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya kuandaa mpango mkakati, miundo ya utumishi, muundo wa mishahara, muundo wa Taasisi, matumizi ya mifumo ya utekelezaji, mkataba wa huduma kwa mteja na maelezo ya kazi. Aidha, tafiti tatu zimefanyika katika maeneo yafuatayo: Utoaji Huduma kwa Mteja, uchunguzi wa kiwango cha chini cha mshahara katika Sekta Binafsi pamoja na Tathmini ya Mafunzo kuhusu maambukizi ya VVU mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma. Matokeo ya tathmini ya VVU ni pamoja na kupungua kwa unyanyapaa, kuongezeka kwa ari ya upimaji kwa hiari na kujitambulisha kwa ajili ya kupata huduma kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao *(TaGLA),* ina jukumu la kutoa mafunzo na taarifa za maendeleo ya kimataifa kwa Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi kwa njia ya mtandao kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imetoa Mafunzo ya Matumizi sahihi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara Serikalini kwa watumishi 1,047. Aidha, Wakala imetoa mafunzo kwa washiriki 2,444 katika nyanja mbalimbali. Kati ya hao, washiriki 320 ni washiriki binafsi na kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali na 2,124 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali. Aidha, midahalo tisa ya kisera na ushirikishaji wa maarifa kwa wadau 159 imeendeshwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala imepanua ushirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo. Taasisi hizi ni pamoja na *Kenya School of Government, African Capacity Building Foundation (ACBF),*

*Association of African Distance Learning Centres (AADLC), Leading Initiatives* ya Australia na Chuo cha Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Wakala ya Serikali Mtandao *(eGA)* imezinduliwa rasmi Julai, 2012, ikiwa na jukumu na mamlaka ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa Taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa Taasisi hizi zinatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(TEHAMA)* katika majukumu yao ya kila siku ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi kwa haraka na kwa viwango na ubora unaotakiwa. Aidha, Wakala ina jukumu la kuweka na kusimamia mifumo na miundombinu ya mawasiliano iliyo salama Serikalini itakayowezesha kufikisha huduma kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wakala imefanya utafiti wa utayari wa Taasisi za Serikali (*e-Government Readiness Survey*) katika kutumia mifumo ya TEHAMA na kufanikiwa kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano (2012/13 hadi 2016/17) uliozingatia hali halisi ya Taasisi hizo. Aidha, Wakala imekalimisha mpango wa mafunzo wa kuwajengea uwezo watalaamu wa TEHAMA kwenye Taasisi za Serikali katika kusimamia mifumo mbalimbali ya TEHAMA iliyopo na itakayosimikwa. Vilevile imekamilisha kuhuisha Tovuti Kuu ya Serikali itakayokuwa dirisha la taarifa na huduma zote zinazotolewa na Serikali kwa Wananchi kwa njia ya mtandao na uzinduzi rasmi unatarajiwa kufanyika mwaka ujao wa fedha (2013/14). Pia Wakala imeshaanza kutoa ushauri wa kitalaamu na kuzisaidia Taasisi mbalimbali za Serikali katika masuala ya kusimika na kusimamia mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwenye Taasisi zao.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398, ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma waliotajwa katika Kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo, inazingatia misingi ya maadili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Serikali ilitengewa jumla ya Shilingi 5,923,437,000 kwa Fungu 33 ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,465,255,000 zikiwa ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2013, kiasi cha Shilingi 2,951,135,000 za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya Shilingi 956,923,600 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Viongozi wa Umma 9,174 wa kada mbalimbali walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia Machi, 2013. Jumla ya Viongozi wa Umma 8,551 sawa na asilimia 93 walikuwa wamerejesha Fomu za Tamko. Viongozi waliokaidi kutekeleza matakwa ya Sheria bila sababu watafikishwa mbele ya Baraza la Maadili;

(ii) Matamko 233 ya Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma wa kada mbalimbali yamehakikiwa ili kujiridhisha kuhusu ukweli na uwazi katika ujazaji wa Fomu za Tamko. Miongoni mwa Viongozi wa Umma waliohakikiwa Rasilimali na Madeni yao ni pamoja na Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wabunge, Madiwani, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wa Idara, Wakala na Mashirika ya Umma, Majaji, Makamishna wa Tume, Wakurugenzi katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mahakimu wa ngazi mbalimbali;

(iii) Malalamiko 102 yalipokelewa na kuchambuliwa ili kubaini ukweli kuhusu malalamiko hayo. Kati ya Malalamiko hayo, Malalamiko 50 yanahusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili na Malalamiko 52 hayahusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa sheria hiyo. Malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yameanza kushughulikiwa na chunguzi 10 zimekamilika. Aidha, Malalamiko 52 yasiyohusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yameelekezwa kwenye mamlaka mbalimbali kwa ajili ya kushughulikiwa;

(iv) Viongozi wa Umma 1,012 kutoka katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Morogoro, Arusha, Tabora na Mwanza, walipatiwa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, kupitia Maonesho ya Nanenane na Siku ya Maadili Duniani, Wananchi 841 walipata fursa ya kutembelea mabanda na kuelimishwa kuhusu majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo vipeperushi 6,000, kalenda 4,100, Beramu 500 na nakala 1,500 za Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ziligawiwa. Vilevile, Vipindi vya redio 12 na matangazo manne ya redio yalitolewa. Aidha, Taasisi inategemea kutoa mafunzo ya Maadili ya Uongozi Mwezi Aprili, 2013 kwa Wabunge 351 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(v) Watumishi sita wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 35 wamepatiwa mafunzo ya uchunguzi ya muda mfupi;

(vi) Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398, yamewasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi. Marekebisho haya pamoja na mambo mengine, yameviimarisha Vifungu vya Sheria vinavyohusu kuzuia mgongano wa maslahi ya Kiongozi wa Umma katika utekelezaji wa majukumu ya Umma;

(vii) Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kipindi 2013/14 - 2017/18 ulihuishwa;

(viii) Ujenzi wa Tovuti ya Taasisi *(www.ethicssecretariat.go.tz.)* umekamilika na kuzinduliwa rasmi mwezi Novemba, 2012;

(ix) Uandaaji wa Mfumo wa Kanzidata za taarifa mbalimbali za Viongozi wa Umma umekamilika; na

(x) Ujenzi wa Miundombinu ya mawasiliano ukiwemo mtandao wa Intaneti kwenye Ofisi zilizopo Jengo la Sukari House umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika mwaka 2012/13, Ofisi ya Rais, Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma, iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,494,524,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2013 kiasi cha Shilingi 1,107,385,545 kilikuwa kimepokelewa na kutumika, ambayo ni asilimia 44.4 ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Ajira imefanya usaili kwa ajili ya nafasi za vibali vya ajira vilivyotolewa katika mwaka wa fedha 2011/12. Nafasi za ajira zilikuwa 4,377 hadi kufikia mwezi Machi, 2013, kati ya hizi ajira mpya zilikuwa 3,346 na ajira mbadala zilikuwa 1,031; nafasi zilizojazwa ni 2,560. Nafasi 1,817 zilizobaki zinaendelea kutangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Ajira iliwapangia waombaji 342 waliofaulu usaili na taarifa zao kuhifadhiwa kwenye Kanzidata *(database)* baada ya waajiri 94 kuwasilisha vibali vya nafasi wazi zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Sekretarieti ya Ajira inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya waombaji kazi kughushi sifa za kielimu, taarifa binafsi na pia sifa za kitaaluma kuonesha ufaulu wa juu kuliko uwezo halisi unaoonekana wakati wa usaili. Hali hii inaweza kuleta athari kwenye upatikanaji wa rasilimaliwatu wenye uwezo na utaalamu unaotakiwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia uendeshaji wa Rasilimaliwatu ili kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Aidha, Tume kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu imeendelea na

majukumu yake ya kusimamia ajira na nidhamu ya walimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Tume iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 7,938,210,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2013 kiasi cha Shilingi 5,540,141,279 kilipokelewa na kutumika, sawa na asilimia 70 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2012/13, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza majukumu yake kwa kuendesha Vikao vya kisheria viwili ambavyo vilitoa uamuzi wa Rufaa 73 na malalamiko manane, kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma 42, kuelimisha wadau kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia uendeshaji na usimamizi wa rasilimaliwatu kupitia kipindi cha redio na vipindi vinane vya televisheni, kufanya Utafiti kuhusu huduma zitolewazo na Tume kwa wadau wake pamoja na kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi 35 wa Tume kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Umma kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu ilitekeleza majukumu yake ya kisheria ambapo walimu 6,362 walisajiliwa; 2,533 walithibitishwa kazini; 510 walibadilishwa kazi; vibali vya maombi ya kustaafu kazi walimu 547 vilitolewa na kumbukumbu za mafao ya hitimisho la kazi za walimu 529 ziliandaliwa. Aidha, Idara ilishughulikia masuala ya nidhamu ya walimu 169, kati ya hao 161 walifukuzwa kazi, sita walirudishwa kazini na mashauri mawili yanaendelea kuhitimishwa. Makosa yanayoongoza katika mashauri hayo ni: utoro kazini – walimu 164 na makosa mengine yakiwemo utovu wa nidhamu, wizi, ubadhirifu wa mali ya umma na kufanya mapenzi na wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kipya kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kupitia Tangazo la Serikali

Na. 162 la tarehe 3 Juni, 2011 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha Mishahara katika Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010). Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais kuhusu viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Bodi iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 2,387,259,200 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2013 kiasi cha Shilingi 933,335,000 kilipokelewa na kutumika, sawa na asilimia 39 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Bodi ya Mishahara na Masilahi ilikusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu Uwiano baina ya Tija, Mshahara na Masilahi. Aidha, Bodi iliendesha mikutano kwa kuwashirikisha wadau wafuatao: Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa; Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Tija na Uchumi; Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Matokeo ya mkutano wa wadau wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yameiwezesha Bodi kuishauri Serikali kuhusu uoanishaji wa michango ya watumishi wa masharti ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha uelewa wa majukumu ya Bodi, elimu imetolewa kwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Mipango, Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha masilahi kwa Watumishi wa Umma yanaboreshwa, takwimu kwa ajili ya kuandaa Mfumo utakaotumika kukadiria Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma umeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2012/13, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/14 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94 na 9 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/14 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/14, Ofisi ya Rais, Ikulu, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa, Masuala ya Jamii na kazi nyingine zinazohusu ushauri kwa Rais;

(iii) Kuendesha mafunzo kwa Taasisi za Umma na Asasi za Kiraia 80 zinazosimamia utawala bora nchini ili Taasisi hizo ziweze kuwa msaada katika masuala ya kupambana na rushwa;

(iv) Kutayarisha Mpango wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

(v) Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi na namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

(vi) Kufanya Mikutano 40 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambapo Nyaraka 80 zitachambuliwa, Mikutano 25 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu *(IMTC)* itafanyika, ambapo Nyaraka 50 zitatolewa ushauri. Mikutano 24 ya Baraza la Mawaziri itafanyika ambapo Nyaraka 40 zitajadiliwa na maamuzi kutolewa;

(vii) Kufanya Mikutano ya Kazi 12 ya Makatibu Wakuu ambapo ajenda 24 zitawasilishwa na kujadiliwa. Aidha, Mikutano 15 ya Kamati za Baraza la Mawaziri itafanyika ambapo Hati/Miswada mbalimbali itachambuliwa;

(viii) Kufanya Mkutano wa tathmini ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri, utakaoshirikisha Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri Wizarani;

(ix) Kuendesha mafunzo ya utawala bora, rushwa na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya rushwa kwa Kamati za Uadilifu za Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kujenga uwezo wa kamati hizo katika uratibu na utekelezaji wa Mkakati katika Taasisi husika;

(x) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 60 na malalamiko 260 ya Watumishi wa Umma na Wananchi. Kuchambua na kutoa ushauri juu ya taarifa 40 za Tume ya Utumishi wa Umma na Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala za Serikali. Vilevile, kufanya mikutano mitatu ya kueleweshana kwa Watendaji 600 kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(xi) Kupanga na kuendesha vikao 12 vya Uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

(xii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa

Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(Open Government Partnership - OGP);*

(xiii) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii. Aidha, Mikutano 15 baina ya Serikali na Viongozi wa Dini mbalimbali itafanyika;

(xiv) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Aidha, kazi za Taasisi ya Uongozi zitaendelea kuratibiwa;

(xv) Kuimarisha mifumo ya Utungaji na Utekelezaji wa Sera, Ufuatiliaji na Tathmini na Uratibu wa Maboresho;

(xvi) Kuendelea na ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano; na

(xvii) Kuanza ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Mbeya na nyumba kumi za wafanyakazi, nyumba ya wageni na Ofisi za Wasaidizi wa Rais katika Ikulu Ndogo ya Chamwino.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika mwaka 2013/14, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuchunguza tuhuma 2,420 zilizopo na mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendelea na uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo, Maliasili na tuhuma mbalimbali zilizobainishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2010/2011. Aidha, chunguzi mpya zinazohusiana na Sekta ya Madini na Gesi zitafanyika;

(iii) Kukamilisha chunguzi za tuhuma saba za rushwa kubwa (*Grand Corruption*) kama ilivyopangwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi;

(iv) Kuendelea kuendesha kesi 495 zilizopo mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa chunguzi mbalimbali;

(v) Kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za rushwa kwa Wananchi, Watumishi wa Umma na Makampuni Binafsi na kuendeleza ushirikiano na Asasi za Kiraia katika mapambano dhidi ya rushwa;

(vi) Elimu kuhusu Rushwa katika Uchaguzi (Serikali za Mitaa) itatolewa;

(vii) Ufunguzi na uimarishaji wa Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa;

(viii) Kuelimisha umma juu ya athari za rushwa kwa kulenga makundi maalum ya Viongozi wa Dini, Viongozi wa Klabu za Wapinga Rushwa, Wasanii wa Nyimbo, Ngonjera na Muziki na Vyama vya Siasa;

(ix) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utendaji dhidi ya mianya ya rushwa kwa kufanya utafiti na udhibiti wa mianya katika Sekta za Madini (Petroli na Gesi) na Maliasili (vitalu vya uwindaji) na utafiti katika miundombinu ya barabara;

(x) Kupitia warsha mbalimbali wadau watashirikishwa kujadili matokeo ya utafiti, kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kudhibiti mianya ya rushwa;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Taarifa ya Utafiti wa Hali ya Rushwa na Utawala Bora Nchini uliofanyika mwaka 2009;

(xii) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi za TAKUKURU katika Mikoa ya Mara na Mbeya na kuanza ujenzi wa Ofisi katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Mkinga;

(xiii) Kuboresha mfumo wa takwimu, ufuatiliaji na tathmini na kanzidata;

(xiv) Ununuzi wa vifaa na utoaji wa mafunzo kwa ajili ya maabara ya uchunguzi wa *forensic* utafanyika;

(xv) Kutoa mafunzo maalum ya urejeshaji wa mali (*Asset Recovery*) zilizopatikana kwa vitendo vya rushwa kwa mujibu wa sheria kwa Maafisa uchunguzi 70;

(xvi) Kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti ya Manunuzi ya Umma (*PPRA*) kuandaa mwongozo wa namna ya kuzuia na kuchunguza malalamiko yanayohusiana na manunuzi nchini; na

(xvii) Kuajiri watumishi wapya 394 kwa ajili ya Ofisi za Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), katika mwaka 2013/14, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na uratibu wa marekebisho ya kisheria na ya kitaasisi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta Tanzania Bara na Zanzibar;

(ii) Kuendelea kujenga uwezo katika Halmashauri za Wilaya nne za Karagwe, Korogwe, Magu na Songea Vijijini Tanzania Bara na katika Wilaya mbili za Zanzibar ambazo ni Chake Chake na Wilaya ya Kati Unguja kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi vijijini;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wakulima 1,500 katika Halmashauri za Wilaya 15 zilizofanyiwa urasimishaji wa ardhi vijijini juu ya matumizi bora ya hati za hakimiliki za kimila katika kujipatia mitaji. Wilaya hizo ni Manyoni, Mtwara, Singida, Ludewa, Bunda, Makete, Mpanda, Kigoma, Mbarali, Muleba, Mbinga, Moshi Vijijini, Meru, Sikonge na Geita;

(iv) Kuendelea na urasimishaji wa mashamba ya

wakulima wa chai katika vijiji 24 vya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na kuanza urasimishaji wa mashamba ya katani katika Halmashauri za Wilaya za Muheza na Lushoto pamoja na mashamba ya miwa katika Halmashauri za Wilaya za Kilosa, Kilombelo na Kagera. Aidha, wakulima ambao mashamba yao yatarasimishwa watajengewa uwezo wa namna ya kutumia hati zao kujipatia mitaji kwa maendeleo zaidi;

(v) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Urasimishaji wa Wilaya katika Halmashauri za Wilaya 10 kwa kuongeza vijiji viwili kila Wilaya. Halmashauri hizo ni Mwanga, Meru, Masasi, Kasulu, Muleba, Sikonge, Singida, Mbinga, Sumbwanga na Ludewa;

(vi) Kuratibu na kusaidia utekelezaji wa Mpango Kazi wa urasimishaji ardhi wa Wilaya katika Halmashauri za Wilaya 10 zingine kwa kuongeza kijiji kimoja. Halmashauri hizo ni Bunda, Mpwapwa, Njombe, Makete, Musoma, Mkuranga, Nachingwea, Mvomero, Manyoni na Uyui;

(vii) Kujenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi mijini katika Jiji la Mbeya na Miji/ Manispaa ya Musoma, Sumbawanga na Tabora. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa Ardhi mjini utafanyika katika maeneo mawili yatakayochaguliwa na Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati;

(viii) Kuendelea na uratibu wa zoezi la kutengeneza na kutoa hati za urasimishaji ardhi Mijini katika maeneo ya Tunduma - Mbeya, Kimara Baruti - Dar es Salaam na Iringa;

(ix) Kuanza urasimishaji wa biashara katika Jiji la Tanga, Manispaa ya Iringa na Wilaya za Micheweni Pemba na Kaskazini B Unguja. Tathmini ya matokeo ya Urasimishaji Biashara itafanyika katika Jiji la Mbeya na Manispaa ya Morogoro; na

(x) Kuendelea na mchakato wa kuratibu

uimarishaji wa mifumo ya kitaasisi inayoendelea ikijumuisha Uanzishwaji wa Chombo cha Kitaifa cha Urasimishaji wa Rasilimali Ardhi na Biashara; Uanzishwaji wa Mfuko wa Urasimishaji wa Wilaya na Taratibu za Kurahisisha Mifumo ya Kodi na Utunzaji wa Fedha kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) itatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 yenye awamu mbili za miaka mitano. Utekelezaji wa Mpango huu wa *TASAF III* utafanyika kwa awamu hadi kufikia Halmashauri zote Tanzania Bara na Unguja na Pemba. Kazi zilizopangwa kutekelezwa na *TASAF* katika mwaka 2013/14 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza utekelezaji wa shughuli za *TASAF* Awamu ya Tatu, kwenye Halmashauri zaidi ya 41 za Tanzania Bara na Unguja na Pemba. Shughuli zitakazopewa kipaumbele ni kujenga uwezo kwa wataalaam katika maeneo ya utekelezaji, kuhamasisha walengwa na kujenga uelewa kuhusu shughuli na fursa za *TASAF* Awamu ya Tatu;

(ii) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara, Unguja na Pemba, kuibua Miradi ya Ujenzi na ile itakayoboresha huduma za afya, elimu, maji na kuongeza kipato. Jumla ya Miradi 1,200 itatekelezwa;

(iii) Kutekeleza Mpango wa Jamii wa Uhawilishaji Fedha kwa kaya maskini sana katika Halmashauri zaidi ya 41 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Aidha, Walengwa zaidi ya 500,000 kutoka Kaya Maskini 75,000 watanufaika na uhawilishaji fedha kwa lengo la kupata huduma za afya, elimu na lishe bora ili kuimarisha rasilimali watu *(Human Capital Development);*

(iv) Kukamilisha utayarishaji wa mifumo itakayotumika katika utekelezaji wa shughuli za *TASAF* Awamu ya Tatu. Wadau mbalimbali watapatiwa mafunzo ya matumizi ya mifumo ili kuweka mazingira mazuri ya kutumia mifumo iliyoandaliwa. Aidha, sambamba na mifumo hiyo,

masjala ya walengwa itaanzishwa (*Unified Registry of Beneficiaries*), ili kutunza kumbukumbu za kaya maskini nchini, ambazo zinaweza kupatikana na kutumiwa na wadau wengine wa maendeleo katika juhudi za kupunguza umaskini;

(v) Kukusanya takwimu za awali (*Baseline data*) katika maeneo ya utekelezaji kabla ya kuanza kutuma fedha za miradi na uhawilishaji kwa walengwa. Takwimu hizi ni muhimu sana kwa ajili ya kufahamu manufaa ya mradi baada ya kufanya tathmini mbalimbali; ili kufahamu hali ya kaya maskini kabla ya mradi na hali itakavyokuwa baada ya kutekeleza mradi;

(vi) Kukuza uelewa wa Wananchi wanaotekeleza miradi kuhusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa Mpango kwa kutumia vipindi vya redio, televisheni na machapisho mbalimbali. Aidha, Mkakati wa Mawasiliano na Upashanaji Habari kwa kuzingatia mahitaji ya Awamu ya Tatu umeandaliwa;

(vii) Kufanya ukaguzi wa fedha za mradi ili kujiridhisha na matumizi ya fedha, ubora wa miradi inayotekelezwa pamoja na kuzingatia miongozo ya sekta husika na ya mradi kwa ujumla; na

(viii) Kufuatilia na kufanya tathmini ya miradi inayotekelezwa ili kubaini hatua zilizofikiwa katika kuondoa umaskini kwa walengwa walionufaika na msaada wa *TASAF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/14, Taasisi ya Uongozi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutengeneza kozi kwenye maeneo ya Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma na maeneo mengine yatakayotokana na maombi kutoka kwa wadau;

(ii) Kuendesha kozi 10 katika fani za Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya maendeleo endelevu, Menejimenti inayozingatia matokeo, Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya

Umma na Kutafakari matokeo ya Uongozi na kuchukua hatua;

(iii) Kufanya mahojiano 10 na wakuu wa nchi, waliopo madarakani na waliostaafu, ndani na nje ya nchi, na Wataalam mbalimbali kuhusu Uongozi na maendeleo endelevu ili kukuza uelewa na kupata uzoefu kwa viongozi na kurusha mahojiano hayo katika televisheni;

(iv) Kuendesha mikutano minne ya majadiliano itakayowahusisha viongozi na wataalamu kuzungumzia masuala mbalimbali ya Uongozi na maendeleo endelevu;

(v) Kuwezesha semina tatu zikiwa ni mpango wa kutekeleza Jukwaa la Uchumi wa Kijani zikiwa na lengo la kuongeza uelewa kwa watunga sera, watoa maamuzi na watu wenye ushawishi katika jamii kuhusu masuala yanayohusu uchumi wa kijani;

(vi) Kufanya tafiti mbili kuhusu Tathmini ya Utawala katika Sekta ya Umma kwa lengo la kubaini upungufu wa maarifa katika eneo la Utawala;

(vii) Kuandaa vipeperushi mbalimbali kwa ajili ya kuitangaza Taasisi ya Uongozi;

(viii) Kutoa Machapisho sita katika maeneo ya Utawala Bora na Maendeleo Endelevu; na

(ix) Kununua vitabu na machapisho mbalimbali kwa ajili ya Maktaba ya Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/14, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF)* umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga na kutekeleza muundo mpya wa Taasisi ili kuleta ufanisi katika utoaji huduma;

(ii) Kuendelea kujenga uwezo wa watendaji ili kutoa huduma bora kwa wateja; na

(iii) Kufanya tafiti ili kubaini huduma wanazostahili vijana hasa wanaomaliza mafunzo kwenye vyuo mbalimbali vya ufundi stadi ili kuwaweka pamoja na kuendeleza ujuzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14, Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 9,248,595,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 242,781,448,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi cha Shilingi 59,587,357,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa Wananchi wanapotoa huduma mbalimbali. Majukumu haya yatafikiwa kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuboresha masilahi ya Watumishi wa Umma kwa kuendelea kutekeleza Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010. Katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 4,763.196 kwa ajili ya kugharamia malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 982.096 ambazo ni sawa na asilimia 26, ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 3,781.100 zilizopangwa kutumika katika mwaka wa fedha 2012/13. Kiasi hiki cha shilingi bilioni 4,763.196 kitatumika kugharamia ajira mpya, upandishwaji vyeo na nyongeza za kawaida za

mishahara za mwaka, pamoja na nyongeza za mishahara kuanzia Julai, 2013.

(ii) Kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 33 nyingine zilizo katika maeneo yenye mazingira magumu ili kubainisha motisha na kuandaa mwongozo wa kutoa motisha kwa watumishi walio katika maeneo hayo;

(iii) Kusimamia matumizi sahihi ya Rasilimaliwatu na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kusimamia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa Umma;

(v) Kufanya tathmini ya kazi kwa lengo la kuhuisha miundo ya utumishi ili iendane na mabadiliko ya utendaji kazi;

(vi) Kutekeleza Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi ya Kitaasisi pamoja na kutoa mafunzo kuhusu mfumo huu kwa Taasisi 11;

(vii) Kupanua na kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya TEHAMA na kuiwezesha Wakala ya Serikali Mtandao kutekeleza majukumu yake;

(viii) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 61,915 ambapo katika Sekta za Elimu ni walimu 33,586, Afya watumishi 11,221, Kilimo 1,804, Mifugo 2,500 na watumishi wengineo 12,804. Aidha, watumishi 42,419 wa kada mbalimbali watapandishwa vyeo;

(ix) Kulipa madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma;

(x) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa Wakala za Serikali na kuhuisha miundo, mifumo ya utendaji kazi na viwango vya kimenejimenti vinavyolenga katika kuboresha utoaji wa huduma katika Utumishi wa Umma

pamoja na kuandaa mfumo wa kusimamia utendaji kazi wa Wakala za Serikali;

(xi) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali;

(xii) Kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kukuza maadili;

(xiii) Kusimamia utekelezaji wa mifumo ya utendaji kazi na uwajibikaji iliyoanzishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika Utumishi wa Umma;

(xiv) Kusimamia uendelezaji wa stadi za uongozi na kuwaendeleza Watumishi wa Umma kitaaluma kwa kuzingatia makundi maalum;

(xv) Kusimamia Mikutano ya Mabaraza ya Wafanyakazi sehemu za kazi, Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma, Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta katika Utumishi wa Umma na Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma.

(xvi) Kusimamia Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma;

(xvii) Kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria;

(xviii) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka cha Kanda ya Ziwa (Mwanza);

(xix) Kufungua rasmi Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma na kukusanya kumbukumbu zilizorundikana katika Taasisi za Umma na kuzihamishia kwenye kituo hiki;

(xx) Kuweka mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu katika ofisi 40 za Wakuu wa Wilaya;

(xxi) Kuanza ujenzi wa Jengo Jipya la Ofisi litakalotumiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Tume ya Utumishi wa Umma; Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ili kutoa mazingira bora ya kufanyia kazi pamoja na kupunguza gharama za pango;

(xxii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Serikali Mtandao (*e-Government Policy);*

(xxiii) Kuandaa miongozo mbalimbali ya matumizi ya TEHAMA Serikalini;

(xxiv) Kuendelea kusimamia na kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Serikali Mtandao kupitia Mradi wa *Regional Communication Infrastructure Programme (RCIP);* na

(xxv) Kuimarisha usimamizi, uendelezaji na kuendelea kutoa usaidizi wa kitaalamu wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara Serikalini *(HCMIS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Chuo cha Utumishi wa Umma *(TPSC)* kinatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kuendesha kozi 43 za muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali;

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 16,690 katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi na utawala bora;

(iii) Kutoa mafunzo ya uongozi na utawala kwa Watumishi wa Umma 360;

(iv) Kutoa mafunzo elekezi *(induction course)* kwa watumishi wapya 360 katika Utumishi wa Umma;

(v) Kutoa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa watumishi 160;

(vi) Kutoa mafunzo ya usimamizi wa ununuzi wa umma na mafunzo ya Sheria mpya ya Manunuzi na Utunzaji wa Kumbukumbu na fedha kwa Watumishi wa Umma 40;

(vii) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 605;

(viii) Kutoa mafunzo ya utoaji wa huduma bora kwa mteja kwa makatibu muhtasi 105;

(ix) Kutoa mafunzo ya Menejimenti, Usimamizi wa Ofisi za Umma kwa washiriki 1,102;

(x) Kuendesha shauri na tafiti za kitaalamu 19 kuhusu kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

(xi) Kufanya tafiti 10 katika masuala mbalimbali yatakayolenga katika kupata taarifa zitakazotumika katika kuboresha Utumishi wa Umma;

(xii) Kuandaa michoro ya matumizi ya ujenzi (*masterplan*) ya upanuzi wa Chuo katika eneo la Ikwiriri, Wilayani Rufiji;

(xiii) Kujenga madarasa mawili na chumba kimoja cha maktaba katika Tawi la Tabora; na

(xiv) Kuwajengea uwezo wa utendaji kazi watumishi 107 kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Mafunzo ya muda mrefu watumishi 27 (10 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, 6 Shahada ya Uzamili, 7 Shahada ya Kwanza na 4 katika ngazi ya Stashahada). Watumishi waliobaki 80 watapata mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao *(TaGLA),* katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuboresha uwezo kwa Watanzania katika kozi mbalimbali za nje na ndani kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Jumla ya washiriki wapatao 3,000 wanatarajiwa kupata mafunzo haya;

(ii) Kukuza Mtandao wa Kituo ili kuwafikia wahitaji walioko Mikoani kwa kuanza utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya upembuzi yakinifu juu ya kuanzisha vituo shirikishi vya elimu mtandao;

(iii) Kuongeza ushirikiano na asasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kuendelea kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kwa gharama nafuu;

(iv) Kukamilisha mchakato wa ajira kadiri ya muundo uliopitishwa ili kuiwezesha Wakala kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi na ubora kwa Wadau wake;

(v) Kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Wakala ili kupata mazingira bora ya kutolea huduma zake kwa wateja;

(vi) Kukuza na kuboresha uwezo wa wafanyakazi ili kukidhi ongezeko la wateja na mabadiliko ya haraka ya teknolojia; na

(vii) Kuendesha midahalo ya Sera ili kupeana taarifa mbalimbali za maendeleo ya Taifa kupitia Mtandao wa Kitaifa wa Maarifa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala ya Serikali Mtandao *(eGA),* katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuanzisha Vituo vya Kuhifadhi Mifumo ya Serikali ili kulinda usalama wa taarifa na mifumo iliyopo na

kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa uhakika wakati wote;

(ii) Kuandaa, kuweka na kuziunganisha Taasisi 50 za Serikali kwenye mfumo wa pamoja wa Barua Pepe;

(iii) Kuwajengea uwezo watumishi 300 wa Serikali wa ngazi mbalimbali kuhusu masuala ya TEHAMA;

(iv) Kuzindua Tovuti Kuu ya Serikali kwa ajili ya kutoa huduma na taarifa zinazotolewa na Serikali kwa njia ya mtandao;

(v) Kubuni na kutengeneza mifumo itakayoweza kutumika katika simu za mkononi kutoa huduma kwa Wananchi;

(vi) Kuiwezesha Sekretarieti ya Ajira Kutengeneza mfumo utakaorahisisha utekelezaji wa majukumu yake; na

(vii) Kuhifadhi tovuti za Idara Zinazojitegemea 20 pamoja na mifumo mtambuka ya Serikali kwenye maeneo mahususi ya uhifadhi wa mifumo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza kazi zilizotajwa hapo juu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imetengewa jumla ya Shilingi 42,884,680,000. Kati ya fedha hizi; Shilingi 23,564,680,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 19,320,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kupokea, kuchambua na kufanya uchunguzi wa awali wa malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kuandaa na kusambaza Fomu 10,270 za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;

(iii) Kufanya uhakiki wa Rasilimali na Madeni kwa Viongozi 300 wa Umma;

(iv) Kuwaelimisha Viongozi wa Umma 874 kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili;

(vi) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Wananchi na Asasi zisizo za Kiserikali 12 kwa lengo la kuzijengea uwezo na kuziwezesha kusaidia kutoa elimu ya Maadili kwa Umma;

(vii) Kuijengea uwezo Ofisi kwa kuwapatia Watumishi mafunzo kulingana na fani zao na kuwapatia vitendea kazi;

(viii) Kununua viwanja kwa ajili ya Ofisi ya Kanda ya Kati – Dodoma, Kanda ya Ziwa – Mwanza na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya;

(ix) Kufanya utafiti kuhusu masuala ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(x) Kukusanya takwimu kwa ajili ya kuainisha viashiria mbalimbali vinavyopima utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(xi) Kuandaa na kusambaza vipeperushi, kalenda, mabango, vipindi vya redio, runinga na ujumbe wa simu za mkononi kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma; na

(xii) Kuendeleza awamu ya pili ya ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14, Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inatarajia kutumia kiasi Shilingi 9,249,426,800. Kati ya fedha hizo, Shilingi 6,165,883,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 3,083,543,800 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/14 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma ili kuwezesha waajiri katika maeneo hayo kupata wafanyakazi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo;

(ii) Kuendesha mchakato wa ajira kwa nafasi wazi za kazi 12,804 kwa ajili ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Wakala wa Serikali;

(iii) Kuimarisha Kanzidata na kutunza Takwimu za wahitimu kutoka kwenye Vyuo mbalimbali kwa urahisi wa Rejea; na

(iv) Kutembelea waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa shughuli za Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14, Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 2,949,833,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma katika mwaka 2013/14 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kuratibu mikutano ya kila robo

mwaka ya Tume, kutolea uamuzi Rufaa na Malalamiko kadiri yatakavyopokelewa;

(ii) Kufanya ukaguzi wa rasilimaliwatu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu; kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuendesha vikao vinne kwa mwaka katika ngazi ya Makao Makuu, Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kutolea uamuzi masuala ya Ajira na Nidhamu kwa walimu katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kuelimisha wadau kuhusu shughuli za Tume kupitia njia mbalimbali kama vile vyombo vya habari, mikutano ya kazi na wadau, maonesho na ziara;

(v) Kufanya tafiti kulingana na mahitaji ya Tume na wadau wake;

(vi) Kutoa elimu kwa Watumishi wa Tume kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI na mapambano dhidi ya rushwa; na

(vii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Tume katika ngazi zote kwa kuwajengea uwezo kitaaluma watumishi 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14, Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 11,064,526,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma imepewa jukumu la kufanya tafiti mbalimbali, kuchambua na kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuoanisha na kuwianisha mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/14, Bodi ya Mishahara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuchambua, kubaini na kushauri kuhusu kuoanisha na kuwianisha mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya tafiti juu ya uhusiano wa tija, mishahara, masilahi na mwenendo wa malipo katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuandaa mwongozo kwa ajili ya upangaji na ukadiriaji wa mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kuanzisha Kituo cha Taarifa za mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;

(v) Kuandaa Sheria ya Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na

(vi) Kujenga uwezo wa kiutendaji wa Wajumbe na Watumishi wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14, Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma, inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 2,213,882,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali imeandaa miongozo ya Maadili katika Utumishi wa Umma. Miongozo hii siyo tu kwamba ni nyenzo ya kuhakiki tabia na mienendo ya Watumishi wa Umma, bali pia ni nyenzo ya kuongeza tija na kuhakikisha matumizi bora na sahihi ya rasilimali fedha, rasilimalivitu na rasilimaliwatu. Ninapenda kusisitiza kuwa Watumishi wa Umma wanapaswa kuzingatia na kutumia miongozo hiyo kwa ukamilifu ili kuziwezesha Taasisi kufikia malengo yake na kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi. Serikali haitasita kuwachukulia hatua stahiki watumishi wasio waadilifu, wasiowajibika na wale wote watakaojihusisha na

vitendo vitakavyosababisha matumizi mabaya ya madaraka na mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu, tunahitaji utawala bora ambapo Sera, Sheria, Taratibu na Kanuni bora zinatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za Umma. Taasisi zenye jukumu la kuhakikisha mazingira haya yanakuwepo ni Ofisi za Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma na Tume ya Mipango. Hivyo, Mipango ya Utekelezaji ya 2013/14 ya Taasisi hizi za Serikali inalenga kufanikisha majukumu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2012/13 na mipango yetu kwa mwaka wa fedha 2013/14, naomba kuwasilisha rasmi maombi yetu ya fedha kwa mwaka 2013/14 kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu
Matumizi ya Kawaida Shs. 9,248,595,000
**Jumla Shs. 9,248,595,000**

(b) Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 242,781,448,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Shs 59,587,357,000

(c) Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 23,564,680,000
(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Shs. 19,320,000,000
**Jumla Shs. 42,884,680,000**

(d) Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretariet ya Maadili ya Viongozi

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 6,165,883,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Shs. 3,083,543,800
**Jumla Shs. 9,249,426,800**

(e) Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 2,949,833,000
**Jumla Shs. 2,949,833,800**

(f) Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 11,064,526,000
**Jumla Shs. 11,064,526,000**

(g) Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi Katika Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Shs. 2,213,882,000
**Jumla Shs. 2,213,882,000**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tunakushukuru sana kwa hotuba yako, ambayo pia imewasilisha masuala ya Utawala Bora pia.

Sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uhusiano wa Uratibu), Mheshimiwa Stephen Wasira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013 na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013. Mapitio haya yamegawanyika katika makundi matatu yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni;

(ii) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge; na

(iii) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi zilizotolewa Bungeni chini ya Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kwa utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha Sheria Na 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango;

(ii) Kutayarisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo wa mwaka 2012/2013 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016);

(iv) Kutangaza Dira ya Taifa 2025, Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/2012 – 2025/2026), na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016);

(v) Kuibua na kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii;

(vi) Kuratibu ubia wa kukuza uchumi kati ya Serikali za Tanzania na Marekani;

(vii) Kuratibu Ushirikiano na Benki ya Dunia kuhusu mkakati wa kuvutia viwanda vya kati kutoka Asia kuja Tanzania;

(viii) Kuratibu ushirikiano na Serikali ya Malaysia, hususan, Kitengo cha Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Majukumu ya Serikali, yaani *the Performance Management and Delivery Unit,* kama kinavyoitwa huko Malaysia *PEMANDU,* kwa lengo la kuanzisha mfumo kama huo hapa nchini; na

(ix) Kuendelea kujenga uwezo wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa ahadi hizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kurekebisha Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango.

Katika mwaka 2012/2013 Tume ya Mipango iliahidi kuwasilisha Bungeni Muswada wa marekebisho ya Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango. Katika kuhakikisha kuwa ahadi hiyo inatekelezwa, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuchambua Taarifa za Utafiti wa Uwianishaji wa Shughuli na Wajibu wa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango katika muundo na majukumu yake mapya *(The Alignment of POPC function to its new Roles and Responsibilities). Utafiti huu ulifanywa na mtalaam mwelekezi (ESRF).* Matokeo ya utafiti huu ndiyo chimbuko la marekebisho ya Sheria Na. 11/1989 na kukusanya maoni ya Watumishi wa Tume ya Mipango;

(ii) Kufanya mikutano ya mashauriano na wataalam kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu mapendekezo yanayokusudiwa katika mabadiliko ya Sheria Na. 11/1989; na

(iii) Kuitisha Mkutano wa wadau kujadili rasimu ya mapendekezo ya kurekebisha Sheria Na. 11/ 1989 iliyounda Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo mengine, wadau walishauri kuwa mchakato wa kurekebisha Sheria Na. 11/1989 usiharakishwe ili kutoa nafasi zaidi ya kuwashirikisha wadau wengi. Hivyo, hatua inayofuata ni kuendelea kupata maoni zaidi kama ilivyoshauriwa, kukamilisha uandishi wa Muswada husika na kisha kupata ridhaa ya Serikali kabla ya kuwasilishwa Bungeni. Tume ya Mipango inakusudia kuwasilisha Muswada wa Sheria husika Bungeni mwaka ujao wa fedha.

(2) Kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014 ambayo yaliridhiwa na Serikali mwezi Januari, 2013.

Aidha, mapendekezo hayo yaliwasilishwa katika Kamati ya Bunge Zima kama Kamati ya Mipango na baadaye kujadiliwa katika Kamati ya Bunge ya Bajeti mwezi Aprili, 2013, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua inayoendelea ni kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine. Baada ya kuridhiwa na Serikali, Mpango huo utawasilishwa rasmi Bungeni mwezi Juni, 2013 ili kupata idhini na kuanza utekelezaji.

(3) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 na wa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unatekelezwa kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka mmoja mmoja. Katika hatua za awali za kufanya ufuatiliaji na tathmini, Tume ya Mipango ilifanya uchambuzi wa Mipango Kazi ya Kisekta kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013. Uchambuzi huo ulifanywa kwa kuzingatia Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/2012 - 2025/2026), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016) na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilifanya ufuatiliaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo mwezi Februari, 2013 katika Sekta za Miundombinu, Nishati, Kilimo, Maji, Viwanda na Elimu.

Lengo la ufuatiliaji huo ilikuwa ni kuhakikisha kuwa hatua za utekelezaji wa miradi zinaendana na Mpango Kazi na fedha zilizotolewa kwa kipindi cha nusu mwaka 2012/2013. Tathmini ya awali inaonesha kuwa miradi mingi ipo nyuma ya ratiba kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha, taratibu za ununuzi na madeni ya miaka iliyopita.

Aidha, kutokamilika kwa tathmini ya fidia na ulipaji wa fidia kwa wakati imechangia kwa baadhi ya miradi kuchelewa kuanza kazi.

Vilevile, miundombinu na huduma wezeshi hususan barabara, maji na umeme ni kikwazo kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi. Mpango wa mwaka 2013/2014, pamoja na mambo mengine utajielekeza kutatua changamoto hizo.

(4) Kutangaza Dira ya Taifa 2025, Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Tume ya Mipango iliendelea kutangaza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/2012 - 2025/2026) na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016). Dira na mipango hiyo ilitangazwa kupitia tovuti ya Taifa na ya Tume ya Mipango, Warsha/Mikutano, vipindi vitano vya runinga, vipindi vitano vya redio na makala mbalimbali zilizoandikwa magazetini. Aidha, Tume iliendelea na uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya

Dira na Mpango wa Maendeleo kwa wadau mbalimbali.

(5) Kuibua na Kufanya Tafiti Katika Maeneo Mbalimbali ya Kiuchumi na Kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, kati ya tafiti tatu zilizoibuliwa mwaka 2011/2012, mbili zimekamilika na moja inaendelea kufanyika. Tafiti zilizokamilika ni *Muundo-taasisi kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda nchini* na *Maendeleo ya miundombinu-msingi kwa kilimo cha kisasa na cha kibiashara nchini*. Tume ya Mipango imejiridhisha na ubora wa taarifa hizo na hatua inayofuata ni kuwasilisha muhtasari wa kisera, yaani *Policy brief* na ushauri Serikalini kwa ajili ya maamuzi na hatimaye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu uendelezaji wa taaluma na ujuzi unaohitajika kuiwezesha Tanzania kuwa na nguvu za kiuchumi ifikapo 2025 unaendelea. Mtaalam elekezi ameshaanza kazi ya ukusanyaji wa takwimu na taarifa zinazohitajika katika maeneo yaliyochaguliwa *(sampled areas)* ili kuwezesha kuandaa taarifa ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbili ziliibuliwa katika mwaka 2012/2013 nazo zilianza kufanyika. Tafiti hizo ni:-

(i) Ufanisi wa Sekta ya Kilimo nchini Tanzania, ambayo iko katika hatua za awali za kumpata mtaalam elekezi; na

(ii) Utafiti kuhusu ukuaji wa Miji Tanzania:- Fursa na Changamoto kufikia Maendeleo Endelevu, ambapo hadidu za rejea kwa ajili ya utafiti huu zimeandaliwa na taratibu za kumpata mtaalam elekezi wa kufanya kazi hiyo zimeanza.

(6) Kuratibu Ubia wa Ukuzaji Uchumi kati ya Tanzania na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2012, Serikali za Tanzania na Marekani zilisaini makubaliano ya awali *"Joint Statement of Principles"* ambayo yaliweka misingi ya ushirikiano wa kutatua vikwazo vya kiuchumi vilivyoibuliwa kutokana na uchambuzi wa kitaalam wa pamoja chini ya programu ya ubia wa kukuza uchumi *(Partnership for Growth*).

Maeneo yaliyochaguliwa na kupewa kipaumbele katika makubaliano hayo ni umeme na barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkazo katika ushirikiano huo unawekwa katika kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji wa sekta binafsi.

Serikali ya Marekani itashirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kujenga uwezo wa rasilimaliwatu na Taasisi za Umma na sekta binafsi ili kusukuma uwekezaji katika maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa.

Katika hatua za awali, *TANESCO, TPDC* na Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* wamepatiwa mafunzo ambayo yatasaidia kupambana na wizi wa umeme kwa kutumia "*automatic reading meter programme (smart meter)"* kwa wateja wenye viwanda vidogo na vya kati pamoja na mahoteli.

Aidha, mtaalam elekezi *(Delloite)* anafanya kazi ya kutathmini uwezekano wa makampuni ya Kimarekani kushirikiana na Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* pamoja na kampuni nyingine za kitanzania katika kujenga miundombinu ya umeme vijijini.

(7) Kuratibu Ushirikiano na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/ 2013, Tume ya Mipango iliendelea kushirikiana na Benki ya Dunia kufanya uchambuzi wa pamoja ili kubainisha aina ya viwanda ambavyo Tanzania inaweza kuvutia vihamie hapa nchini kutoka nchi za Asia (China, Malaysia, Vietnam, Singapore, na kadhalika) na matakwa ya wamiliki wa viwanda hivyo.

Viwanda vilivyobainishwa chini ya utaratibu huu ambao unaitwa *"Growth Identification Framework"* ni pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na maziwa; nguo na mavazi; nyama na ngozi; kuunganisha pikipiki na mabasi madogo; na vile vya kutengeza bidhaa za watalii.

Lengo kuu ni kuharakisha ukuaji wa uchumi kupitia ujenzi wa Sekta ya Viwanda vya kati hasa vile ambavyo vinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini na vile vyenye fursa kubwa ya kuongeza ajira hasa kwa vijana. Rasimu ya mwisho ya uchambuzi huo itawasilishwa Serikalini kwa maamuzi na hatimaye utekelezaji wake utafuata.

(8) Kuratibu Ushirikiano na *PEMANDU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/ 2013 Tume ya Mipango kwa kushirikiana na kitengo kinachojulikana kwa jina la *"Perfomance Management and Delivery Unit, (PEMANDU)"* cha Malaysia iliandaa warsha tatu za Baraza la Mawaziri kuhusu mfumo wa ufuatiliaji unaotumika nchini Malaysia ili kujenga uelewa wa pamoja na kuangalia namna bora ya kutumia mfumo huo hapa nchini.

Katika warsha hizo, Baraza la Mawaziri liliazimia mambo yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kwa mfumo mpya wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kuzingatia mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini unaotumika na *PEMANDU*;

(ii) Kuundwa kwa chombo maalum cha ufuatiliaji na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na ya kimkakati iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo. Chombo hicho ilipendekezwa kiitwe "*President Delivery Bureau (PDB)"* na kiwe chini ya Ofisi ya Rais;

(iii) Serikali kuingia mkataba na *PEMANDU* ya Malaysia ili kusaidia kujenga *PDB* na kutekeleza mfumo wa uchambuzi wa ki-maabara *(labs)* hapa nchini; na

(iv) Maeneo sita (6) ya uchambuzi wa kimaabara *(labs)* katika awamu ya kwanza ili matokeo yake yatumike kwenye maandalizi ya bajeti ya 2013/ 2014 ambayo ni utafutaji wa mapato, kilimo nishati, uchukuzi, elimu na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maazimio ya Warsha ya Baraza la Mawaziri, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na wadau wengine imekamilisha mapendekezo ya muundo wa chombo cha *"President Delivery Bureau (PDB)."*

Aidha, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na *PEMANDU* wameratibu awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mfumo wa uchambuzi wa kimaabara *(labs)* na kuandaa programu ya kina ya utekelezaji wa kila mradi au Programu ya Maendeleo. Awamu hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Februari 2013, Dar

es Salaam na lilifungwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 5 Aprili, 2013, Dar es Salaam.

Hatua inayofuata ni kujumuishwa matokeo ya maeneo sita (6) ya uchambuzi wa kimaabara *(labs)* katika bajeti za wizara zinazohusika kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2015/2016. Maelezo ya kina kuhusu matokeo hayo yalitolewa katika Warsha ya Baraza la Mawaziri iliyojumuisha Naibu Mawaziri, Katibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu tarehe 11 Aprili, 2013, Dodoma. Aidha, Baraza la Mawaziri liliridhia matokeo ya awamu ya kwanza ya uchambuzi wa kimaabara *(labs)* na kuanzishwa kwa *"President Delivery Bureau (PDB)"* tarehe 12 Aprili, 2013, Dodoma.

(9) Kuendelea Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya watumishi 32 walihudhuria mafunzo mbalimbali, ambapo watumishi saba walihudhuria mafunzo ya muda mrefu katika shahada ya kwanza na ya pili katika fani za Uchumi, Uchambuzi Sera, Utawala, Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhasibu Na Mawasiliano Kwa Umma. Watumishi 25 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani za Udereva, Ukatibu Mahsusi na Uhasibu. Kati ya watumishi hao 32, watumishi saba walihudhuria mafunzo nje ya nchi ili kuimarisha uwezo wao katika uchambuzi wa sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watumishi watano waliajiriwa katika mwaka 2012/2013 ili kuziba pengo liliokuwepo kwa kada za Afisa Rasilimali Watu ni mtumishi mmoja, Mhasibu mmoja, Mkutubi mmoja na Katibu Mahsusi wawili. Kadhalika, Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/2014 imewasilisha maombi ya ajira mpya 50. Katika maombi hayo, nafasi 31 ni za wachambuzi

sera na wachumi wanaohitajika kuziba upungufu katika klasta za Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2012/2013, iliyokuwa Kamati ya Fedha na Uchumi ilitoa maagizo kwa Tume ya Mipango kwa ajili ya utekelezaji. Maagizo hayo yalikuwa ni pamoja na:-

(i) Tume iwasilishe kwenye Kamati, taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka;

(ii) Tume iendelee kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara nyingine zikiwemo Taasisi za Serikali ili kuhakikisha inasimamia na kuratibu ipasavyo miradi ya maendeleo inayotakiwa kutekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016. Aidha, Tume ya Mipango ishirikiane na Wizara ya Fedha katika kuweka vigezo vya mgao wa bajeti ya Serikali ya kila mwaka ili kuhakikisha kuwa vipaumbele vya kitaifa na vya kimkakati vinatengewa fedha za kutosha; na

(iii) Mfumo wa kutoa na kupata taarifa uboreshwe ili kubainisha ushiriki na mchango wa sekta binafsi katika kutekeleza shughuli zinazotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi hususan ya kimkakati na kuandaa taarifa ambayo itajumuishwa na taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na sekta mbalimbali katika mpango wa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Taasisi nyingine.

Katika kuhakikisha ushirikiano na Wizara ya Fedha unaendelezwa, Tume ya Mipango imeendelea kuwa Mwenyekiti-mwenza wa Kamati ya kutayarisha Mwongozo wa Mpango na Bajeti. Vilevile, Tume ya Mipango imeendelea kupitia Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na kutoa ushauri na mapendekezo kwa Wizara ya Fedha kuyazingatia katika mgao wa fedha za maendeleo kwa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imekuwa ikikutana na wizara zote katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka. Vilevile, Tume ya Mipango imeshirikiana na wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi katika zoezi la uchambuzi wa kina wa kimaabara *(Labs)* ili kubaini changamoto kubwa za kiuchumi na kuandaa programu za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mipango inandaa "*Public Investment Manual*" ambapo tayari hadidu za rejea na taratibu za kumpata mtaalam elekezi wa kuandaa mwongozo huo kwa kushirikiana na wataalamu wa Tume zinaendelea. Lengo kuu ni kuelekeza Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu misingi ya kuandaa na kuwasilisha maandiko ya miradi ya maendeleo na kufanya uchambuzi wa miradi hiyo. Kukamilika na kuanza kutumika kwa mwongozo huo kutarahisisha upatikanaji na uwekaji wa taarifa sahihi za miradi ya maendeleo kwa Sekta ya Umma na hata ile miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 4940, Mradi wa Kuhakikisha Ukuaji wa Uchumi Unashirikisha walio Wanyonge na Maendeleo Endelevu Kimazingira *(Pro Poor Economic Growth and Environmental Sustainable Development Project)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/ 2013 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Uchambuzi wa taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya utunzaji wa mazingira, ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini;

(ii) Mijadala na mawasiliano na wadau mbalimbali, yakijumuisha sekta, Taasisi za elimu ya juu, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Kijamii, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo Tanzania bara na Zanzibar yamefanyika ili kupata muafaka na mchango wa Tanzania katika maandalizi ya agenda ya maendeleo ya Dunia baada ya kikomo cha malengo ya milenia mwaka 2015 kitakapofika; na

(iii) Kuwezesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuendesha tafiti na mijadala ya kiuchumi na maendeleo chini ya Kigoda cha Mwalimu Julius K. Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 6526, Mradi wa Kufuatilia Idadi ya Watu *(Population Planning Project).* Katika mwaka 2012/2013 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kuandaa taarifa ya Tanzania ya Utekelezaji wa Maazimio ya Kongamano la Kimataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo lililofanyika Cairo, Misri mwaka 1994. Taarifa hiyo ilikamilika mwezi Desemba, 2012 lengo lake ikiwa ni kuchambua mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa maazimio ya Malengo ya Milenia 2015.

Taarifa hiyo inaonesha kuwa vifo vya akinamama wajawazito vimepungua kutoka 529 mwaka 1990 hadi 454 mwaka 2010 kwa kila vizazi hai

100,000, maambukizi ya UKIMWI yamepungua kutoka wastani wa Taifa wa asilimia 5.7 hadi asilimia 5.1, kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka vifo 137 mwaka 1996 hadi 81 mwaka 2010 kwa kila vizazi hai 1,000 na kuimarika kwa huduma za afya ya uzazi na ongezeko la idadi ya watu Mijini kufikia asilimia 26 mwaka 2012 kutoka asilimia 20 mwaka 2000; na

(ii) Siku ya Idadi ya Watu Duniani iliadhimishwa kitaifa Mkoani Morogoro tarehe 11 Julai, 2012. Maadhimisho hayo yaliambatana na maonesho ya wadau mbalimbali walioelimisha jamii juu ya faida na changamoto kubwa za ongezeko la idadi ya watu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa. katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2012/2013, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilikabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Idadi ndogo ya wataalam, hasa wachambuzi sera: Kwa ujumla, Tume ya Mipango ina upungufu wa wataalam 61 wenye weledi katika nyanja mbalimbali. Upungufu huu unatokana na muundo mpya wa tume, pengo la watumishi waliohama, kuacha kazi na kustaafu. Ili kuziba pengo hili, kwa mwaka 2013/2014, Tume ya Mipango imewasilisha maombi ya ajira mpya 50, ambapo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imesharidhia na kutoa kibali hicho.

Sambamba na kuongeza idadi ya watumishi, juhudi za kuwapatia watumishi waliopo fursa zaidi za mafunzo kazini zinaendelea;

(ii) Wafadhili kutotekeleza ahadi zao kwa wakati: Miradi yote mitatu chini ya Tume ya Mipango inatekelezwa kwa fedha za wafadhili. Hadi Machi 2013, kiasi cha asilimia 20.36 tu za fedha zilizoahidiwa ndizo zilikuwa zimetolewa. Kiasi hicho ni kidogo mno ikilinganishwa na mpango wa mtiririko wa fedha *(cash flow plan)* uliokusudiwa kwa utekelezaji wa miradi hiyo kwa kipindi husika;

(iii) Uelewa mdogo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, miongoni mwa wadau: Mapitio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yanaonesha kuwa licha ya hatua zilizofikiwa, mafanikio bado yako chini ya malengo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Dira bado haieleweki vyema miongoni mwa wadau walio wengi. Hii ni changamoto kubwa kwa kuwa wadau wanapaswa kuwa ndio watekelezaji wakuu wa malengo ya Dira. Kwa kutambua hili, Tume imefanya jitihada mbalimbali za kutangaza Dira kwa wadau, ikiwa ni pamoja na kupitia tovuti, warsha, vipeperushi na vyombo vya habari ili kuongeza uelewa wa wadau kuhusu nafasi na wajibu wao katika utekelezaji wa Dira na malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya utekelezaji na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2012/2013, sasa ningependa kuchukua fursa hii kuainisha kwa muhtasari maeneo ambayo Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itayapa kipaumbele katika mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

(i) Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itaendelea na utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

(ii) Usambazaji wa machapisho mbalimbali ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/ 2014, Tume ya Mipango itaendelea kutengeneza vipindi vya luninga, redio na makala kwenye magazeti kwa lengo la kuwaelimisha wananchi juu ya mipango ya maendeleo ya nchi. Pia Tume ya Mipango itaendelea kusambaza nyaraka mbalimbali kupitia tovuti na vyombo vya habari. Nyaraka hizo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo, Mpango Elekezi, Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo wa mwaka.

(iii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 na ule wa Miaka Mitano, 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2013/ 2014, Tume ya Mipango itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kupitia ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013.

(iv) kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2013/2014, Tume ya Mipango itaendelea kuibua na kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo ya kiuchumi

na kijamii. Jumla ya tafiti nne zitaibuliwa na kuanza kufanyika katika mwaka huo.

(v) Kuratibu Mfumo mpya wa Ufuatiliaji na Kuendesha awamu ya pili ya *labs.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Tume ya Mipango itaratibu uanzishwaji mfumo mpya wa kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ambao utahusisha kuanzishwa wa chombo maalum kiitwacho *President's Delivery Bureau.* Aidha, Serikali itajumuisha katika mpango wa maendeleo wa mwaka baadhi ya miradi ya maendeleo iliyochambuliwa kwa kina katika awamu ya kwanza ya *labs*. Aidha, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na *PEMANDU* ya Malaysia itaendelea na awamu ya pili ya kufanya uchambuzi wa kina wa miradi ya maendeleo kwa njia ya *lab*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2013/2014, Tume ya Mipango itatekeleza miradi mitatu ifuatayo:-

(i) Mradi wa Kuhakikisha Ukuaji wa Uchumi Unashirikisha walio Wanyonge na Maendeleo Endelevu Kimazingira *(Pro-Poor Economic Growth and Environmental Sustainable Development Project);*

(ii) Mradi wa Kufuatilia Idadi ya Watu *(Population Planning Project); na*

(iii) Programu ya Tekeleza sasa kwa Matokeo Makubwa *(Big Results Now Programme).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Bajeti 2014; katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaomba Sh. 37,696,984,000/=.

Kati ya fedha hizo, Sh. 5,860,055,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, yaani mishahara na matumizi ya kuendesha Ofisi na kutekeleza kazi za msingi za Tume zilizoorodheshwa na Sh. 31,836,929,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa kiasi hiki ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida, Mishahara ni Sh. 1,394,246,000/=, Matumizi Mengineyo ni Sh. 4,465,809,000/=. Jumla ni Sh. 5,860,055,000/=. Matumizi ya Maendeleo kwa fedha za ndani Sh. 5,264,300,000/= na fedha za nje ni Sh. 26,572,629,000/=. Jumla ya fedha zote za Miradi ni Sh. 31,836,929,000/=. Jumla ya Fungu 66 ni Sh. 37,696,984,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru wananchi wote wa Bunda kwa kuendelea kuniamini kuwawakilisha. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais kwa hotuba yako ambayo imetufisha mahali pazuri sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais inahusisha mafungu nane, Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu); Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 9 Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, na Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata muda wa kutosha wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Celina O. Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu pamoja na Mheshimiwa George Mkuchika Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Aidha, Katika maelezo hayo Kamati ilielezwa kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imefanyia kazi maoni ya Kamati. Naipoingeza Ofisi ya Rais na Serikali kwa ujumla kwa kutekeleza maagizo ya Kamati. Aidha, kwa yale maagizo ambayo utekelezaji wake uko katika hatua za awali, Kamati inashauri kuwa ni vyema yafuatiliwe kwa makini ili yaweze kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Ufinyu wa bajeti unaotokana na ukomo wa kibajeti. Changamoto hii imekuwa ni kikwazo katika kuleta ufanisi kwani majukumu mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais yanashindwa kutekelezwa kutokana na kukosekana fedha za kutosha.

Aidha, pale inapotokea kwamba kuna fedha zimetengwa mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa jambo fulani, fedha zimekuwa zikichelewa kutoka Hazina hivyo kutofautiana na mpango kazi ambao Ofisi inakuwa imekwishajiwekea kwa muda uliopangwa.

(ii) Vile vile Idadi ndogo ya Watumishi. Kwa kweli Taasisi zinakabiliwa na upungufu wa wataalamu katika nyanja mbalimbali. Mfano Tume ya Mipango ina upungufu wa wataalam 44 na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ina upungufu wa watumishi 400.

(iii) Baadhi ya wafadhili kutotekeleza ahadi. Hii ilijitokeza katika majadiliano ya bajeti ya Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango, ambapo ilionekana kuwa miradi yote mitatu ya Tume ya Mipango inatekelezwa kwa fedha za wafadhili pekee. Hadi kufika mwaka 2012, kiasi cha asilimia 20.36 tu cha fedha ndicho kilichokuwa kimepatikana. Hii ni changamoto kubwa inayopelekea Taasisi hii kushindwa kutekeleza miradi kama ilivyokusudiwa.

(iv) Uelewa mdogo kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yanaonyesha kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo bado haieleweki vyema kwa wadau. Hii ni changamoto kubwa kwani watekelezaji wa Dira hawajapata uelewa juu ya Dira yenyewe na wajibu wao katika kuitekeleza.

(v) Uelewa mdogo katika miradi ya *TASAF III* na MKURABITA. Katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF* awamu ya tatu wananchi wengi wamekosa uelewa wa kutosha na kusababisha miradi ama kutokamilika au kutotekelezeka ipasavyo. Aidha, kwa upande wa MKURABITA mpango wa urasimishaji ardhi na urasimishaji biashara haijaeleweka ipasavyo kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa na kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa mbele ya

Kamati, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Ofisi hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, yapo mambo mbalimbali yaliyojadiliwa, hii ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa majukumu katika Taasisi hii. Kamati inatambua kazi mbalimbali zinazofanywa na Ofisi ya Rais Ikulu. Hata hivyo, kwa upande wa Baraza la Mawaziri Kamati inashauri kuwa ili kuboresha utendaji kazi kwa viongozi wa nchi yetu, ni vyema uanzishwe utaratibu wa kujaza Mikataba ya Upimwaji kazi, yaani *performance contract* kwa Mawaziri na Sekretarieti yote ya Baraza la Mawaziri kwa lengo la kuboresha ufanisi wa kazi kwa ngazi za viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia utekelezaji na makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Rais mtoa hoja aliieleza Kamati namna taasisi hii inavyofanya kazi na kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa watumishi, ucheleweshwaji wa mashauri yanayohusiana na rushwa, upungufu wa Ofisi za Kanda katika maeneo mbalimbali hapa nchini hususan Mikoa na Wilaya mpya na uelewa mdogo wa wananchi kuhusiana na masuala ya rushwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali izingatie mambo yafuatayo ili kuiwezesha Taasisi hii kukabiliana na changamoto zinazoikabili:-

(1) Takukuru waongezewe uwezo wa kifedha ili waweze kutoa elimu kwa umma kuhusiana na athari za rushwa kwa wananchi, Watumishi wa Serikali, makampuni binafsi na hata zile zinazojitokeza katika chaguzi na mikataba mbalimbali. Aidha, Kamati inaona kuwa ni vyema elimu ya kupambana na rushwa

ifundishwe shuleni. Lengo ni kupanua wigo wa elimu inayohusu rushwa na kuisaidia taasisi kupambana na rushwa hapa nchini kwani rushwa ni adui wa haki.

(2) Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi katika Taasisi hii ni vizuri Takukuru wakapewa fursa ya kuajiri kwa nafasi 400 walizoomba kwa lengo la kuongeza ufanisi katika zoezi zima la kuzuia na kupambana na rushwa. Aidha, Kamati inashauri Taasisi hii ipewe nafasi ya kuweza kufungua ofisi katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kuongeza ufanisi wa chombo hiki madhubuti cha kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ucheleweshwaji wa mashauri yanayohusu rushwa linaonekena kuwa changamoto kubwa kwa Taasisi hii. Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali ikaendelea kushughulikia na kutafakari changamoto hii kwa haraka zaidi. Mbali na hayo, katika kujadili bajeti lilijitokeza suala la ufinyu wa mashauri yanayofanyiwa kazi ikilinganishwa na yale yanayojitokeza. Kamati inashauri kuwa iko haja ya kushughulikia mashauri yote ya rushwa kikamilifu. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia Februari, 2013 taarifa zilizopokelewa ni 3,280 majalada yaliyofunguliwa 773, yaliyopelekwa kwa *DPP* ni 191 na kesi zilizoshinda ni 33.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, utafiti ufanyike kutoka katika maeneo na nchi mbalimbali kuona jinsi chombo kama hiki kinavyofanya kazi. Hii itasaidia nchi yetu kupata uzoefu wa kutosha na kujifunza kutoka katika nchi mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Takukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

Na. 11 ya 2007, kwa kiasi kikubwa sheria hii imesaidia kudhibiti rushwa nchini. Lakini pamoja na sheria hiyo iko haja ya chombo hiki kutambulika ipasavyo na kupewa nguvu ya kushughulikia rushwa kikamilifu. Jambo hili lilijadiliwa kiundani katika Kamati, na Kamati inashauri kwamba, chombo hiki kitajwe katika Katiba ya Nchi kama vilivyotajwa vyombo vingine vinavyosimamia haki nchini kwa lengo la kuipa Taasisi nguvu ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuwa ibuni mbinu mpya na kuongeza juhudi katika kushughulikia maeneo sugu yanayoendelea kujihusisha na rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano ya bajeti lilijitokeza suala la kutofahamika na kutambulika vizuri kwa Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba ni vyema MKURABITA ikajengewa uwezo ili waweze kutoa elimu kwa wanachi katika maeneo mbalimbali hususan vijijini kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuelewa dhana shirikishi ya MKURABITA. Kamati imebaini kwamba yapo maeneo ambayo wananchi hawafahamu uwepo na umuhimu wa mradi huu muhimu. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba ni vyema mradi huu ukaongezewa uwezo wa fedha ili waweze kwenda katika maeneo ya Wilaya zote za Tanzania kwa lengo la kusambaza mpango huu kwa nchi nzima kwa lengo la kuwanufaisha Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata taarifa ya miradi ya Mfuko wa *TASAF* kwa Awamu ya Tatu iliyozinduliwa Mwaka 2012 mjini Dodoma. Awamu hii inalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika awamu zote mbili zilizopita. Hata hivyo, tarehe 19/03/

2013 Kamati ilifanya ziara na kukagua awamu ya tatu ya Mradi wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini katika kijiji cha Mataya. Vile vile ilitembelea mradi wa *TASAF* wa ujenzi wa jengo la utawala uliopo shule ya sekondari ya Dunda katika Halmashauri ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo yapo mambo mbalimbali yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na changamoto ambapo iliripotiwa kutotosheleza kwa fedha zinazotolewa katika kuendesha miradi na mahitaji halisi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa samani katika madarasa yanayojengwa. Changamoto nyingine ni uelewa mdogo wa wanachi katika kuanzisha na kuendesha miradi ya awamu ya tatu *(TASAF III).* Ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaishauri *TASAF* watoe elimu kwa wananchi kabla ya kuanza kutekeleza mradi wowote kwa lengo la kuwajengea uelewa wananchi ili kuleta mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kamati inashauri *TASAF* iweke usimamizi mzuri wa fedha ikiwa ni pamoja na Taasisi hii kusimamia fedha zake yenyewe katika miradi iliyopo Serikali za Mitaa, kuliko kuajiri mtu kutoka nje ya *TASAF* katika kila Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(Presidential Trust Fund)* ulianzishwa mwaka 1983 na shughuli zake kuanza rasmi mwaka 1984. Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali za kuendeleza uchumi wa nchi na kuwakwamua watu wa hali ya chini kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi na shughuli mbalimbali za kiuchumi, ili kuongeza kipato na ajira kwa madhumuni ya kupunguza umaskini na kuongeza uzalishaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi mijini na vijijini.

Mhesimiwa Naibu Spika, Kamati ina ushauri ifuatao kuhusu mfuko huu:-

(i) Mfuko uongezewe fedha kwa lengo la kuuwezesha kutoa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali ili kufufua shughuli za mfuko na kutoa huduma bora kwa wateja;

(ii) Kuwe na utaratibu wa wazi wa kutoa na kupokea fedha katika mfuko huu; na

(iii) Kamati inashauri mfuko huu uangalie riba ya mikopo kwa wateja wake ili Riba ipungue ikilinganishwa na Benki za hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais menejiment ya Utumishi wa Umma Fungu 32 imeendelea kutekeleza majukumu yake katika kuajiri na kuhudumia watumishi wa umma. Tarehe 20/03/2013 Kamati ilitembelea Wizara hii.

Pamoja na mambo mengine Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeongeza maslahi kwa watumishi wa umma, na imejitahidi kusimamia mchakato wa ajira, ambapo kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imeongeza idadi katika kuajiri watumishi wapya kufikia idadi ya 22,799 ambapo kiapaumbele ni kutoka katika Sekta ya Afya, Elimu, Mifugo na Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Wizara hususan katika kuongeza ajira na kuboresha mishahara. Aidha, Kamati inashauri kuwa ongezeko la mishahara ni vizuri likajielekeza zaidi katika kuzingatia ukuaji wa uchumi, kwamba uchumi unapoboreka Serikali ijitahidi kuongeza kipato cha wananchi. Lengo ni kutoa motisha kwa Watumishi wa

Umma na kupunguza mianya yoyote ya rushwa itakayoweza kujitokeza.

Aidha, msisitizo wa Kamati ni kwa wale watumishi hewa na wasiowajibika, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka katika kuwabaini watumishi hewa na kufuatilia wale watumishi wote wasiowajibika ipasavyo. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa kwa wale watumishi ambao wanathibitishwa kukutwa na makosa, ni vizuri wachukuliwe hatua za kinidhamu na siyo kuhamishwa kutoka Kituo kimoja cha kazi hadi kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kuuliza namna Wizara ilivyojipanga katika kufuatilia na kuzingatia maadili ya watumishi katika Wakala wa Serikali, Wizara na Idara mbalimbali za Serikali na zile zinazojitegemea. Kamati ilielezwa kwamba ufuatiliaji wa maadili umefanyika katika maeneo mbalimbali nchini hususan katika maeneo tajwa na matokeo ya ufuatiliaji yanaonyesha kuwa asilimia 89.5 ya malalamiko ya ukiukwaji wa maadili yamefanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa pamoja na ufatiliaji huo elimu ya ukuzaji wa maadili hususani katika eneo la kuzuia rushwa na utunzaji siri kwa watumishi wa Umma iendelee kutolewa kwa kasi zaidi kwa lengo la kuboresha maadili kwa Watumishi wa Umma wa kada mbalimbali nchini Tanzania.

Vile vile**,** Kamati inaishauri Serikali kuwa ili kuboresha nidhamu ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma ni vyema mfumo wa wazi wa kupima Utendaji Kazi wa mtumishi, *Open Performance Appraisal System (OPRAS)* ulioanzishwa kwa lengo la kufuatilia utendaji kazi wa Watumishi wa Umma ni vyema ukatafutiwa mbinu maalum ya kuzingatiwa kwa lengo la kusaidia kuboresha nidhamu ya uwajibikaji katika utumishi wa

umma. Aidha, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma kuwa ni vizuri zoezi la kupima uwezo wa uwajibikaji likaimarishwa hata kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji wa viongozi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinua vipaji na uchumi wa nchi yetu ni vyema Ofisi na Taasisi za Serikali zikajiwekea utamaduni wa kununua samani za Ofisini kutoka ndani ya nchi, hii ni kutokana na ubora wake zikilinganishwa na zile zinazotoka nje ya nchi.

Agizo hili limetekelezwa na baadhi ya Taasisi mbalimbali zilizopo hapa nchini, mfano mzuri ni Wakala wa Serikali Mtandao *(eGA)* iliyopo chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika ziara iliyofanywa katika Taasisi hii, Kamati ilifarijika kuona ununuzi wa samani nzuri zinazotengenezwa ndani ya nchi. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa ni vyema Taasisi nyingine za Serikali zitekeleze agizo hili kwa lengo la kupata samani nzuri kwa bei nafuu na zinazodumu kwa muda mrefu. Aidha, ununuzi wa samani za ndani ya nchi utaongeza ajira kwa wananchi na kukuza uchumi wa chi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lilijitokeza suala la kuongezeka kwa gharama ya umeme katika maeneo mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii. Kamati inashauri kuwa matumizi ya umeme mbadala kama wa jua *(Solar)* pamoja na vyanzo vingine vya umeme yazingatiwe ili kupunguza ongezeko la gharama ya umeme katika Taasisi mbalimbali. Aidha, Kamati inashauri kuwa kwa Taasisi zote za Serikali ni vizuri zikaingia katika mfumo huu wa matumizi ya umeme mbadala kwa lengo la kupunguza gharama zozote za umeme zitakazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojitokeza katika kuchambua makadirio ya bajeti ya Ofisi hii ni kupanda kwa gharama za ukarabati na ukodishaji wa majengo. Mfano Taasisi moja inakodisha jengo kwa Shilingi milioni 200 kwa mwaka na nyingine inakarabati jengo kwa Sh.138,600,000/= kwa mwaka kiasi ambacho ni kikubwa sana. Kamati inashauri kuwa ili kuondokana na gharama hizi, kila Wizara/Taasisi ambazo hazina majengo yake zifanye jitihada za kupata viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi. Hii itasaidia Wizara kuepukana na gharama za kukodi Ofisi, kwa siku za mbeleni na miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Fungu 67. Kwa mujibu wa kifungu cha 29(4) cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na 18 ya Mwaka 2007 Sekretarieti ya Ajira inalo jukumu la msingi la kuendesha mchakato wa ajira wa Watumishi wa Umma kwa niaba ya waajiri nchini. Wajibu wao mkubwa ni kutangaza, kusaili, kutoa matokeo ya usaili na kuwapangia vituo watumishi wapya kwa mujibu wa matokeo ya usaili.

Kamati inashauri kuwa ajira nyingine za Serikali za Mitaa kwa ngazi za chini ziondolewe kutoka kwenye Sekretarieti ya Ajira na kuziachia Taasisi au Mamlaka husika kuajiri zenyewe. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kuleta Bungeni Muswada wa marekebisho wa sheria hii husika. Agizo hili linatolewa katika bajeti hii kwa mara ya pili kwani lilitolewa kwa mara ya kwanza katika bajeti ya 2012/13 na utekelezaji wake unaonekana kukawia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuboresha utendaji kazi ni la muhimu kwa taasisi zote na lina maslahi kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa kusema hivyo, Kamati inaishauri Sekretarieti kuwa ni vema wakati wa

kuandaa bajeti wawe wanaweka makisio kwa maeneo mbalimbali ambayo ajira zitaweza kuhitajika/kujitokeza. Hii itasaidia Sekretarieti kuajiri kwa wakati na kukaa vikao vinavyotakiwa kwa Mwaka wa Fedha inavyopaswa kwa kufanya hivyo itasaidia Taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano ya bajeti ya ofisi hii, lilijitokeza suala la kuongezeka kwa gharama za ukarabati wa pango kwa ajili ya Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira ambazo kwa mwaka ni Sh. 138,600,000/=, kwa miaka mitano fedha hizo zingeweza kujenga jengo la Taasisi hiyo.

Kwa minajili hiyo Kamati inashauri kwamba Sekretarieti ya Ajira ijitahidi kujenga majengo yake yenyewe ili kupunguza gharama za kukodi pango zinazoendelea kujitokeza.

Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Sekretarieti ifungue Ofisi zake za Kanda katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kupata vituo mbalimbali vya kufanya usaili kwa wanaotafuta nafasi za ajira katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kazi zinazofanywa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Pamoja na kazi hizo, Kamati inashauri kuwa Sheria na taratibu za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma zifanyiwe marekebisho. Aidha, suala la maadili lijumuishe na masuala mengine mbalimbali na siyo masuala ya mali peke yake.

Vilevile Serikali inashauriwa kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kuondokana na gharama za ukodishaji wa pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Umma ni Tume Rekebu iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza jukumu lake kubwa ikiwa ni pamoja na kusimamia uendeshaji wa Raslimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Aidha, Kamati inashauri kwamba, elimu kwa wananchi kuhusu shughuli zinazofanywa na Tume ya Utumishi wa Umma iendelee kutolewa kupitia njia mbalimbali kama vyombo vya habari, maonyesho na ziara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Bodi ya Mishahara na Maslahi, pamoja na majukumu mengine imefanya tafiti ya kuchambua na kutoa ushauri kuhusiana na mishahara na maslahi kwa Kamati za Kudumu za Utendaji, na vyombo vya ulinzi na usalama. Aidha, Kamati inaishauri Bodi hii kuzingatia uchumi wa nchi katika kuboresha mishahara ya watumishi wa umma, kwamba kila uchumi unapoboreshwa ni vizuri pia mishahara ya watumishi ikaongezeka, hasa kwa kuzingatia tija na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Bodi iwe makini na malimbikizo ya mishahara, mishahara hewa na madeni mbalimbali ya watumishi kama Walimu na wafanyakazi wa kada nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Tume ya Mipango imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia uchumi wa nchi yetu, kubuni sera za uchumi wa nchi na kutoa Dira na Mwongozo wa Uchumi wa Taifa. Tunapaswa tukumbuke kwamba Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2013/2014 ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hata hivyo Kamati

imebaini kwamba Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 bado haieleweki ipasavyo, hivyo ni ushauri wa Kamati kwamba elimu ya kutosha itolewe kwa wadau na watekelezaji wa Dira.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Tume ya Mipango, Tume ya Mipango inapaswa itengewe fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kuliko kutegemea fedha za wafadhili kama ilivyoelezwa kwenye utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni maombi ya fedha na malengo ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombihaya ya fedha yaingie kwenye *Hansard* kama yanavyoonyeshwa kwenye kitabu cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake ili kutekeleza majukumu yake inaomba fedha kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 20: Ofisi ya Rais Ikulu Sh. 9,248,595,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.

(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri Sh. 242,781,448,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida na Sh. 59,587,357,000/= kwa miradi ya maendeleo.

(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Sh. 23,564,680,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida, na Sh.19,320,000,000/= kwa matumizi ya miradi ya maendeleo.

(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ta Maadili ya Viongozi Sh. 6,165,883,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida na Sh. 3,083,543,800 kwa matumizi ya miradi ya Maendeleo.

(e) Fungu 67: Sekretarieti ya Ajira Sh. 2,949,833,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.

(f) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma Sh. 11,064,526,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.

(g) Fungu 9: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma Sh. 2,213,882,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.

(h) Fungu 66: Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Sh. 5,860,055,000/= kwa Matumizi ya kawaida na Sh. 34,736,929,000/= kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa napenda kuchukua nafasi hii kuhitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi, busara, hekima, uchapakazi na umakini uliopo katika Serikali na Ofisi hii ya Rais. *(Makofi)*

Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, tunakupongeza kwa busara zako katika kuliongoza Bunge letu Tukufu lenye changamoto nyingi hasa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Celina O. Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi

ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira - Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Charles Mkuchika - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati Kamati ilipochambua makadirio ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge wote wanaonisikiliza na kipekee Wajumbe mahiri, wataalam wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2012/2013. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Utawala, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana – Mwenyekiti, Mheshimiwa William M. Ngeleja - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Jason S. Rweikiza, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine na Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia

Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Haika Mtui na Matamus Fungo, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kwa kuwasilisha ripoti ya Kamati yako vizuri namna hiyo. Sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora pamoja na Uratibu na Mahusiano nawe pia utatumia nusu saa kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati ametumia nusu saa. Naomba nikukaribishe Profesa.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA PAMOJA NA URATIBU NA MAHUSIANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitahusika na masuala ya Utawala Bora, na naomba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard* kwa sababu ni ndefu na muda niliopewa hautoshi.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kahigi, samahani, kidogo tu dakika chache, kuna taarifa unataka kupewa. Kaa kidogo tu, nitalinda muda wako.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 68(1) naomba mwongozo wako. Ukisoma hii taarifa ya kutoka Kambi ya Upinzani kuanzia *page* ya kwanza pale namba mbili pale Utawala Bora mpaka *page* ya nne *paragraph* ya mwisho, naomba mwongozo wako. Ukisoma kilichoandikwa hapo ndani, cha kwanza, utaona tunaingilia uhuru wa Mahakama.

Mambo mengi yaliyoandikwa hapa ndani ni jambo ambalo lipo Mahakamani. Ni juzi tu Mheshimiwa Akunaay wa CHADEMA alitukumbusha hapa Bungeni kwamba haya tunayoyasema ni *prejudice to the Court*, na sidhani kama Bunge lako Tukufu tunaweza sasa leo tukaanza kujadili mambo ambayo yapo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, unaona hapa tunataka kufanya jambo ambalo lipo Mahakamani kulifanyia siasa. Hii ni hatari sana kwa mustakabali wa nchi yetu. Lakini la tatu, litakuwa Taifa la ajabu sana duniani kama leo tunakuja hapa kama Bunge tunataka kuongea mambo ambayo tuna-*elude*

*credibility* ya nchi yetu, tuna-*elude credibility* ya Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Nitakusikiliza Mheshimiwa Mnyika lakini nataka nimsikilize Msemaji kwanza mwenyewe. Profesa una cha ku-*comment* kuhusu hotuba yako kama ilivyoelezwa na Mbunge mwenzako?

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tu niendelee kusoma.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kumpa taarifa tu mzungumzaji aliyetangulia, ame-*refer* hotuba ya Kambi kabla hata haijasomwa, ukurasa wa Kwanza hakuna jambo lililopo Mahakamani kilichoandikwa tu ni kuhusiana na tuhuma za utekaji kuhusu Usalama wa Taifa.

Ukurasa wa pili umezungumzia kiapo cha Dkt. Ulimboka ambapo katika haya yaliyozungumzwa ukurasa wa pili hakuna jambo lolote lililopo Mahakamani. Kumezungumzwa kufungiwa kwa Mwanahalisi ambalo haliko Mahakamani, masuala ya Kibanda hayapo Mahakamani. Ukurasa wa tatu imezungumzwa kazi za Usalama wa Taifa ambazo haziko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba tu Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani aruhusiwe kuendelea kuisoma hotuba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepewa taarifa, naomba niijibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba, tuachie. Mheshimiwa Chief Whip Tafadhali.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba sijakupa nafasi. Mheshimiwa *Chief Whip*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako tu, tunaweza tukafanya sarakasi nyingi sana. Lakini ukurasa wa tatu huu umetaja kwa jina kesi ya Lwakatare.

**MJUMBE FULANI:** Ukurasa wa nne.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Sawa, ukurasa wa nne. Lakini... Sasa nasema mimi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wazungumzaji wengine, maana mimi sikusema wakati wanasema. Nami nikisema na wenyewe wasikilize tu. Ukurasa huu aliousema Mheshimiwa Peter Serukamba ni utangulizi unaoendelea kuzungumzia masuala yaliyopo kwenye Mahakama na ndiyo maana amesema kesi ya Lwakatare ipo Mahakamani.

Kwa mujibu wa kuondoa kesi iliyopo Mahakamani kuifanya iwe kwenye siasa na kwa kweli ni kuingilia uhuru wa Mahakama na tunakiuka Kanuni

ya 64(1)(c). Inakiukwa hapa kwa kuzungumzia mwenendo wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, hata hayo anayoyasema hayakuandikwa kwenye Kanuni Mheshimiwa Serukamba, ni kinyume cha Sheria ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unayo Sheria ya Usalama wa Taifa hapo. Hairuhusiwi katika Kifungu cha 16 kutaja humu ndani au kutangaza hata majina ya watu/watumishi wa Usalama wa Taifa. Sheria ipo hapa, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema; naomba Waheshimiwa Wabunge mkae, mimi nimeshasimama.

**MBUNGE FULANI:** Bwana! Wewe Kiti? Ah!

**NAIBU SPIKA:** Kama tulivyokwishasema, suala la muda ni muhimu sana katika Bunge hili ili kutenda haki, na muda wetu kwa kweli hauruhusu. Lakini jambo hili limejitokeza ndani ya Kipindi hiki cha Bunge la ku-*refer* baadhi ya mambo ambayo yapo Mahakamani. Mheshimiwa aliyetukumbusha humu ndani alikuwa ni Mheshimiwa Akunaay kwamba suala hili ambalo lilikuwa limeandikwa kwenye hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na likaleta kasheshe humu ndani, alitukumbusha akatumia neno '*subjudice*', na sote tutakubaliana kwamba baada ya pale, Mheshimiwa

Spika akasema sasa mambo kama haya yasiendelee tena.

Kwa hiyo, yalishatolewa *Ruling.* Kama kweli hotuba hizi mnaziandika kama Kambi na haziandikwi na watu wachache, mimi nashangaa ni kwa nini mambo haya haya tena bado yanarudi kwenye uwanja ule ule ambao kwa kweli tulikubaliana sote kwamba mambo haya ambayo yapo Mahakamani siyo vizuri sana kuyaleta ili yaweze kujadiliwa hapa.

Vinginevyo mnakipa Kiti wakati mgumu sana kuzuia Mbunge mwingine yeyote atakapoanza kuyaongelea mambo haya haya, itakuwa ni tatizo kubwa sana.

Kwa hiyo basi, *ruling* yangu ni kwamba kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa nne, kwa mambo yote yanayohusu masuala yanayohusiana na Usalama wa Taifa, Dkt. Ulimboka na Lwakatare...

*(Hapa Mheshimiwa Halima Mdee alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, Kanuni zetu zinasema ninapokuwa mimi nimesimama, siyo vizuri kufanya hivyo. Lakini vile vile Chief Whip ninapokuwa na mimi naongea na wewe unasema haiwezekani huko inakuwa haipendezi. Lakini kwa heshima yenu kwa sababu wote wawili ni wanasheria, nianze na ninyi kwa kuwapa upendeleo maalum kwa dakika mbili mbili tu, mtusaidie. Maana mambo haya ni ya kisheria. Tuanze na Halima utamalizia *Chief Whip*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ukurasa wa kwanza mpaka wa tatu haujataja jina la Lwakatare kabisa. Ukurasa wa nne ndiyo umetaja jina la Lwakatare, lakini haujazungumzia mwenendo wa

kesi, wamezungumzia yaliyojiri kuelekea kukamatwa kwake.

Kwa hiyo, siyo sahihi kabisa kusema kwamba ukurasa wa kwanza mpaka wa tatu hautakiwi kuzungumzwa kwa sababu kuna kesi Mahakamani wakati hakuna kesi yoyote ambayo inahusiana na maelezo yaliyotolewa ukurasa wa kwanza, maelezo yaliyotolewa ukurasa wa pili ama maelezo yaliyotolewa ukurasa wa tatu.

Hizo hoja ambazo anazileta Mheshimiwa Lukuvi, sijui kwamba kuna Sheria ya Usalama wa Taifa ambayo inakataza sijui mambo gani yasizungumzwe; nadhani yeye angetutajia hiyo Sheria, atutajie hivyo vipengele ambavyo vinakatazwa, kisha alinganishe na hiki kilichoandikwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hotuba iendelee kama inavyopaswa kwa sababu kilichoandikwa hapa hakuna kipya. Hakuna kitu kisichojulikana. Tunalileta mbele ya Bunge lako Tukufu ili Serikali iweze kutekeleza wajibu wake dhidi ya watuhumiwa ambao wako humu, ambao wanaendelea kufanya uhalifu miaka nenda miaka rudi. Ni hayo tu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Nilimpa nafasi Mheshimiwa Tundu Lissu. Utapata nafasi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijasema ninachotaka kusema, niseme tu kwamba, ninayo Sheria hapa ya Idara ya Usalama wa Taifa na Ujasusi ya Mwaka 1996, Sheria Namba 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno kwamba masuala yanayohusu Idara ya Usalama wa Taifa hayazungumziwi Bungeni, ni maneno ya kuokoteza Mitaani, ambayo hayapo katika Sheria yoyote ya nchi hii.

Kitu ambacho kinakatazwa kuzungumzwa huko kwenye magazeti, kwenye Mikutano ya hadhara na mahali pengine ni *disclosure* ya watu wanaofanya kazi Idara ya Usalama wa Taifa. Hiyo *prohibition,* hayo makatazo yanahusu huko, siyo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Usalama wa Taifa inaongozwa na Mkurugenzi ambaye anapewa maelekezo na Waziri anayehusika na masuala ya Usalama wa Taifa, kwa mujibu wa Sheria hii, ndiye anayeipa Idara ya Usalama wa Taifa Maelekezo ya namna ya kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria.

Kama kuna mambo yamefanyika hovyo huko nje na Idara ya Usalama wa Taifa, anayetakiwa kuwajibishwa na Bunge, ni Waziri aliyeleta hotuba yake hapa. Namna ya kumwajibisha ni kumruhusu mzungumzaji azungumze masuala yanayohusu Idara ya Usalama wa Taifa, inayowakilishwa humu ndani na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa hatari kama Bunge lako Tukufu litakatazwa kwa hoja za ajabu ajabu tu, kuzungumza masuala muhimu ya utendaji wa Idara za Serikali zinazotumia fedha za wananchi na zinazotakiwa kuwajibika ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hakuna mahali kesi imetajwa. Hakuna! Hakuna

mahali popote ambapo *nature* ya ushahidi uliotolewa Mahakamani imezungumzwa. Hakuna!

Watu wengi humu hawafahamu maana ya hiyo *rule* ya *subjudice.* Hayo makatazo yanahusu nini? Yanahusu kuzungumza ushahidi uliozungumzwa Mahakamani kwa namna ambayo ita-*influence* uamuzi wa Mahakama. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Maliza! *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize.

**NAIBU SPIKA:** Nawaomba Waheshimiwa wote ambao mnataka kuongea, nawahakikishia kwamba nitawapa nafasi na Mheshimiwa Tundu Lissu amalizie kwa kifupi sana. Lakini wale watatu ambao mmesimama kwa sasa hivi, nitawapa nafasi wote, kwa sababu muda tunao. Msiwe na wasiwasi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imezungumzia ushahidi uliotolewa Mahakamani kwa kesi yoyote ile, mimi nitakuwa wa kwanza kukuunga mkono kwamba hizo *portions* ziwe *deleted.* Nitakuwa wa kwanza. Lakini kama hakuna mahali popote ambapo kesi imezungumzwa, kama hakuna mahali popote ambapo ushahidi wa hizo kesi umezungumzwa, kumkataza Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuzungumza, ni kuziba mdomo Kambi Rasmi ya Upinzani na hicho kitendo hakitakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa naomba, wasemaji watatu watakuwa ni wa mwisho, baada ya hapo nitatoa *rulling* yangu. Tutaanza na Taarifa ya

Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu Mheshimiwa Peter Serukamba, wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Sendeka, halafu nitatoa *rulling* yangu.

Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu, kidogo alikuwa anapotosha. Ukisoma kifungu cha 16 (1) cha Sheria hii ya Usalama wa Taifa, kinaeleza bayana kwamba, "hairuhusiwi kwa mtu yeyote bila ya kupata ruhusa ya maandishi kutoka kwa Waziri mwenye dhamana, kutangaza au kuchapisha au kuruhusu kitu chochote kuchapishwa katika gazeti au katika nyaraka yoyote mtu yeyote ambaye yupo katika Usalama wa Taifa, isipokuwa Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa." Ni dhahiri kabisa ukiangalia katika Taarifa hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ametaja jina. Amewataja akina Ramadhani na watu wengine. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**NAIBU SPIKA:** *Order, order, order!* Tusikilizane na tuvumiliane, kila Mbunge asikilizwe na avumiliwe. Ahsante. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nilitaka niwasomee na wananchi waelewe kwamba, wanasema suala la kesi halijatajwa kwenye ripoti yao. Nenda *page* ya nne.

**WABUNGE FULANI:** Mwenendo!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** *Come on, fuck you!*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba, ndiye mwenye nafasi ya kusema. Endelea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhidi ya kesi inayomkabili Mkurugenzi wa Usalama wa *CHADEMA,* Ndugu Wilfred Lwakatare.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, hapa kuna kesi iko Mahakamani na inamtuhumu huyu Bwana Lwakatare kwa Ugaidi. Tunasema haiwezekani tuje hapa Bungeni, eti tuanze kujadili jambo hilo. Mwenendo ni upi? Tunachoongelea hapa na Kanuni yetu inasema? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani nimeshakupata. Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Sendeka, halafu nitatoa *rulling* yangu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo ambalo wala hatuna haja ya kubishania.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nilikuwa nimeomba mimi, lakini mbona ameninyima!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kuhusu ukurasa wa nne, Hotuba ya Kambi ya Upinzani, inataka achukuliwe hatua mtu ambaye wao wanadai ndiye aliyegushi na kutengeneza ushahidi wa uwongo dhidi ya ndugu Lwakatare na jambo hili liko Mahakamani. Huo ni mwenendo. Kama wanasema huyu amegushi, wakati kesi iko Mahakamani ni jukumu la wale walioko Mahakamani kuthibitisha kama wao waligushi au ukweli ni kwamba Lwakatare alihusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuzungumza jambo hili, Bunge lako litakuwa limeingilia shughuli zilizoko Mahakamani.

Kwa hiyo, bado ni rai yangu kwamba utumie nafasi yako kukataza mambo haya na Bunge hili

lijiheshimu, lifanye kazi yake ya msingi na lisiingilie Mamlaka nyingine na mihimili mingine. Huo kwa kweli, utakuwa ni kutokutimiza wajibu wetu kama Wabunge.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, mimi niliomba kabla ya Mheshimiwa Sendeka.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa, sikukuona, Kanuni yetu inasema anayeonwa na jicho la Spika. Nilishasema wale ni watatu wa mwisho.

Mwongozo wangu ni huu ufuatao katika jambo hili. Kwamba, kwa vile jambo hili ni la kikanuni, ninaagiza kwamba Kamati ya Kanuni ya Bunge hili, ikutane mara moja baada ya kusitisha shughuli hizi katika Ukumbi wa Spika ili iweze kujadili jambo hili na kukisaidia Kiti katika namna na mwenendo wa jambo hili. Tutakaporudi saa 11.00 jioni, tutakwenda na utaratibu ambao utakuwa umewekwa na Kamati ya Kanuni ya Bunge. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, naomba sasa nisitishe...

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Sasa nasitisha shughuli za Bunge, hadi saa 11.00, jioni hii.

*(Saa 7.00 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnachofanya ni fujo Bungeni hebu naomba mkae kwanza ninapokuwa nimemwita Katibu tumpe nafasi, Kanuni zinasema Mbunge mwenye jambo lolote anasimama mahali pake na nafikiri bado nina macho yanaweza tu kuona vizuri na sidhani kama kuna Mbunge ambaye amewahi kusimama hapa akakosa nafasi ya kupewa nafasi. Tukipeana nafasi na kusikilizana nina hakika shughuli zetu zitaenda vizuri sana bila matatizo. Nimeona Waheshimiwa Wabunge wawili Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, leo mchana wakati naomba mwongozo wako na kwa desturi yangu kuna jambo lilitokea nimefadhaika sana na jambo ambalo limetokea mchana leo. Nimeamua nije mimi mwenyewe nikuombe radhi Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa neno lililonitoka ambalo kwa kweli siyo la kiungwana baada ya kusema hayo naomba neno hili liondolewe kwenye *Hansard*.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na isomeke pamoja na Kanuni ya 64(1) (f) na (g). Asubuhi alipokuwa anaomba Mwongozo Mheshimiwa Peter Serukamba ni kweli kwamba alitumia neno la tusi kubwa sana ambaye hakuna Mbunge yeyote humu ndani ambaye amewahi kutumia neno chafu la tusi kubwa kiasi hicho alivyofanya yeye. Kwa *summary* alichofanya ni *gross misconduct* na Mhehimiwa Naibu Spika, jana kiti chako kilitoa maelekezo kwa Wabunge wote kwamba Mbunge yoyote yule atakayetumia tena lugha ya matusi humu ndani ataitiwa Polisi na kuondolewa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kiti chako kweli kinatenda haki na kinasimamia Maadili ya Wabunge humu ndani tunaomba yale maagizo ya jana Polisi waje sasa hapa. Nakushukuru na naomba Mwoongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje haya unayoongea siyo haya ambayo ameomba radhi? Tunaongea na mtu mmoja mmoja, nataka kujua kama hoja zao ni zile zile au ni nyingine maana yake kuna Mheshimiwa Mbunge hapa amesimama na kuomba radhi mbele ya Bunge hili kuhusu yaliyotokea na wewe unayoyasema ni yale yale au ni mengine?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama kuomba Mwongozo wako kutokana na agizo la Spika lililotoka jana lakini pia nimesimama kuomba Mwongozo wako nikiamini kwamba humu ndani mtu akitoa tusi kubwa siyo kwamba akiomba msamaha inaishia hapa na Spika hakusema kwamba akiomba msamaha itaishia hapa Spika alisema ataita Polisi. Kwa hiyo naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Kanuni hizo hizo zinaniruhusu kunipa mu Mwongozo muda sio mrefu sana tuendelee na shughuli zilizopo mbele yetu nitatoa Mwongozo baadaye. Waheshimiwa Wabunge tulipokutana asubuhi ya leo kwenye shughuli yetu ya mwisho ilikuwa ni kumpa nafasi Msemaji wa kambi ya Upinzani kuhusu hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi asome hotuba yake, pakatokea sintofahamu na mvutano kuhusiana na baadhi ya mambo yaliyokuwa yameandikwa kwenye ripoti ya Kambi ya Upinzani ambayo Mheshimiwa Msemaji wa kambi ya upinzani alikuwa aisome mbele yetu. Nikaomba kwamba Kamati ya Kanuni ikutane wakati wa mchana na naomba kulitaarifu Bunge kwamba Kamati ya Kanuni imekutana na wajumbe wake karibu wote kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge.

Walichokuwa wanaelekeza Kamati ya Kanuni ni kwamba ni kweli kulikuwa na matatizo kati ya ukurasa wa kwanza na ukurasa wa nne wa hotuba ile kwamba baadhi ya mambo yangeweza kuingilia uhuru wa Mahakama au kuvunja baadhi ya sheria nyingine.

Kwa hiyo, ilikubalika kwamba ukurasa wa kwanza hadi wa nne ukaandikwe upya kwa kadiri ambavyo kambi itakuwa imeona ni sawasawa kwa kuzingatia ushauri huo wa Kamati ya Kanuni.

Halafu ripoti hiyo ikishaandikwa upya basi tuendelee na shughuli kama kawaida kwa maana ya usomaji na kadhalika. Sasa sina mawasiliano yoyote lakini mawasiliano rasmi niliyonayo hapa ni kwamba sijapata nakala halisi ya hicho ambacho kitasomwa hadi sasa ninavyosimama hapa sina hakika kama Ofisi ya Spika imepata. Kwa ajili ya uendeshaji bora ya shughuli za Bunge nitaomba kwamba tuendelee na uchangiaji wakati wowote nakala hiyo itakapokuwa imepatikana, nakala hiyo nikaletewa hapa mezani, nitamwita Mheshimiwa Profesa Kulikoyeka Kahigi ili, aendelee kusoma kama kawaida. Hakuna kilichoharibika kila kitu kitaenda vizuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Tundu Lissu amesimama vizuri kwa utaratibu ule ule ambao tunakubaliana sasa huku kuzomeana kwingine kunatokana na jambo gani, nini kimeharika. Utaratibu ni kama anavyofanya *Chief Whip* unasimama kama alivyofanya nakupa nafasi unasema lakini huu utaratibu mnaotaka kuuanzisha Waheshimiwa Wabunge hebu kaa kidogo Mheshimiwa Tundu Lissu.

Utaratibu wa kuvunjiana heshima, kuonyeshana watu wote hatuna akili, zinazotosha si sawa sisi wote hapa ndani ni viongozi unasimama mahali pako unapewa nafasi unazungumza. Nimetoa ripoti ya kilichotokea kwenye Kamati ya Kanuni kama alivyofanya Mheshimiwa Tundu Lissu, amesimama ndiyo utaratibu wetu mzuri, Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naomba nipendekeze kwako kwamba Msemaji wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni aendelee na hotuba yake kama alivyokuwa ameanza kwa sababu huo ukurasa wa kwanza mpaka wa nne umefanyiwa

marekebisho kama ambavyo Kamati ya Kanuni ilivyoelekeza na nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba hayo marekebisho yaliyofanyika nimeyasimamia mimi mwenyewe. Kwa hiyo, yale yote ambayo walikuwa wanadhani hayako sawa yameondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwa taratibu zetu za Kikanuni mjadala huwa unaanza baada ya Msemaji wa Kambi rasmi ya Upinzani kuwasilisha maoni yake. Kwa hiyo, nadhani umeshaletewa kwenye kiti Msemaji wa kambi azungumze mjadala ufunguliwe, ni hayo tu.

**NAIBU SPIKA:** Hakuna ugomvi katika jambo hili sasa nimeletewa nakala kama utaratibu unavyotaka ingekuwa ni kitu cha ajabu sana kije kisemwe kitu hapa ambacho hata mimi sina nakala. Hata kama ninyi hamjapata mtaletewa kwa wakati lakini meza ni lazima iwe na nakala ya kile ambacho kinasomwa na ndiyo utaratibu wetu.

Kwa hiyo, hakuna mtu anayeonewa wala jambo gani lakini moja kwamba jamani wote mnaoandika hotuba humu ndani msiandike yale mambo ambayo ni kinyume na Kanuni na utaratibu wetu usumbufu wote huu usingetutokea. Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, kwa muda huu tulio nao sasa una nusu saa, nakuomba uendelee kusoma hotuba kama ilivyorekebishwa, tafadhali Profesa.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI- MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naomba niendelee lakini hotuba yangu kama ambavyo imewasilishwa mezani itokee hivyo hivyo kwenye *Hansard* kwa sababu nusu saa sidhani kama itatosha kusoma hotuba yote.

**NAIBU SPIKA:** Hotuba ambayo inatakiwa itoke kwenye *hansard* ni hii ya sasa ambayo nimepewa mezani na itatoka hivi hivi ilivyo ahsante sana endelea.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI- MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika nitaanza na utawala bora na nitaanza kuzungumzia Idara ya usalama wa Taifa na ujasusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, kipindi hiki itajikita katika mambo machache mahususi katika Ofisi ya Rais - katika Utawala bora, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mahusiano na Uratibu - ambayo tunayaona ni mapungufu. Lengo la kufanya hivyo ni kuitaka Serikali ama ichukue hatua ya kuyatokomeza mapungufu hayo kwa kutangaza hadharani nia yake ya kuyakomesha, kisha ichukue hatua mwafaka au ijiuzulu kwa kushindwa kuongoza dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, idara ya usalama wa taifa na ujasusi (TISS) ilianzishwa kwa mujibu wa kifungu 4(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Usalama wa taifa na ujasusi *(The Tanzania Intelligence and Security Service Act)* ya 1996 sura ya 406 ya sheria za Tanzania. Kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha sheria hiyo, Idara ya Usalama wa Taifa na Ujasusi inafanya kazi chini ya udhibiti wa waziri anayehusika na masuala ya usalama wa taifa.

Kifungu cha 5(1) a,b,c na d vinailazimu idara hiyo kumtaarifu waziri juu ya shughuli zake za kijasusi; inamshauri waziri juu ya masuala yanayohusu usalama na inampa waziri mamlaka ya kuielekeza idara kumjulisha Rais au mtu mwingine yoyote juu ya masuala ya ujasusi na usalama. Kifungu cha 5(2) kinaikataza idara ya usalama wa taifa na

ujasusi kufanya ujasusi kwa mtu yeyote au kikundi cha watu kwa sababu tu kwamba mtu huyo au kikundi hicho kinajishughulisha na upinzani linalohusu Katiba, sheria au Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, idara ya usalama wa taifa na ujasusi imekuwa ikijihusisha sio tu na vitendo vya kijasusi dhidi ya watu, makundi au taasisi zinazopinga Serikali au sera zake na au taratibu zake bali pia imeshiriki katika vitendo vya kuwateka na kuwatesa watu hao. Kama ambavyo imeripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari vya hapa nchini, maafisa wa idara ya usalama wa taifa wamehusishwa na vitendo vya utekaji nyara vya watu ambao wameendesha jitihada za migomo dhidi ya taasisi za serikali au waandishi wa habari ambao magazeti yao yameikosoa serikali au sera zake.

Pamoja na idara ya usalama wa taifa kutajwa kwa majina kuhusika na vitendo hivyo vya kihalifu, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na jeshi la polisi kuwakamata maafisa hao na kuwafikisha mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya jeshi la polisi kutochukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya maafisa wa usalama wa taifa wanaohusika umepelekea vitendo hivyo kuongezeka na hivyo kutishia uhuru, haki na maisha ya wale wote wanaoipinga au kuikosoa Serikali kwa njia zilizokubalika kikatiba.

Aidha, badala ya jeshi la polisi kuchukua hatua ya kuwadhibiti wanaohusika na uhalifu huo, Serikali imechukua hatua ya kuvifungia vyombo vya habari kama gazeti la mwanahalisi vilivyofanya uchunguzi na kuihusisha idara ya usalama wa taifa na vitendo vya utekaji nyara na utesaji. Badala ya kuwakamata wahalifu, serikali hii ya CCM imeamua kuwaadhibu wale waliopiga kelele kuashiria kwamba kuna uhalifu umefanyika.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inaamini kwamba kama jeshi la polisi lingechukua hatua za dhati kuwakamata maafisa wa Usalama wa taifa waliotajwa na vyombo vya habari kuhusika na utekaji na utesaji wapinzani wa serikali au wanaokosoa sera na utendaji wake basi kutekwa na kuteswa kwa Mhariri Mtendaji wa magezeti yanayomilikiwa na kampuni ya *New Habari Corporation Ltd.* na mwenyekiti wa jukwaa la wahariri Ndugu Abasalom Kibanda, kungeweza kuepukwa.

Hii ni kwa sababu mazingira ya kutekwa na kuteswa kwa bwana Kibanda na aina ya mateso aliyofanyiwa kama vile kung'olewa kucha, meno na kutobolewa jicho kunafanana na utekaji nyara uliohusishwa na maafisa wa Usalama wa Taifa na ujasusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekaji nyara na utesaji wa watu kwa aina ambayo tumeizungumzia siyo tu ni makosa ya jinai kwa mujibu wa sheria yetu ya kawaida ya jinai *(penal code sura ya 16)* vilevile ni makosa ya kigaidi kwa mujibu wa sheria ya kuzuia ugaidi ya mwaka 2002 sura ya 430 ya sheria zetu. Kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) (d) cha sheria ya idara ya uslama wa taifa na ujasusi, idara hiyo ina jukumu la kumtaarifu Rais au mtu mwingine yoyote au mamlaka juu ya masuala ya ugaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kutoka kwa Waziri husika wa usalama wa taifa, Kama idara hiyo au maafisa wake wanatuhumiwa au kuhusishwa na vitendo vya ugaidi kama vilivyotafsiriwa na kifungu cha 3 cha sheria hiyo, ni nani sasa atakayemtaarifu Rais juu ya masuala hayo ya ugaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, idara ya usalama wa taifa haihusishwi tu na vitendo vya kihalifu na kigaidi tulivyovielezea hapo juu bali pia inahusishwa na vitendo vya kijasusi dhidi ya vyama halali vya kisiasa hasa hasa CHADEMA. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina nyaraka zinazoonesha kwamba idara ua usalama wa taifa na baadhi ya maafisa wa ofisi binafsi ya Rais wameshiriki katika kutengeneza ushahidi wa kuichafua CHADEMA kwa kuihusisha na njama za ilichokiita kudhuru wana habari.

Nyaraka zenyewe ni barua ya tarehe 13 Machi, 2013 kutoka kwa mtumishi wa Rais Muhidini Issa Michuzi kwenda kwa maafisa wengine wa ofisi binafsi ya Rais akiwemo mkurugenzi wa mawasiliano wa Ikulu Salvator Rweyemamu na Katibu wa Ofisi binafsi ya Rais Prosper Mbene yenye maneno yafuatayo: Ndugu wana OBR jioneeni njama za CHADEMA kudhuru wana habari.

*"Huyu na wengine wote si wa kuwaachia. Kudos to TISS kwa kufanya kazi ya ziada kupata hii kitu hii ni kete kubwa kwetu, lazima tupige kelele kwa nguvu zote."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushahidi mwingine unaowahusisha maafisa wa idara ya usalama wa taifa na vitendo vya kuwarubuni na kuwahonga maafisa na watumishi wa CHADEMA ili washiriki katika njama za kukichafua chama.Njama hizo zinamhusisha afisa mwandamizi wa usalama wa taifa ambaye anatuhumiwa kumhonga afisa usalama wa CHADEMA.

Aidha Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ina nyaraka zinazoonesha kuwako kwa mawasiliano ya karibu kati ya maafisa wa usalama wa taifa waliohusishwa na vyombo vya habari kwa vitendo vya utekaji na utesaji na viongozi waandamizi wa CCM na serikali yake kama vile Naibu Katibu Mkuu wake Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi. Mawasiliano hayo pia yanamhusisha Saum Malugu ambaye aliwahi kuwa karani katika Makao Makuu ya CHADEMA ambaye amekuwa akitumiwa kusambaza hongo kwa maafisa na watumishi wa CHADEMA-Makao Makuu. Kwa kadri tunavyofahamu, si Mwigulu Nchemba au Mhe. Dkt. Nchimbi ambao ni miongoni mwa watu wanaotakiwa kupewa taarifa na watu wa usalama wa taifa.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kutoka kwa waziri wa Usalama wa Taifa, kama amewahi kutoa maagizo ya maandishi kwa idara hiyo kufanya ujasusi dhidi ya CHADEMA au viongozi, watendaji maafisa na watumishi wake.

Vilevile, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama Waziri anayehusika na Usalama wa Taifa amewahi kutoa maelekezo kwa idara hiyo kuwa na mawasiliano na viongozi waandamizi wa CCM au na watumishi wa zamani au wa sasa wa CHADEMA kwa malengo ya kukusanya taarifa za kijasusi dhidi ya CHADEMA.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka waziri kueleza kama amewahi kushauriana na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa juu ya jambo lolote linaloihusu CHADEMA au harakati zake za kisisa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, nakuomba tumpe nafasi, amalize nusu saa yake kusoma. Mheshimiwa Profesa endelea!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI- MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya maswali haya ni muhimu kwa mustakabali wa taifa letu na kwa ulinzi wa haki na uhuru wa kikatiba wa kupinga serikali au sera zake uliowekwa kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu. Endapo idara ya usalama wa taifa na ujasusi, itaachwa iendelee na vitendo vya kihalifu na kigaidi inavyotuhumiwa navyo au iendelee kufanya vitendo vya kijasusi dhidi ya vyama vya siasa, taasisi za kiraia au wananchi wa kawaida basi Tanzania itajikuta imegeuzwa dola la kiusalama wa Taifa (*National Security State*) na haki zote za kisisasa na kijamii zikiwemo za kupinga serikali iliyoko madarakani kwa njia ya amani zitaangamizwa.

Nchi yetu itageuzwa sawa na madola ya kipolisi (*Police States*) ambapo matendo ya Serikali au ya watendaji wake hayahojiwi na wananchi au na vyombo vya habari au na vyama vya siasa kwa hofu ya kukamatwa na kuteswa na

usalama wa taifa. Tukifika hapo nchi yetu haitakuwa tofauti na na Misri ya Hosni Mubarak, au Tunisia ya Zine Abidine ben Ali au Afrika ya Kusini ya Zama za Makaburu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa na Mwelekeo wa Matukio ya Rushwa Nchini Rushwa inavyodidimiza uchumi na Maendeleo ya Taifa. rushwa na ufisadi bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu na kikwazo kikubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Bado hatujafanikiwa kupunguza tatizo hili kubwa linalodidimiza uchumi wa nchi yetu na linalochangia katika kujenga matabaka ya matajiri haramu na masikini waliosababishiwa umasikini na mfumo wa kifisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali ina kigugumizi kuhusu rushwa na ufisadi, baadhi ya taarifa zihusuzo mambo hayo hufichwa. Kwa mfano, Serikali imekaa kimya kuhusu baadhi ya mikataba na ripoti mbalimbali – jambo linalotafsiriwa kwamba ni mchakato wa kuwalinda watu waliohusika na vitendo vya rushwa au ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti kwa mfano za EPA, MEREMETA, Uchunguzi na ukaguzi wa kituo cha mabasi Ubungo, ripoti ya ufisadi katika UDA, ripoti ya sakata la aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini David Jairo zote ni baadhi tu ya ripoti ambazo bado ni siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya (*The National Governance and Corruption Survey)* ya mwaka 2009, Ubinafsi na tamaa hasa ya viongozi wa Serikali inaongoza kwa asilimia 95.5 kama kisababishi cha rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina ya rushwa anayonufaika nayo afisa wa Serikali kwa kupewa mgao wa kifisadi baada ya kutoa kandarasi kinyume na utaratibu au upendeleo kwa kampuni fulani. Hivyo, fedha hizo za mgao zinaelekezwa kwa taasisi ambayo ana uhusiano nayo au kujengewa nyumba ili mradi fedha hizo za kifisadi zisipitie kwenye akaunti yake binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea maafa ya kuanguka kwa majengo ya ghorofa na kuangamiza maisha ya watu hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba maafa haya yalitokea kwa sababu ya mfumo wa kifisadi na rushwa katika utendaji wa Serikali. Hii ni kwa sababu Serikali ilishashauriwa na na Tume ya Uchunguzi iliyoundwa na aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa kuwa maghorofa zaidi ya 100 Dar es Salaam yamejengwa chini ya kiwango, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa, pamoja na Tume hiyo kutumia mamilioni ya fedha za walipakodi kufanya uchunguzi na kuandika taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashawishika kuamini kwamba ukimya wa TAKUKURU kwenye maafa haya ya maghorofa kuporomoka ni kutokana na taasisi hiyo kuwa sehemu ya mfumo wa kifisadi unaoitafuna nchi hii. Ukiukwaji wa makusudi wa kikomo cha maghorofa (maghorofa 10) ulikuwa ni ishara tosha kuwa mradi huu uligubikwa na ufisadi – na TAKUKURU ilipaswa kufanya kazi yake ili kubaini kwa nini maghorofa yalizidishwa, na pia kwa nini hadi wakati huo taarifa za Tume ilikuwa haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu moja muhimu iliyotajwa katika Taarifa ya Tume hiyo ni kukosekana kwa usimamizi na uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa serikali (86%), uwezo mdogo wa kusimamia sheria na kuhakikisha zinatekelezwa na upungufu katika utoaji wa adhabu kali kwa wanaojihusisha na vitendo vya rushwa (85.6%).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, kwanza kabisa ni lazima tujenge taasisi imara na huru na zenye kufanya kazi zake kwa weledi na umakini mkubwa. Lazima taasisi hizi si tu ziwe huru; bali pia zionekane kuwa huru. Muundo wa TAKUKURU ni vyema ukaangaliwa upya katika mchakato unaoendelea hivi sasa juu ya kuandika Katiba mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi wa TAKUKURU ambaye ni mteule wa Rais, ni vigumu sana kuwa huru na kuvichunguza vyombo vingine ambavyo vipo chini ya mamlaka ya Rais. Kwa maneno mengine, ni vigumu kumchunguza aliyekuteua na kuchukua hatua kali dhidi yake. Katika mfumo uliopo, Rais huyo huyo ndiye Mwenyekiti wa chama tawala; hivyo inakuwa ni vigumu sana kwa chombo hiki kuchukua hatua kali hata dhidi ya chama; kwani kufanya hivyo kutakuwa pia kumuadhiri mkuu wake wa kazi aliyemteua ambaye kwa kofia yake nyingine ni Mwenyekiti wa chama.

Lakini ni mara ngapi katika chaguzi za Chama cha Mapinduzi tumesikia Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM akilalamikia chaguzi hizo kuwa ziligubikwa na rushwa, lakini hatujawahi kusikia kuwa wahusika wa matukio hayo wamekamatwa na TAKUKURU japokuwa ushahidi unakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Umasikini ya mwaka 2011 iliyotolewa Mei, 2012, umma haujaridhika na juhudi zinazofanywa na Serikali katika utendaji mzima wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa kutokana na sababu kuu kuwa watu wengi waliokuwa wanahusika na rushwa kubwa wameachiwa huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maazimio ya Kongamano la Wadau wa Rushwa. Mnamo tarehe 3 Mei, 2010 kulikuwa na Mkutano wa kutathmini maazimio ya Kongamano la Rushwa la mwaka 2009 ambalo lilihusisha wadau mbalimbali wa kupambana na rushwa nchini wakiwemo kutoka Ofisi ya Bunge na mgeni Rasmi katika kongamano hilo alikuwa Mheshimiwa Samwel Sitta ambaye alikuwa Spika wa wakati huo. Katika kongamano hilo, maazimio zaidi ya 30 ya jinsi ya kukabiliana na kupambana na rushwa katika taifa letu yalipitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa maazimio hayo ni pamoja na azimio namba (4) ambalo lilikuwa ni kuitaka TAKUKURU kuanzisha gazeti maalum litakalosambazwa mpaka vijijini lenye kuelimisha umma kuhusiana na masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kulieleza Bunge juu ya hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kuanzishwa kwa gazeti hilo. Aidha, azimio namba 11 lilihusu viongozi kutangaza mali zao pindi wanapokuwa wanaondoka madarakani; utekelezaji wake umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azimio namba 15 la Kongamano la Rushwa, TAKUKURU ilitakiwa kuhakikisha kuwa inawekeza zaidi katika fani ya habari za kiuchunguzi (*investigative journalism*) Kwa ajili ya kuwajengea uwezo zaidi wanahabari katika kufichua na kuandika taarifa za rushwa hapa nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua utekelezaji wa azimio hili umefikia wapi na hasa ikizingatiwa kuwa gazeti la Mwanahalisi lililokuwa linaandika habari za kiuchunguzi kuhusiana na rushwa sasa limefungiwa kwa muda usiojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio la 27 la kongamano hilo liliitaka serikali iache mara moja utaratibu wa kuwahamisha watumishi wa umma ambao ama ni wabadhirifu/walarushwa kama sehemu ya adhabu kutokana na kitendo cha wizi na/au ubadhirifu wa mali ya umma kwenye ofisi za umma na badala yake washughulikiwe kwa mujibu wa sheria za rushwa na za jinai zilizopo katika mfumo wetu wa sheria hapa nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ni hatua gani serikali imefikia katika kutekeleza azimio hili kama kweli tuna nia ya dhati ya kupambana na wabadhirifu wa fedha za umma na walarushwa kwenye Ofisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti Ya Utumishi Wa Umma, Utaratibu wa Ajira kwa Mkataba kwa Watumishi waliostaafu, kwa mujibu wa sheria za Tanzania, watumishi wa umma hutakiwa kustaafu kwa hiari wakiwa na umri wa miaka 55, na watimizapo miaka 60 hutakiwa kustaafu kwa lazima. Hata hivyo, baadhi yao wamekuwa wakipewa mikataba ya kuendelea na kazi hata baada ya kutimiza umri wa kustaafu kwa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi kumwajiri mstaafu kwa mkataba kama mstaafu huyo ndiye pekee mwenye ujuzi na uzoefu wa kazi anayotakiwa kufanya. Ila kuna baadhi ya watumishi waliotimiza umri wa kustaafu kwa lazima, wakapewa mikataba ya kuendelea na utumishi Serikalini, bila kuwa na sifa iliyotajwa. Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea kwamba, Serikali ingeajiri watumishi wengine kushika nafasi hizo baada ya mikataba hiyo kumaliza muda wake hasa ukizingatia tatizo kubwa la ajira linalowakumba vijana katika nchi yetu.

Serikali ya CCM imeendelea kuwaacha wastaafu hao kuendelea na utumishi bila hata kutoa mikataba mipya baada ya ile ya mwanzo kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba iwataje baadhi ya wazee waliotimiza umri wa kustaafu kwa lazima, wakapewa mikataba ya utumishi Serikalini, mikataba hiyo ikamaliza muda wake, lakini bado wanaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu John Tendwa, Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania Mkataba wa Ajira wa Msajili wa vyama vya Siasa John Tendwa ulimaliza muda wake tangu Novemba, 2012 lakini bado anaendelea na kazi bila ya mkataba mwingine.

Aidha, alipohojiwa na waandishi wa habari juu ya jambo hili alikiri kuwa ni kweli mkataba umeisha lakini sababu za yeye kung'ang'ania ofisi alisema iulizwe mamlaka ya uteuzi wake, yaani Rais. Hata hivyo, Ndugu Tendwa aliwakataza waandishi wa habari kutoa taarifa hii katika vyombo vya habari kwa alichodai kuwa ingeleta mgogoro na malumbano makubwa yasiyo na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haiamini hata kidogo kwamba John Tendwa ndiye mtu pekee mwenye sifa za pekee za kuwa Msajili wa vyama vya Siasa miongoni mwa Watanzania.

Hatupendi kusema kuwa ufanisi wake umepungua wala hatupendi pia kusema kwamba kuendelea kwake kubaki ofisini bila hata ya mkataba ni kutokana na kujipendekeza kwake kwa Rais na uhodari wake wa kukipendelea chama tawala na Serikali yake lakini tunapenda kusema kuwa wapo watu wengine wenye sifa ya kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Ni jambo jema kuwapa wengine uzoefu, na ni jambo jema pia kuzingatia sheria na kanuni zinazoelekeza masuala ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi, Manispaa ya Moshi, Bernadeta Kinabo. Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Moshi, Bernadeta Kinabo, naye alishastaafu kazi, akapewa mkataba kuendelea na kazi na mkataba huo uliisha muda wake tangu mwaka 2011, lakini bado yupo ofisini anaendelea na kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe majibu, ni kwa nini Halmashauri na Manispaa ziendeshwe na watumishi wa mkataba wakati kuna watumishi waandamizi katika Halmashauri na Manispaa hizo ambao wangeweza kufanya kazi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi na Haki za Walimu katika Sekta ya Utumishi wa Umma, kwa muda mrefu sasa walimu wamekuwa ni kada ya utumishi wa umma ambayo haitendewi haki na Serikali. Nasema hivi kwa sababu kwa miaka mingi walimu wamekuwa wakilalamika kuhusu

mishahara duni, lakini pia baadhi yao (wengi kiasi) wamekuwa hawalipwi stahili zao kwa mfano malimbikizo ya mishahara, fedha za uhamisho, na kadhalika. Mara zote walimu kupitia chama chao wanapolalamika kupata maslahi yao Serikali imekuwa ikiwajibu kwa jeuri kuwa madai yao hayalipiki na pia wanapotangaza mgomo halali kama njia ya kuifanya Serikali iwasikilize, Serikali imekuwa na tabia ya kukimbilia mahakamani kuweka zuio la mgomo huo na hivyo kuwaacha walimu njia-panda bila kujua la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti ya Elimu mwaka 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa angalizo kwamba Serikali isiwaburuze walimu wasije wakabaki na kinyongo na kufanya mgomo baridi ambao matokeo yake huwa ni mabaya kuliko mgomo halisi. Serikali hii ya CCM, kama kawaida yake, iliendelea kuziba masikio, na matokeo yake tunaona jinsi ambayo elimu ya nchi hii inavyozidi kuporomoka.

Kwa mara ya Kwanza katika historia ya Tanzania, wanafunzi zaidi ya asiliami 60 waliofanya mtihani wa kidato cha nne kidato cha nne 2012 walipata daraja sifuri. Bila shaka mojawapo ya sababu kubwa za anguko hili ni Serikali kupuuza madai ya walimu kama Kambi Rasmi ya Upinzani ilivyodokeza mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hukumu ya mahakama juu ya mgomo wa walimu mwaka jana 2012, ni kwamba Serikali ilitakiwa kukaa na chama cha walimu (CWT) na awepo msuluhishi kati yao (*third party*) katika kutafuta ufumbuzi wa madai ya walimu dhidi ya Serikali. Kwa kuwa mpaka leo hapajakuwepo na kikao cha usuluhishi kati ya Serikali na Chama cha Walimu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge sasa kama chombo cha uwakilishi lakini pia kama muhimili wa dola unaojitegemea kuwa msuluhihishi kati ya Serikali na Chama cha Walimu ili haki itendeke kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utaratibu wa Kupima Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma. Mwaka 2004 Serikali

ilitoa waraka wa utumishi namba 2 wa mwaka 2004 kuhusu utekelezaji wa utaratibu na kupima utendaji kazi wa watumishi kwa uwazi. Lengo na madhumuni ya waraka huu ni kupima na kuongeza ufanisi kwa watumishi wa umma ili kuleta tija, na hivyo kustawisha maendeleo ya nchi yetu. Zaidi ya hayo, waraka huu unaondoa utaratibu wa zamani wa kupima utendaji kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iliambie Bunge hili na wananchi wa Tanzania kwamba ni mafanikio kiasi gani yamepatikana tangu kuanza kwa utekelezaji wa waraka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahusiano Na Uratibu. Mchakato wa Katiba Mpya na Mapungufu yake**,** kwa mujibu wa Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, aliyoitoa kwenye mkutano huu wa bunge tarehe 11 Aprili, 2013 ni kwamba kulikuwa na makubaliano kati ya kamati maalum ya CHADEMA na Rais juu ya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011. Kwa mujibu wa makubaliano hayo, marekebisho yalitakiwa kufanywa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ilifanyika katika Bunge la Februari, 2012.

Aidha, kwa mujibu wa makubaliano hayo, awamu nyingine mbili za marekebisho ya sheria hiyo ya mabadiliko ya Katiba yalitarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka jana, yaani 2012. Mwaka 2012 ulimalizika kabla ya makubaliano hayo kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake ya kuukaribisha mwaka 2013, Rais Kikwete, alipokuwa akilihutubia taifa kama ulivyo utaratibu wake wa kila mwisho wa mwezi alisema hivi, nanukuu:

*"Katika hotuba yangu ya mwisho wa mwezi wa Februari, 2012, nilieleza kwamba katika mazungumzo baina ya Serikali na vyama vya siasa na wadau wengine juu ya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba tulikubaliana tushughulikie marekebisho ya Sheria hiyo hatua kwa hatua. Tulikubaliana kuanza na mambo yanayohusu Tume ya*

*Kuratibu na Kukusanya Maoni ya Wananchi ili Tume iundwe na ianze kazi. Baada ya hapo tuangalie vipengele vinavyohusu Bunge Maalum na Kura ya Maoni.*

*Tulifanya hivyo kuhusu Tume ya Katiba na sasa tunajiandaa kuanza mazungumzo kuhusu ngwe iliyobaki yaani, Bunge Maalum na Kura ya Maoni. Kama mazungumzo yatakamilika mapema kunako Januari, 2013 mapendekezo hayo yatafikishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kikao cha Februari kwa uamuzi. Vinginevyo itakuwa katika Bunge la Aprili, 2013.*

*Ndugu Wananchi Kuhusu Kura ya Maoni, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inaelekeza kuwa Kura ya Maoni itatungiwa Sheria yake maalum. Ni matumaini yangu kuwa matayarisho yake yataanza mapema iwezekanavyo. Nawasihi wananchi wenzangu, viongozi wa vyama vya siasa na asasi za kijamii tuwe watulivu, tuendelee kushirikiana katika mchakato huu wa Katiba mpaka tulifikishe jahazi ufukweni salama kwa mustakabali mwema wa nchi yetu na watu wake".*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Rais kwamba Serikali ingeleta awamu zote mbili za marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kabla ya mwisho wa mwaka 2012 haikutimizwa. Aidha ahadi nyingine aliyotoa Rais wakati akitoa hotuba ya kuukaribisha mwaka 2013 kwamba marekebisho hayo yangefanyika katika mwezi Februari 2013 au Aprili 2013 bado haijatekelezwa na hatuoni dalili ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuweka kumbukumbu vizuri kwamba, madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya katiba siyo ya kuokoteza. Ni makubaliano halali kati ya wadau mbalimbali kama vile vyama vya siasa, asasi/mashirika na kadhalika na Rais. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Rais asimamie ahadi zake na taifa lina haki ya kujua nini kilitokea mpaka ahadi hizi kushindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tarehe 16 Aprili, 2013, Waziri Mkuu, wakati akihitimisha hotuba yake alitoa ahadi kuwa, "*huenda serikali ikawasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo kwenye Bunge hili la Aprili kama muda ukipatikana kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza".* Kwa maelezo hayo, ni wazi kuwa Waziri Mkuu hana hakika na kutekelezeka kwa ahadi ya Rais katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa kutambua kwamba mambo haya yako chini ya Ofisi ya Rais, tunaitaka serikali itamke mbele ya bunge hili ni lini marekebisho hayo yatafanyika.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inayoongozwa na CHADEMA inarudia tena, kwamba haitakuwa tayari kuendelea na mchakato wa Katiba mpya endapo marekebisho ya sheria hiyo hayatafanyika pamoja na utekelezaji wa mambo ambayo tuliyoyasema wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mipango na Majukumu yake. Jukumu kubwa la Tume ya Mipango, pamoja na mambo mengine, ni kuratibu utekelezwaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro na utendaji kazi wa tume hii, ila inashangazwa na uundaji wa chombo kingine chini ya Ofisi ya Rais ambacho kimsingi kazi zake zingepaswa kufanywa na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu, katika hotuba yake ya bajeti alisema kwamba: **"***Serikali imeona ni muhimu kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kuanzisha mfumo imara zaidi wa kupanga vipaumbele, kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo. Mfumo huo ambao utasimamiwa na Chombo maalum (President's Delivery Bureau) chini ya ofisi ya Rais, Ikulu, unazingatia uzoefu wa nchi ya Malaysia*."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inatambua kwamba Serikali imeuchukua mpango huu kutoka Malaysia, kutokana na mkutano wa kimataifa wa '*Langkwi'* uliofanyika mwezi Juni 2011 ambao Rais Dkt. Jakaya Kikwete alishiriki kwenye '*mkutano wa tafakuri Putrajaya'* ambapo Waziri Mkuu wa Malaysia Mheshimiwa *Dato' Razak* aliuelezea mpango huu kuwa ulileta mabadiliko ya kiuchumi katika nchi yake. Katika mkutano huo wa tafakuri, Waziri Mkuu wa Malysia alisema kwamba mafanikio ya mpango huo ulitokana na misingi ifuatayo:-

(i) Uongozi shupavu na ulio tayari kwa mabadiliko ya kuipeleka nchi mbele.

(ii) Kuweka mipango ya kimaendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa.

(iii) Nidhamu katika utendaji na utekelezaji.

(iv) Uwajibikaji wa serikali na kuwa tayari kukiri madhaifu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu wa kuanzishwa kwa idara hii ambayo inajitegemea kwenye Ofisi ya Rais tayari umeshaanzishwa kama alivyokiri Waziri Mkuu, katika hotuba yake na kwamba Rais tayari ameshazindua awamu ya kwanza ya maabara tangu tarehe 22.2.2013, na vipaumbele ambavyo vimepitishwa ni sita kama ifuatavyo:-

Nishati, Uchukuzi, Kilimo, Elimu, Maji na Ukusanyaji wa Mapato.

Aidha, kwa mwaka huu wa fedha mpango huo umeweka bayana kuwa kwa upande wa Nishati lengo ni kuongeza uzalishaji wa nishati kutoka Megawati 1,438 hadi kufikia Megawati 2,780. Katika usafirishaji kipaumbele ni kufungua korido ya kati kwa kufikia uwezo wa kusafirisha tani milioni 5 ifikapo 2015 na hatimaye tani milioni 8 ifikapo mwaka 2025.

Kwa upande wa elimu kipaumbele ni kuboresha elimu ya msingi na sekondari na kuhakikisha kuwa kiwango cha ufaulu kinafikia asilimia 70. Kwenye kilimo mkakati kipaumbele ni kufungua mashamba ya kibiashara wakati upande wa maji ni kuhakikisha kuwa asilimia 67 ya Watanzania wanapata maji safi na salama. Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, lengo ni kuhakikisha kuwa tunaongeza mapato kwa kiwango cha asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshatenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu wa 2013/2014 kiasi cha shilingi bilioni 8 na imeomba fedha kutoka kwa wafadhili wa nje kiasi cha shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kitengo hiki kipya chini ya Ofisi ya Rais Ikulu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kutoa majibu kwa Watanzania juu ya mambo yafuatayo:-

(i) Je, vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano uliopitishwa na Bunge hili mwaka 2011 ndio vimeachwa au vitatekelezwa sambamba na vipaumbele hivi vipya?

(ii) Je, Kwa nini Serikali imeanzisha kitengo kipya cha *Performance Management and Delivery Unit* (PEMANDU) (Kitengo cha Usimamizi na Ufanisi wa Utendaji) chini ya Ofisi ya Rais wakati kuna Tume ya Mipango ambayo kimsingi ndiyo yenye wajibu wa kusimamia vipaumbele vya Taifa na Mpango mzima wa Maendeleo wa Taifa?

(iii) Je, ikitokea tena, Rais akakaribishwa kwenye "mkutano mwingine wa tafakuri" kama uliofanywa na kiongozi wa Malaysia, na kukuta mipango mizuri zaidi, Serikali italazimika tena kupanga upya vipaumbele vya Taifa na Mpango wa utekelezaji kama inavyofanya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA, ni mdau mkubwa wa maendeleo na inauheshimu mpango wa Taifa wa Maendeleo lakini namna Serikali inavyotekeleza Mpango huo hatuna hakika kama malengo ya Mpango huu yatafikiwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu yoyote ya msingi ya kuanzisha kitengo kipya cha usimamizi wa mpango wa maendeleo wakati Tume ya Mipango ipo.

Kinachoonekana dhahiri ni kwamba Serikali hii ya CCM kila kukicha inatafuta mbinu mbalimbali za kutumia fedha za walipa kodi wa Tanzania bila kujali sana matatizo ya Watanzania. Nasema hivi kwa sababu kitengo hiki kipya kilichoanzishwa bila sababu ya msingi, hivi punde kitaanza nacho kuomba mabilioni ya fedha kwa ajili ya uendeshaji wake wakati tayari kuna Tume ya Mipango ambayo ndio mratibu na msimamizi wa Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahusiano ya Madhehebu ya Dini na Serikali. Kiongozi wa Kambi Rasmi Bungeni alieleza vizuri tatizo la udini katika hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 11 Aprili, 2013. Hapa itatosha tu kusema kuwa katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo matukio ambayo yanaashiria udini. Baadhi ya matukio hayo ni:-

- Kushambuliwa kwa viongozi wa dini, na wengine kuuawa;
- Kuchomwa moto nyumba za ibada; na
- Mgogoro wa nani achinje.

Yapo matukio mengine na haya yote yamesababisha taharuki, vilio, na utovu wa amani na usalama miongoni mwa wananchi walioguswa na matukio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati watu wakizidi kuathirika na matukio yanayoashiria udini, serikali haijachukua hatua kali kukomesha matukio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kushindwa kukemea au kusuluhisha kwa haraka migogoro wa kiimani uliotokea hapa nchini, umesababisha kutolewa kwa matamko makali na madhehebu ya dini ambayo kimsingi yanaonesha jinsi mahusiano kati ya Serikali na taasisi za dini yanavyozidi kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa kati ya migogoro yote ya kijamii hakuna mgogoro mkubwa na tete kama ule wa kiimani, kwani mgogoro huo hauna itikadi za kisiasa na kwa maana hiyo athari zitakazotokana na mgogoro wa kidini unaathiri jamii nzima. Ni jukumu la Serikali kuwaeleza Watanzania ni hatua gani za maksudi zinachukuliwa katika kutatua mgogoro huo unaoelekea kusambaratisha amani na mshikamano wa Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali yetu na vyombo vyake vya usalama, sheria na amani kuchukua hatua mara moja bila kuchelewa dhidi ya watu au vikundi vyovyote vinapoanza uchochezi wa kidini. Tabia ya kuachia uchochezi wa kidini kuendelea pasipo hatua madhubuti kuchukuliwa ni udhaifu mkubwa wa uongozi na uwajibikaji wa Serikali ambayo jukumu lake la kwanza ni kulinda usalama wa nchi na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala Mengine, Utawala Bora Ngazi za Halimashauri, Kata na Vijiji kwa muda mrefu sasa dhana ya utawala bora imekuwa ikionekana kuwa inapaswa kutekelezwa kwenye ngazi ya serikali kuu. Katika ngazi ya serikali za mitaa utawala bora kwa jumla umeachwa bila kuwekewa msisistizo.

Ni muhimu serikali ihakikishe kuwa utawala bora unakuwa ni sehemu ya utendaji wa kila siku kwenye ngazi zote – kitongoji, kijiji, kata, wilaya na mkoa. Ni muhimu Serikali ihakikishe kuwa waliopewa wajibu wa kusimamia hilo wanatimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya utawala bora imezorota sana kwenye ngazi ya serikali za mitaa, na hasa ikizingatiwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa mbalimbali nchini wamekuwa na utamaduni wa kuingilia maamuzi mbalimbali yanayofanywa na vikao halali vya Halimashauri za Manispaa na Wilaya. Sasa hivi Wakuu wa Wilaya na Mikoa wamekuwa wakiingilia na hata kushurutisha maamuzi mbalimbali na hivyo kukwamisha utekelezaji wa maamuzi yanayofanywa na vikao hivyo na kuathiri utendaji kazi wa Halimashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya kutokuheshimu utawala bora kwenye ngazi ya Halimashauri umekua na kusambaa mpaka kwenye ngazi za Kata na Vijiji kwani sasa watendaji wa vijiji na Kata wamejigeuza na kuwa wao ni Polisi, Mahakama na Magereza. Viongozi hawa wamekuwa wakiwanyanyasa sana wananchi kwa kuwakamata, kuwahukumu na hata kuanzisha magereza kama ambavyo wengi wanavyoweza kushuhudia kuwa yapo baadhi ya maghala ya mazao ambayo sasa yamekuwa ndio mahabusu kwa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina kuhusiana na suala la utawala bora kwenye ngazi za Halimashauri, kata na vijiji. Ni hatua gani Serikali imewachukulia viongozi wa Halmashauri, Kata na Vijiji wanaowanyanyasa wananchi kutokana na itikadi zao za siasa na sababu nyingine?

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza: Wananchi wachukue hatua gani ili kuukomesha uonevu wa aina hiyo pindi unapotokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukosefu wa Ajira na Ongezeko la Umasikini kwa Wananchi kwa mujibu wa jarida la "*The African Executive*" toleo Na. 415 la tarehe 3 -10 Aprili, 2013, ni kwamba: Tatizo kubwa kabisa la binadamu kwa siku hizi ni umasikini. Ili kuondokana na umasikini huo, hitaji la msingi kabisa ni kupata kipato kizuri ambacho chanzo chake kikubwa ni ajira. Kwa hiyo, njia madhubuti ya kupambana

na kutokomeza umasikini ni kutengeneza nafasi nyingi za ajira iwezekanavyo na kuwapatia watu ujuzi na utaalamu ili kujaza nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jarida hilo linaelezea pia kwamba, kutengeneza nafasi za ajira bila kuwajengea wananchi ujuzi na utaalamu wa kufanya kazi hizo ni kazi bure kwa kuwa kazi hizo zitafanywa na wataalam kutoka nje na hivyo kutowanufaisha wananchi wetu. Kwa hiyo kama Serikali inawapa watu wake elimu bora na kuwajengea watu wake ujuzi na utaalamu na kama Serikali inaweka mazingira mazuri ambayo watu wanaweza kufanya biashara na kupata fedha, basi watu hao watajinufaisha wenyewe, watawanufaisha wengine na wanaweza kuisaidia Serikali kuondokana na umasikini. Hivyo uwezo wa watu kupata ajira na kipato unategemea sana jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa ajira hapa nchini linazidi kuwa kubwa na Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kutatua tatizo hili. Tangu mwaka 2005 Rais kikwete aliwaahidi Watanzania Maisha Bora kupitia kaulimbiu yake ya “Maisha Bora kwa Kila Mtanzania”. Hiki ni kipindi cha pili cha utawala wake na maisha ya Mtanzania yanazidi kusinyaa, umasikini unazidi kuongezeka, na tatizo la ajira linazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja Serikali hii ya CCM kushindwa kutoa ajira za kutosha tofauti na ilivyoahidi bado imekuwa ikiwakejeli wananchi kuwa eti hata kufungua visoda ni kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kufukuzwa Kazi kwa Kuonewa. Baadhi ya waajiri wa serikali wamekuwa wakinyanyasa na kuwanyanyapaa watumishi wa umma kutokana na itikadi za kisiasa. Unyanyapaa huu umechukua sura mpya kiasi ambacho mtumishi anapotoa mawazo mazuri ambayo ni ya kukosoa mfumo wa uendeshaji wa taasisi ya umma ili ufanye kazi vizuri zaidi anaitwa kuwa ni pandikizi la CHADEMA.

Jambo hili linawavunja moyo watumishi wa umma kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuogopa kuitwa ni wapinzani na matokeo yake utendaji katika sekta ya umma unazidi kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kusikitisha, Ndugu Emmanuel V. Gwalanje, ambaye ni Afisa Mifugo Msaidizi Daraja la II katika Halmashauri ya Mufindi, alifukuzwa kazi kwa mashtaka dhidi yake kwamba anajihusisha na masuala ya siasa wakati wa kazi. Katika utetezi wake, Ndugu Emmanuel V. Gwalanje alieleza bayana kuwa hajawahi kujihusisha na mambo ya siasa akiwa kazini na wafanyakazi wenzake ni mashahidi. Pia rekodi yake ya mahudhurio kazini ni nzuri lakini amesingiziwa hivyo kwa kuwa alihudhuria mkutano wa siasa baada ya saa za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumfukuza Ndugu Emmanuel V. Gwalanje ulikuwa mfupi sana. Notisi ya Mashitaka iliandikwa tarehe 18.03.2013, utetezi uliwasilishwa tarehe 21.03.2013, barua ya kufukuzwa kazi tarehe ilitoka tarehe 28.03.2013. Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba uamuzi wa kumfukuza kazi Ndugu Emanuel Gwalanje haukuwa wa haki ikizingatiwa kwamba hakuwahi kupewa onyo hata moja kama kweli alikuwa akijihusisha na kazi ya siasa wakati wa kazi.

Aidha, muda mfupi wa mchakato wa kufukuzwa kwake unatia shaka kama kuna uchunguzi wa kina uliofanyika kubaini bila shaka yoyote kuwa Ndugu Emmanuel Gwalanje kweli alihusika na kazi ya siasa wakati wa saa za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inamtaka Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mufindi, Ndugu E. Kaduma, pamoja na Afisa wake wa Mamlaka ya Nidhamu kuwasilisha mchakato na hukumu ya mashitaka dhidi ya Ndugu Emmanuel Gwalanje kwa Waziri wa Utumishi wa Umma ili kubaini uhalali wa mchakato mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetolea mfano shauri la Ndugu Emmanuel Gwalanje wa Halmashauri ya Mufindi, lakini yapo matukio mengi ya watumishi wanaofukuzwa kazi kiholela katika Halmashauri na taasisi za Serikali kutokana na chuki binafsi na unyanyapaa wa kisiasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukemea tabia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwa Watumishi wa Umma wanaoishi na VVU. Mwaka 2006 Serikali ilitoa Waraka wa utumishi wa umma namba 2 wa mwaka 2006 kuhusu huduma za watumishi wa umma wanaoishi na virusi vya ukimwi. Chini ya waraka huu waajiri wa watumishi wa umma wanapaswa kuhamasisha watumishi kupima VVU, na kutoa huduma muhimu kwa wale watakaokuwa wameathirika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe taarifa katika Bunge hili kuwa ni kwa kiwango gani waraka huu umetekelezwa na ni gharama kiasi gani imetumika mpaka sasa katika kuwahudumia watumishi wa Umma wanaoishi na VVU kwa maana ya lishe bora, madawa, nauli za kuhudhuria matibabu na stahili nyingine?

**NAIBU SPIKA**: Sikukupata kidogo Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, kwa sababu muda wenu bado, ile nusu saa haijakamilika, sijui huyu mwenzako ni nani wa kumalizia hizi dakika zilizobaki; au tunaendelea na uchangiaji sasa, maana alimalizia kwa kusema mwenzake. Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, ufafanuzi!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyozifanyia marekebisho Kanuni, muda wetu wa nusu saa ambao haujatumika unabaki ni halali yetu na utatumiwa na wale waliomba kuchangia kwenye mjadaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanasema aaah! Naomba tu niwarejeshe kwa yaliyotokea jana ambapo Mheshimiwa January Makamba, alikopa muda wa Waziri Majaliwa Kassim Majaliwa. Kwa hiyo nusu saa yetu ni ya kwetu na leo asubuhi naambiwa kuna Mheshimiwa Waziri mwingine amekopesha au kakopa muda wake kwa mtu mwingine, ndiyo Kanuni zinavyoenda.

**NAIBU SPIKA:** Ahasante sana, Makatibu zimebaki dakika ngapi? Ni dakika kumi, naweka kwenye benki yangu. Tunaendelea na uchangiaji waheshimiwa Wabunge. Sasa naomba usikivu wenu, kwa sababu wengi katika waliokuwa wameomba kuchangia siwaoni ingawa wataendelea kuja watatukuta tukiendelea na wale ambao angalau nawaona humu ndani, naomba tuanze na Hamedi Ali Hamadi na atafuatiwa na Mheshimiwa Halima J. Mdee na atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema, ambao wao watagawana dakika tano tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu ni nini tena?

**MHE. TUNDU M. LISSU:** Tulitakiwa tuwe na saa nzima, kwa sababu...

**NAIBU SPIKA:** Unazungumza na Mheshimiwa Celina Kombani au unazungumza na Naibu Spika!

**MHE. TUNDU M. LISSU:** Tulitakiwa tuwe na hotuba mbili kama ambavyo, ofisi ya Rais ina hotuba mbili. Tulitakiwa tuwe na saa nzima, tumetumia nusu saa, tumetumia dakika ishirini *actually*. Tumetumia dakika 20, sasa kwa vile tulikuwa na saa nzima yenye hotuba mbili tumetumia dakika 20, muda wetu wa dakika 40, hauwezi ukachukuliwa na watu wengine, huo ni wa kwetu.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Tundu A. Lissu, nakuomba ukae na niwaombe sana ushirikiano, waheshimiwa Wabunge. Muda wa Hotuba ya Kambi ya Upinzani huwa unalingana kabisa na muda wa hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati wa jambo lililohusika.

Kwa utaratibu wa leo, mwenyekiti wa Kamati iliyohusika, amepata nusu saa na tulieleza tangu mwanzo.

Mheshimiwa Professor Kulikoyela Kanalwanda Kahigi na wewe una nusu saa, ndiyo utaratibu ambao ulikuwa umepangwa leo, siku zote ndiyo hivyo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa uendelee, zile dakika kumi nimezikubali nitazitumia utakapo nielekeza na ule mgao wa dakika zako ninao kutokana na barua ambayo umeniandikia wewe mwenyewe Mheshimiwa Tundu A. Lissu na kuisaini wewe mwenyewe, na mligawana wenyewe dakika zako.

Nimefanya vitu ambavyo umenielekeza, situngi mambo ambayo ni ya kwangu mwenyewe, nafanya vitu ambavyo umeshanielekeza wewe mwenyewe, namna gani wachangiaji wako wawe na dakika ngapi watumie.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. Nashukuru nami kwanza kwa kunijalia jioni hii nikawa miongoni mwa wachangiaji katika Bajeti hii ya Ofisi ya Rais. Awali ya yote, naomba nianze na masikitiko katika hotuba yangu, hasa katika suala la Utawala Bora.

**NAIBU SPIKA:** Katibu yeye ni dakika kumi?

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri Celina O. Kombani. Suala la Utawala Bora limezungumzwa kwenye ukurasa wa 101, kifungu cha 88 kwa mistari kumi 15 peke yake. Hii inaonyesha kwamba, kwa CCM utawala bora siyo *issue*, na *issue* ni bora utawala na katika hili ndiyo maana, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, amekuwa mara kadhaa, akiomba serikali, ianzishe mjadala wa kitaifa, hili lingetupatia utawala Bora lakini pia utawala wa sheria na hata democrasia ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba sasa, nizungumzie au niseme kwanza kwamba, napata mshangao na sielewi vizuri, nikisikia kwamba tunasema tuna utawala Bora Tanzania.

Katiba tunayo itumie sasa ya mwaka 1977 Ibara ya 133, imesema wazi kwamba kuwe na *account* ya pamoja kati ya SMZ na SMT; jambo hili ni mwaka wa 46 sasa bado kuna kusuasua, inashangaza na naomba nihoji.

Wakati SMZ wameshaleta mapendekezo yao, lakini serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imelikalia jambo hili. Ikumbukwe pia kwamba baada ya iliyokuwa Afrika Mashariki, ile fedha ambayo ilikuwa iko kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, ilikwenda Hazina na ndiyo iliyotumiwa kama mtaji wa *BoT,* lakini mpaka leo hii, kumekuwa na kigugumizi katika kufungua *account* hii na ikifahamika wazi kwamba, inanyimwa fursa Zanzibar ya kujua kinachoingia katika Benki yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo utawala bora kweli? Lakini pia kama hilo halitoshi, bidhaa zote zinazoingia Tanzania kwa boda yoyote, kwa bandari yoyote, kwa huku bara inakuwa ni bidhaa halali kwa Tanzania nzima. Inashangaza mpaka leo kwamba bidhaa ikitoka Zanzibar, ikiingia bara inakuwa ni bidhaa ya magendo, jambo hili linasikitisha.

Pia, Raia wa Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda anapoamua kuja kutembea Tanzania kwa shughuri zake, akiamua anataka kuchukua gari, anaruhusiwa kuingiwa na anapewa *permit*. Inashangaza kwamba, Mzanzibari akisema nataka kwenda Dodoma, akisafirisha gari yake, lazima aweke bondi. Huu ndiyo utawala bora kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Balozi 31 za Tanzania nje ya Nchi, katika hizi, Wazanzibari ni wanne tu. Lakini pia katika ile Bodi ya Wizara *(Management Team*) inayoongozwa na Waziri na Naibu Waziri, ina *Directors* 18, katika hao Wazanzibari ni wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawlili hawa ni kwa sababu ya nafasi ya Naibu Waziri, lakini pia kwa sababu Zanzibar kuna Ofisi, ndiyo maana amepewa nafasi Mzanzibari pale, yuko pale bwana Asimai Kombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo Utawala Bora kweli! Naomba sasa nizungumzie suala la mauaji ya Raia Tanzania. Kumekuwa na tatizo kubwa, sugu ambalo bado linaendelea la mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi *(Albino),* lakini pia na wale Wazee na hata wenye sura za kizee kwa sababu ya dhiki ya maisha wanachukuliwa kwamba ni wachawi wanauawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, kwamba bado Serikali haijataka kulipa nafasi stahiki jambo hili. (*Makofi*)

Haijataka kulikomesha kwa dhati na inaonekana kama kwamba kundi hili la wenye ulemavu wa ngozi na wazee limekuwa kama hili ni kundi halali la kafara kwa Watanzania. Kesi nyingi za watuhumiwa waliofanya matendo haya ya kikatili zimepelekwa Mahakamani, kifungo cha miaka 20 si adhabu stahiki kwa kosa hili! (*Makofi*)

Pia kwa sababu watuhumiwa watano walihukumiwa kunyongwa na kwa sababu Rais hajasaini, imeonekana kwa wale wengine kwamba, kumbe hili si jambo gumu, kubwa na halina athari yoyote. Mauaji yameendelea na hivi karibuni miezi mitatu iliyopita *Albino* wawili wameuawa na wawili wamekatwa viungo vyao.

Naiomba Serikali, iombe msaada kama hili limekuwa gumu ili tupate Wataalam wa kuja kuchunguza matokeo haya ya kikatili wanayofanyiwa kundi hili la Watanzania wenzetu. Ikiwa hili haliwezekani, mimi hapo ndiyo naendelea kusema kwamba je huu ni Utawala Bora kweli? Kwamba kundi fulani liwe ni Mbuzi wa kafara katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hali ya uchumi. Mwaka 2011, pato la Mtanzania lilikuwa ni laki 869,432.36, ambazo ni sawa na shilingi 72,453 kwa mwezi ambazo pia ni sawa na 2,415 kwa siku, lakini pia 2012 pato ni 995,293 sawa na 82,000 wastani kwa mwezi, lakini pia sawa 2,764 kwa siku. Serikali imekuwa ikisema kwamba tuna maisha bora kwa kila Mtanzania, Serikali ya CCM inahubiri maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilo ya mchele inauzwa kwa 2,300, Mtanzania anayepata 2,700, ukipata mchele lazima upate mboga, lazima watoto waende shule, waende hospitali, halafu tunaweka bei Watanzania kwa kusema kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania, haya si maisha bora kwa kila Mtanzania, hili ni balaa kwa kila Mtanzania na huu si Utawala Bora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ahmed kwa kutuanzishia mjadala wetu, sasa kama nilivyosema Mheshimwa Godbless J. Lema, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima J. Mdee kufuatana na orodha yangu na wote nawapa dakika 10.10. Sasa tuelewane, CHADEMA mna dakika 40 na kwa kadiri ya muda wenu mmegawana dakika 10, 10 wote wanne katika orodha yenu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, ni mara ya kwanza naongea Bunge hili, baada ya kutoka likizo ya muda mrefu niliyokuwa nayo ya kuvuliwa Ubunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda sana kujikita katika suala la udini, ambalo nimesikiliza mijadala mingi sana humu Bungeni kuanzia juzi na ninaona viongozi naona Wabunge wenzangu jinsi ambavyo kwa namna moja ama nyingine wanapojaribu kuchenga ukweli ambao uko wazi sana huko mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili limegawanyika, wala siyo siri. Taifa hili lina mgogoro mkubwa sana wa itikadi ya kidini na waasisi wa mgogoro huu wanajijua ni Chama cha Mapinduzi. Wakati Chama cha *CUF* kinapata nguvu za kisiasa miaka michache ya nyuma iliyopita, Chama cha Mapinduzi kilisema, kiliwaambia wakristo, Chama cha *CUF* ni Chama cha uislamu, na baadaye Chama cha *CUF* kilivyokuwa dhoofu katika maeneo mengi katika eneo la Tanzania Bara, CHADEMA ilianza kupata nguvu na ikapata kiongozi wa kambi rasmi ya upinzani Bungeni.

Chama cha Mapinduzi kiliwaambia waislam CHADEMA ni chama cha Wakristo. Tatizo ambalo hamkuliona ambalo mliendelea kulifanya sana huko mitaani, mlifikiri mnaweza mkagawa vyama vya siasa kwa itikadi za kidini, bila kuwagawa watu kwa itikadi za kidini na ndiyo maana sasa migogoro mikubwa imeanza kuibuka ya nani achinje nani achinjiwe, kwa sababu ya siasa za Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho mnafikiri mnaweza mkakaa madarakani kwa kivuli cha siasa za kidini na siasa za ukabila.

Bado mnaendelea kusema hadharani kutumia viongozi wenu wa chama kwamba CHADEMA ni chama cha ukanda cha kikabila, mkifikiri mtapunguza nguvu ya CHADEMA.

Lakini kumbe mnaendelea kugawa Taifa kwa ukabila na udini na ninashangaa wanaosema hivyo wengi ni mabwashee wetu kama Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba ni kinara wa siasa za ubaguzi, lakini ni bwashee wangu ameoa kule Moshi, sasa sijui tatizo la watu wa Kanda ya Kaskazini ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa hili tukikwepa ukweli wa kujadili suala la udini wakati huu, itakapofika miaka michache inayokuja Taifa hili litaingia katika mgogoro mkubwa na Nchi hii inakwenda kuingia kwenye vita kubwa ya dini zetu, na mambo haya yamefanywa na hata juzi Mheshimiwa Joseph R. Selasini alivyoleta hapa *CD* ya kilichokuwa kinaendelea kule *UDOM*, bado hauoni kama Serikali imechukulia kwamba ni jambo *Serious, CD* ile ni mbaya inachochea vurugu za kidini, lakini Serikali inaogopa kulishikilia jambo hili kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unagundua mambo mengi sana, unagundua kwamba suala hili, linafanywa kwa makusudi na ni mkakati wa makusudi na ni mpango ambao mimi siogopi kusema, niseme tu kwamba wakati nakwenda kuongea maneno haya, nahofia kucha zangu, nahofia meno yangu na kope zangu ambazo Usalama wa Taifa wamekuwa wakitumia *pliers* kuzitoa.

Lakini kwa sababu ya nchi yangu nasema kwamba mnaogopa kusema suala la udini! Kwa sababu anayehamasisha mkakati wa udini ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno kuyasema inahitaji kusema kama nilivyotangulia kusema kwamba kucha zangu zinaweza zikawa hatarini na kope zangu, lakini kwa sababu ya watoto wangu nitasema ukweli na ninyi mnajua ukweli, ndiyo maana linapokuja suala la udini, badala ya ya kushughulikia mambo ya msingi, mnapitapita pembeni wakati nchi yetu ikiendelea kuharibika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, naona umesimama. Mheshimiwa Godbless Lema tafadhali, Makatibu tunzeni muda wa Mhemiwa Godbless Lema.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, sijui tutafanya nini Bunge hili, maana tumesema lakini hatusikilizwi. Kanuni ya 64(1)(d), inakataza kutumia jina la Rais kwa dhihaka, msemaji aliyetangulia kusema sasa hivi Mheshimiwa Godbless Lema, anasema Rais Kikwete, kwa jina, ni mwasisi wa masuala ya udini Tanzania, hii ni dhihaka ya ajabu!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kiti chako kichukue hatua ya kumwomba Mheshimiwa Lema, athibitishe au afute kauli hii kwa sababu inakiuka Kanuni za Bunge.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba matatizo makubwa ya viongozi ya Serikali ni uoga na dhambi kubwa kuliko zote duniani ni uoga, hakuna kauli ya kufuta hapa isipokuwa kusisistiza, kwamba anaye-*insist* na anayefanya siasa za ubaguzi katika Taifa hili ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, kushirikiana na wewe kama Waziri katika Taifa hili.

Mheshimiwa William Lukuvi jana wewe umeongea na Mheshimiwa Selasini, *CD* imeletwa Bungeni hapa ya mambo ya udini *UDOM* unamwambia Mheshimwa Selasini hiyo ni *CD* ya CHADEMA imetengenezwa, na ni Waziri, unaongea kauli kama hiyo, ni Waziri. (*Makofi*)

Sasa unaona dhihaka kwa sababu ni ukweli, hii kauli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema ni vizuri ukaelekeza mazungumzo yako kwangu, mkishaanza kushambuliana ninyi kwa ninyi, kwa vyo vyote kikao hiki kitakuwa kigumu, endelea lakini zungumza na mimi kama Mwenyekiti, endelea Mheshimiwa Godbless Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya *reference* kwa sababu jana pia alifanya dhihaka hiyo na anaona dhihaka kwa sababu haoni Taifa hili mbele ni nini kitatokea, anaangalia maslahi yake, Ujumbe wake wa Kamati Kuu na cheo chake, lakini sisi tunaangalia Taifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Lukuvi, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimeomba Mwongozo wako, lakini la pili, jana Mheshimiwa Selasini alipotoa hizi *CDs*, mimi nimekwenda kwa Katibu wa Bunge kuzidai, na Mheshimiwa Selasini akaambiwa na Katibu wa Bunge kwamba hatuzipokei hizi mpaka uweke sahihi kuonyesha kwamba umezileta wewe.

Sijaziona, wala sijazipokea, Serikali haijapokea hizo *CDs*, hayo maneno anayoyasema humu ndani mimi siyaelewi, kwa sababu hizo Kanda wala sijaziona, hazijakabidhiwa kwangu na Katibu wa Bunge amesema mbele ya Mheshimiwa Selasini, athibitishe hapa na mimi nikiwepo, kwamba hatazipokea mpaka aweke sahihi kwamba ni za kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Bunge lako Tukufu linaruhusu watu kuzusha maneno yasiyokuwa ya ukweli? Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanatuangalia. (*Makofi*)

Kama kila mmoja ambaye ana nia ya kuongea leo, atazungumza kama tulivyokubaliana, hakuna tatizo hata kidogo, niko hapa kulinda muda wa kila mmoja kuzungumza kidemokrasia kabisa.

Lakini mkichagua kuanza kupakazana maneno, kuanza kueleza maneno ambayo sisi hatukuwepo, wala hatupo, tukianza kusema hapa kwamba toeni ushahidi yatakuwa ni magumu sana na ninyi ni Waheshimiwa Wabunge, si jambo zuri kuwakatakata. Kwa hiyo, natoa Mwongozo tena kwa mara nyingine Waheshimiwa Wabunge, tujielekeze kwenye hoja iliyo mbele yetu. Mawaziri hawa wameeleza mambo waliyoyaeleza, sasa tuchangie tujielekeze katika hoja.

Mheshimiwa Godbless Lema endelea, dakika zake mumlindie. Muache malumbano tafadhali. (*Makofi*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya siyo malumbano, huu ni ukweli ambao ama muukubali ama muukatae mimi nitaendelea kuusema kwa sababu ya Taifa langu. (*Makofi*)

Kuchangia hoja siyo lazima ninyi mfurahi na niko hapa kupigania Taifa langu, ninachosema, ni kwamba tatizo la udini lina asisiwa na viongozi wakubwa wa Chama cha Mapinduzi na lina asisiwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), ndiyo sababu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko na kwa sababu nilivyo hivi sitakiwi kushiriki kwenye mabishano, nina tai halafu na kitambaa hiki, ambacho ni ushahidi wa ustaarabu.

Hoja iliyoko mbele yetu na ninamwomba ndugu yangu Mheshimwa Godbless Lema, apunguze kidogo haya mambo mengine. Hoja ni kwamba, amesema, mtu ambaye ni kinara wa mambo ya udini, ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na amemtaja kwa jina.

Sasa aliposimama Mheshimiwa Waziri ameomba kwamba, ametaja ile Kanuni ya 64 (1) (d), inayosema Mbunge hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala. Sasa hiyo ndiyo hoja iliyoko mbele yetu, sasa. Je, maneno ambayo Mheshimiwa Godbless Lema ameyasema ni dhihaka? Upande huu na ni maoni yangu, kwamba maneno hayo ni ya dhihaka na yanazuiwa na Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ambacho kingefanyika, ni kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Godbless Lema, namheshimu sana na yeye anajua kabisa kwamba namheshimu. Aidha afute ile kauli au wewe sasa utoe Mwongozo kwamba haya maneno yanaruhusiwa? Badala ya kuanza kubishana sisi Wabunge wananyosheana vidole na mimi naogopa kwamba, nilivyo hivi, sistahili kabisa kushiriki katika ugonvi wa aina hii.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU- MNADHIMU MKUU WA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mnazimu wa kami rasmi ya upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Pia nikikuita Mheshimwa Tundu Lissu nadhani sijakosea wala sijakuvunjia heshima na wewe ni Mheshimwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MNADHIMU MKUU WA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Naomba kwanza kama inawezekana na mimi nikope busara za Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64 (1) (d), inakataza kutumia jina la Rais kwa dhihaka, haijakataza kumkosoa Rais. (*Makofi*)

Inakataza kutumia jina la Rais kwa dhihaka, bahati mbaya, sikuja na Kamusi hapa ya Kiwahili, tuone tafsiri ya neno dhihaka ni nini! Kwa maoni yangu pamoja na kwamba

sina Kamusi ya Kiswahili, dhihaka ni mambo ya kiutani utani hivi, kama angesema yule Rais msanii, hii ingekuwa dhihaka, au maneno ya aina hiyo. Lakini kusema kwamba ana asisi ni maneno makubwa yenye nguvu, lakini hayawezi yakachukuliwa kuwa ni dhihaka. (*Makofi*)

Labda tubadilishe leo tafsiri ya neno la Kiswahili dhihaka iache kuwa utani utani, iwe kwamba usimseme vibaya. Anamsema si vizuri, anatumia maneno ambayo siyo mazuri kwa jina la Rais, lakini siyo, dhihaka na hayo maneno ambayo anayatumia, yanaruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni, kwa sababu siyo ya dhihaka, Kanuni haijasema Rais asikosolewe, *conduct* yake isishambuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri upande wa pili watuvumilie tu, tukianza kutumia maneno ya dhihaka wasimame, lakini haya ambayo ni *criticism* yaani *honest criticism*, hayawezi yakawa yakachukuliwa kuwa ni ya dhihaka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, si vizuri kuonyeshana umahiri wa lugha ya Kiswahili, lugha ambayo nimeisomea, maneno haya aliyosema Mheshimiwa Lema, hatumwekei mdomoni, anasema Rais ni mdini!

Kinara maana yake nini, mdini na mdini ni sawasawa na kusema ni msanii, sasa kwa hiyo, kama unaona maneno haya siyo dhihaka, mimi ninaomba Mheshimiwa Lema athibitishe ukinara wa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba unilinde. Kama Mheshimiwa Godbless Lema anaweza kumkosoa Rais na mimi ninamkosoa humu ndani kwa sababu sasa hivi vyuo vikuu vina uchaguzi na wanafunzi wamelalamika *UDOM* kwamba Mheshimiwa Lema ni mlezi wa CHADEMA *UDOM,* jana umeonekana na wanafunzi kwenye basi ukiwatoa *UDOM* na siyo.....

**MBUNGE FULANI:** Siyo dhambi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Siyo hilo tu, tunafahamu hata Mheshimiwa Mnyika anafanya hivyo kwani nimeshamkuta mimi mwenyewe mara nyingi *Mabibo Hostel* akifanya hivyo ....

**MBUNGE FULANI:** Hiyo siyo dhambi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Na hizo zote ni mbinu za ....

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Ni mbinu za kueneza uchochezi pamoja na udini.

**MBUNGE FULANI:** Umesimama kwa Kanuni gani?

**MBUNGE FULANI:** Kanuni gani hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Kanuni gani hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wananchi wanafuatilia pia mijadala ya namna hii ina afya tu kwa sababu inasaidia wananchi kuweza kujua ni nini ambacho kinaendelea, nini kinaruhusiwa na nini hakiruhusiwi.

Mheshimiwa Godbless Lema baada ya kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Je, unauchukua ushauri huo ili uweze kumalizia dakika zako? *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa maoni yake na sijafanya dhihaka kwa jina la Rais ila nilichokisema ni kwamba Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ni mwasisi wa siasa za udini pamoja na ninyi.

Kama unataka nithibitishe kama alivyodai naomba nithibitishe kwanza yale ya awali ambayo ninayo mengi tu humu ndani ya kuthibitisha halafu nitathibitisha na hili. Nipo tayari kuthibitisha lakini yale ya mwanzo kwanza niyathibitishe halafu nitathibitisha na haya. Niko tayari! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee!

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ni makali sana lakini yana maana kubwa sana katika taifa letu na nimekuwa *serious*..... kidogo. Nimeona wengi mnapiga chenga kuongea ukweli ambao unaweza ukalisaidia taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba leo hii tunavyoongea kuna migogoro mikubwa sana ya kidini katika taifa letu. Mheshimiwa Wasira alikwenda Mwanza kwenye mgogoro wa nani achinje kati ya Muislamu na Mkristo. Lakini ukiangalia hata jinsi mgogoro ule ulivyotatuliwa unagundua kwamba kulikuwa na hekima iliyojaa hofu na siyo ujasiri kwa Serikali yenye mamlaka ambayo inaongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchinja ama kutokuchinja imekuja na limekuwa ni suala la imani. Muislamu anaposema Mkristo akichinja hawezi kula ni suala la imani na Mkristo akisema hawezi kula nyama iliyochinjwa na Muislamu siyo dhambi na wala siyo udini kwa sababu ni imani. Lakini badala yake unaona jinsi ambavyo Serikali ilikwenda kutatua tatizo lile, Serikali ikasema Waislamu waendelee kuchinja nyama kama ilivyokuwa huko nyuma siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli ilikuwa hivyo siku zote na sasa imeshakuwa tatizo la kiimani na kama limeshakuwa tatizo la kiimani maana yake ni kwamba mgogoro huu ni lazima utatuliwe kwa hekima za kiimani na huwezi kutumia bunduki wala risasi kulazimisha dini nyingine kufuata itikadi ya dini nyingine na kufanya hivyo haionyeshi busara bali inaonyesha woga wa kutetea imani za dini hizi mbili.

**NAIBU SPIKA:** Kuna taarifa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Lema kwamba nilikwenda Mwanza na nilipokuwa Mwanza nilizungumza na watu wa madhehebu yote, naam! Vilevile nilikwenda Geita nilichowaambia ni kwamba suala la mgogoro wa kiimani haliwezi kuamriwa na Serikali.

Pili, niliwaambia kwamba katika nchi yetu hakuna sheria ambayo inasimamia uchinjaji. Kwa hiyo, nilichosema Mwanza na Geita ni kwamba madhehebu yale wakutane wazungumze na waondoe mgogoro wao na waishauri Serikali namna ya kumaliza mgogoro huo. Lakini kwa sababu uchinjaji hauwezi kusimama wala hatuwezi kusimamisha watu kula nyama nilisema waendelee na utaratibu uliopo mpaka madhehebu yale yatakapokutana na kuishauri Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema malizia muda wako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ninaosema woga wa Serikali. Mheshimiwa Wasira ame - *confess* hadharani hapa kwamba yeye ni Serikali amekwenda Mwanza amekuta kuna mgogoro anasema akawaambia, sasa wewe ni Serikali unamwambia nani? Kwa sababu maana ya Serikali maana yake ni *Mediator*.

Mheshimiwa Wasira alichotakiwa kukifanya sasa ni kukutana na viongozi wa dini zote mbili kufahamu mantiki ya kiimani ya jambo hilo lakini akasema nikawaambia halafu akaondoka, alitaka Mbunge ama Diwani afanye jambo hilo? Hii inashangaza na ndiyo maana nasema hii ni woga wa Serikali wa kujadili mambo ya msingi yanayohusu udini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaweza mkatuchukia mkaona kama tunaongea hovyo lakini tusiposema mambo hayo nchi hii iko kwenye mgogoro mkubwa wa kiimani na taifa hili leo litaingia pabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo meseji zinatembea, nchi hii miaka iliyopita Rais alikuwa akifanya uteuzi watu walikuwa hawajadili dini wala kabila la mtu, lakini leo ukienda kwenye mitandao ya kijamii Rais pindi anapomaliza kufanya uteuzi watu wanauliza dini ya huyo mtu ni dini gani. Haya siyo mambo ya kufumbia macho bali ni mambo *sensitive* ambayo tukiyaacha yatapasua taifa. Watu walikuwa wanatambuana kwa *contents* na siyo dini wala kabila zao, lakini leo imekuwa ni *serious issue*.

Mimi nashauri Bunge hili ni bora likaenda kwenye *retreat* wakaona namna gani wanaweza wakafikiria vema tatizo la udini na ukabila. Siyo tatizo dogo ni tatizo serious na litaligawa taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya usalama wa taifa, sitataja majina ya wale viongozi wa usalama wa taifa ambao wanaongoza lile genge la kutoa watu kucha na meno, sitawataja kama ambavyo mmekubaliana kwenye vikao vya Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo kama taasisi ya Usalama wa Taifa inatiliwa mashaka na wananchi, viongozi wake wanaonekana wanafanya *communications* za kuumiza watu siku wananchi wakiamini usalama wa Taifa hauko nao?

*(Hapa Kengele Ililia Kuashiria Muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, ni kengele ya pili Mheshimiwa Lema. Nilisema nilinde muda wa mchangiaji na wachangiaji wengine kazi yangu kubwa ni kuwalinda kuhakikisha kwamba ile Ibara ya 100 ya kutoa mawazo kwa kweli kila Mbunge inafanya kazi vizuri kwake.

Lakini kwa maneno ambayo ameyasema Mheshimiwa Lema na kurudia tena kwamba ana ushahidi nayo kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ndiyo mwasisi wa udini unaoendelea hapa nchini. Kwa hilo nitamtaka Mheshimiwa Lema ndani ya wiki moja yaani siku saba, basi atuletee ushahidi wa jambo hilo ili Bunge hili liweze kufahamu kuhusu jambo hilo.

Tunaendelea na uchangiaji na nilimtaja Mheshimiwa Halima Mdee lakini simwoni humu ndani, kama Mheshimiwa Chiku Abwao uko tayari naweza nikakupa dakika hizo kumi, upo katika orodha yangu pia.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe shukrani kwa ofisi yako ilivyoshiriki kikamilifu wakati nikiumwa kwa misaada mbalimbali. Nashukuru sana na ninawashukuru sana watendaji wote wa Bunge na ninawashukuru sana Wabunge wote ambao wameshirikiana na mimi wakati nikiwa na matatizo.

Pia namshukuru sana kiongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kunijali wakati nilipokuwa naumwa lakini na Wabunge wenzangu wote nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limefika mahali pabaya, Bunge sasa linaendeshwa kwa hofu, Bunge linataka kudhibiti wapinzani tuseme nini. Sisi ni Wabunge wa Chama cha Upinzani yaani Kambi Rasmi ya Upinzani ndani ya Bunge. Tupo hapa kwa kazi moja tu ya kuhakikisha Serikali iliyopo madarakani inawajibika ipasavyo na kuhakikisha tunatetea maslahi ya wananchi waliotuchagua wakiamini sisi ndiyo tunaoweza kuikosoa Serikali kihalali ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini sasa kinachojitokeza ni kwamba tuseme yale ambayo Serikali inapenda tuyaseme, tuje hapa kuipongeza Serikali. Lakini pale tunapopingana nao kwamba hawatendi vizuri ni kosa, tunapoikosoa ni dhambi.

Sasa hivi tunapelekeshwa kufikisha hatua ya kusema vibaya, kiongozi ambaye yupo ndani ya chama tawala Mheshimiwa Mbunge anaamua kusimama hapa kwa makusudi kuanza kutuchokoza na kututukana na kutukashifu. Lakini sisi tukijibu ni kosa la jinai, tutukanwe tunyamaze, lakini tukijibu na kukosoa ni kosa! (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inakaa inajadili mambo gani ambayo inaonekana yanafaa yatekelezwe na Serikali, inaleta hotuba hapa lakini cha kusikitisha yale mazuri yote ambayo yanakuwa yamependekezwa na Kambi hayaonekani, yanayotiliwa mkazo ni yale malalamiko ya mapungufu ambapo kiongozi Mkuu wa Bunge anasimama hapa Bungeni anaamua kuponda ponda toka mwanzo wa kujibu hoja zake mpaka mwisho wa kujibu kwamba Kambi ya Upinzani, hatuendi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia bado nasimamia suala la Utawala Bora. Nchi yetu kama hatutazingatia suala la Utawala bora sijui niseme kitu gani, kwa hakika tutafikishwa mahali pabaya. Sasa hivi nchi hii haina amani tena kwani watu wanakamatwa, wanapigwa na kuumizwa haya yote yanahusika na Utawala Bora lakini leo hii tukisema tugusie tu suala la Utawala Bora tuulize kwa nini watu wanashikwa na kupigwa, kwa nini wale wanaoonekana wanaikosoa Serikali

wanapata matatizo ni kosa, mnataka sisi Wabunge tuje tuzungumze nini hapa Bungeni? Mnataka sisi tuje hapa kukaa na kushangilia wakati wenzetu wanateseka? Tuje hapa tuanze kuwasifia wakati hamstahili sifa? Tukianza hapa kuwasifia kila kitu ina maana sasa hivi upinzani hauna maana hapa Bungeni kuwepo, tukae tu nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni kwamba Kambi ya Upinzani iheshimike, iheshimike na chama tawala kitambue kwamba ni wajibu wetu sisi kuwakosoa, huo ndiyo wajibu wetu. Tunawakosoa ili muweze kurekebisha ule upungufu ambao haustahili muweze kuweka taifa liende vizuri lakini tukisokoa inakuwa ni shida. Hatuendi vizuri!

Masuala yanayofanyika sasa hivi katika taifa letu ambayo mimi naweza kusema kwa kweli yanaasisiwa na Chama cha Mapinduzi, Chama cha Mapinduzi kinatetea maovu, hakiko *serious* kukemea kwa vitendo ndiyo maana leo hii mtu hata akipigwa ama akiumizwa Serikali haitaki tuzungumze ndani ya Bunge, inadhibiti maovu na hata hizi Kanuni na sheria zinazowekwa ndani ya Bunge hapa ni za kudhibiti maovu kwamba kama kesi ikienda Mahakani isizungumzwe na hata kama hazungumzii suala la Mahakama.

Watanzania wanataka watusikie tukisema sisi kwamba watu wanapigwa, wanatekwa nyara na hawana amani. Sisi Kambi ya Upinzani tunasema nini ndani ya Bunge? Ni wajibu wetu na tutasema! Matokeo yake mambo mabaya yanafanyika Serikali inaona lakini haichukui hatua za msingi bali inaamua kubambikiza kesi kwa watu wasiokuwa na hatia ili mradi tutakaposema kusema ndani ya Bunge ionekane kwamba sisi tunasema mambo ambayo yapo Mahakamani.

Kesi Mahakamani haziishi, ni utawala bora gani huu? Tutasemea wapi? Wananchi wanategemea nini? Hatuwezi kuwa tunaogopa kuzungumza mambo ya msingi ambayo yanaonekana wazi yanakiukwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuhofia kwamba tutaonekana hatuna nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho Chama cha Mapinduzi kinatakiwa kitambue na kikubali ni kwamba hakuna chama chochote ambacho kitaingia madarakani ambacho kitaendesha Serikali kwa uwezo wa mawazo yake peke yake, hakuna! Hakuna kabisa! Chama ambacho kitaingia madarakani na hii naiongea kwa msisitizo kabisa.

Chama ambacho kitaingia madarakani kikijiamini kwamba chenyewe kimeweza kushinda kikaingia madarakani kwa ushindi wa kuchaguliwa na wananchi kwa kura nyingi kwamba kitaongoza nchi hii kwa kutegemea mawazo ya wao wenyewe kama walivyo, hicho kitu hakipo. Ni lazima muwe tayari kupokea mawazo ya vyama vingine na kuyafanyia kazi.

Lakini leo hii staili ambayo mmejiwekea Chama cha Mapinduzi hamtaki kupokea maoni yoyote yanayotoka upinzani hata kama hoja zikiwa nzuri namna gani hamtaki kuzipokea, hivi nini mnafikiri ni binadamu wa aina gani ambao mmekamilika kwa kila kitu, hamuwezi mkashaurika.

Tunapofikia hatua kama hiyo ya ninyi kutuona sisi kama vile ni watu ambao hatuna maana wala hatuna ushauri wa kutoa ndani ya Serikali yenu ndiyo haya yanapofika kwamba yale ambayo yanalalamikiwa na wananchi ambayo wananchi wanafikiri sisi kama wasemaji wao wakuu kwa sababu wapinzani wa Serikali ndiyo wenye fursa ya kuangalia upungufu.

Mtu hajiangalii mwenyewe nadhani ndiyo mfumo wa vyama vingi ulikuja kwa staili hiyo kwamba tunatakiwa sisi tuwakosoe ninyi ili na ninyi mwendeshe shughuli za Serikali vizuri lakini ninyi sasa mnataka kutufanya sisi tuwe kama mandondocha hapa na kibaya zaidi mnataka kupotosha zaidi maana ya amani, amani mnataka kuchukulia kwamba ni ujinga, ni mtu ambaye anakubali tu kufanyiwa vyovyote vile, asiwe na chochote cha kusema, asikatae kuonewa, asikatae kunyanyaswa eti akifikia hatua hiyo anavuruga amani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao nakukumbusha tu kuongea na kiti, endelea.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naongea na wewe lakini sijakutazama tu maana hapa naongea kwa sababu ya ruhusa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ninayosema ni mambo ambayo yanatia uchungu.

Chama cha Mapinduzi kama chama kikongwe ambacho ndiyo chama cha siasa mwasisi wa nchi hii, chama ambacho kilitakiwa kuwa mwongozo mzuri, yote haya yanayotokea ndani ya Bunge kukosa nidhamu au chochote kile inatokana na Chama cha Mapinduzi kwa sababu hamfanyi vizuri matokeo yake watu wanakosa kuelewa wafanye nini na waseme nini. *(Makofi)*

Chama cha Mapinduzi mkiamua kufanya mambo kwa hekima na mkiamua kuwa wasikivu kama mnavyodai kwamba Serikali yenu ni sikivu mkasikiliza yale yanayolalamikiwa mkayafanyia kazi Bunge hili litakuwa na nidhamu. Viongozi wetu wanaoongoza Bunge ukiwepo wewe Mheshimiwa Naibu Spika, haki ikitendeka isionekane kwamba kuna upande wowote unaoonewa, basi Bunge litakwenda vizuri.

Kinachotakiwa ni haki, heshima itakuwa na amani itadumu lakini kama hali itaendelea hivi *Chief Whip* wa Upinzani akisimama hasikilizwi mara moja mpaka aseme mara tatu au nne.........

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chiku Abwao, ni dakika kumi zimekwisha!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Moza atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu.

Mheshimiwa Moza Abeid!

**MHE. MOZA ABEIDI SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa na mimi nafasi ili niweze kuongea machache kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kupanda kwa mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuelezea kwamba mishahara imeongezeka kwa kiasi cha 20,000/=.

Je, kiwango hiki kinaendana sawa na hali ya uchumi iliyokuwepo sasa hivi katika nchi yetu? Tukumbuke kwamba juzi tu tangazo limetangazwa kwamba nauli zimepanda bei, iwapo kama nauli zimepanda bei mfumuko nao wa bei umepanda.

Je, Serikali inadhibiti vipi mfumuko huu wa bei na ongezeko la mshahara waliosema kwamba wameongeza mshahara?

Tutabeba kapu la mishahara kichwani ili kwenda kununua bidhaa zenye mfumuko wa bei juu uliopo katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa nini Serikali isiwe na mpango wa kudhibiti mfumuko wa bei ili kila mwananchi apate unafuu na mfanyakazi wa kima cha chini naye apate unafuu wa maisha katika ongezeko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la utumishi, katika nyumba za watumishi. Nyumba za watumishi ilikuwa Serikali hapo awali au mwanzo ilikuwa ikijenga nyumba za watumishi karibu na maeneo wanayofanyia kazi.

Lakini sasa hivi imekuwa ni kero kubwa mno katika nchi yetu ya Tanzania. Imefumuka kujenga mashule mengi na mashule haya ukitaka kuangalia shule imejengwa lakini shule iliyojengwa haina nyumba za Walimu hata moja, mwalimu anakaa mbali na shule anayofundisha katika eneo la shule, hivi unategemea kwamba elimu hii kweli tutakuwa nayo?

Kiwango cha elimu pia kinachangia kushuka kwa staili ya namna hiyo. Iwapo kama Serikali ingetoa huduma zote katika maeneo ya shule inapojengwa kwa kweli nafikiri hata hili suala lingine nalo lisingekuwa kero katika nchi yetu ambayo sasa hivi tunaliona na bado udhibiti mkubwa wa utendaji wa kazi bado haujafanyika hasa kwa ufasaha katika nchi yetu ya Tanzania na wala hakuna utawala bora wala uwiano wa kiwango ambacho kwamba tunasema sasa tunatendeana haki, bado tunamkandamiza mtu mmoja.

Tuje kwenye suala la nyumba za watumishi wa afya, tunashuhudia kwamba watumishi wa afya na vituo vingi vimejengwa vya afya lakini havina watumishi karibu, nyumba ya Mganga inajengwa mbali kabisa na kituo cha afya, hivi unategemea kwamba mama mjamzito anayetaka kwenda kujifungua katika kile kituo atamkuta muhudumu wakati huo ili aweze kujifungua. Hii inachangia kwa kiasi kikubwa mno cha kupoteza uhai wa Mama hasa katika maeneo ya Wilaya zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi mzuri wa hospitali moja ya huko Mloda, mzazi anapokwenda kujifungua amkikuta yule Daktari hayupo anatozwa shilingi 10,000, akikutwa amejifunga pale bila yeye kuwepo anamtoza yeye shilingi 10,000. Je, kama angekuwa karibu na eneo hilo, si ingedhibitiwa, hata rushwa nayo isingekuwepo kama wale watu wa rushwa wangekuwepo maeneo hayo. Unakuta hata hao wanaoambiwa wanakula rushwa, rushwa yote inatendeka Wilayani na Mijini lakini huko vijijini haiko, hebu mwaangalie Daktari huyo kitendo anachokifanya. Kwa kweli kinawaumiza watu sana wa eneo hilo katika Mkoa huo wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la Polisi. Polisi wetu ni watu ambao tunastahili tuwatendee haki. Polisi anaishi katika nyumba moja na watoto wake, je, huu ni utawala bora? Polisi anapokaa yeye na mtoto wake kwa kutenga na pazia, je, hayo ni maadili mema? Unategemea akiamka asubuhi atafanya vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta yule Polisi ambaye ametoka *depot* leo hii kwa kuwa ana cheo kikubwa kidogo anapewa nyumba yenye vyumba viwili lakini yule wa zamani ambaye ana mke na watoto wanalala kwenye chumba kimoja kwa kukitenganisha na pazia. Je, hebu mtwambie, huu ni udhalilishaji gani ambao mnaowafanyia Polisi? Serikali lazima ijenge nyumba za watumishi karibu na maeneo wanayofanyia kazi. Hebu tuige mkoloni alivyokuwa amefanya na sisi labda huenda tutakafanikiwa mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la MKURABITA. Dhana ya mwongozo huu, kwa kweli bado haijaeleweka na wala haiwaletei tija wananchi walio wengi na hasa wa huko vijijini. Suala hili linasababisha adha kubwa ambapo wananchi wanakosa hatimiliki za kimila ili kuweza kupata mikopo. Hebu tuangalie migogoro iliyopo ya ardhi katika maeneo mengi ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ninayo miwili, mitatu, ninaweza kutoa. Mgogoro mmoja upo katika Wilaya ya Kondoa, Mkongonero. Wananchi wale walikuwa wanalima katika eneo lile na limeonekana kwamba ni eneo la hifadhi wameambiwa waondoke na wameambiwa tu waondoke lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko na kuelekeza katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa awaambie watu wale waendelee kulima kwa mwaka huu, mwakani waweze kutafuta maeneo mengine wakalime. Je, kiutawala bora watu wale wanakwenda wapi bila kupewa hata fidia? Watu wale sasa hivi wana adha kubwa, wamechomewa nyumba zao, wamechomewa mbegu zao, vitu vyao wamenyang'anywa na vitu vingine na watu wengine karibu 25 wameshtakiwa wapo Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie kule Mwanza eneo la Bugarika. Bugarika hali kadhalika watu hivyohivyo wamenyang'anywa viwanja na wanauziwa kwa bei ghali, wananchi haohao na Serikali hii hii, je, huu ndiyo utawala? Naomba Waziri atapokuwa anafanya majumuisho yake atueleze nini maana ya utawala bora na ufanisi wa utendaji kazi katika nchi yetu ya Tanzania. Mbona tumekuwa tukifanya kazi kimazoea zoea tu. Kwa nini tusifanye kazi kwa kulingana na viwango vya kuweza kuthaminiana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nitarudi katika dhana hiihii ya utawala bora katika eneo la Kondoa hilohilo. Haohao viongozi wakubwa walioambiwa kwamba wawaangalie wananchi wale na wawaondoe katika eneo lile, wao ndio wameenda kulima katika eneo lililopangwa la malisho, wanalima wao na ndiyo wananufaika wao na ni kwa nini na ni utawala gani uliokuwa bora na Serikali inajua na inaliangalia hilo. Kwa nini inalifumbia macho na wananchi wale waliokuwa kule wanaambiwa waondoke? Hivi wale ndio hawana haki na maisha yao yamekuwa ndio basi au hao wenyewe ndiyo wao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hili, nije kwenye *TASAF*. *TASAF* ina miradi mingi hususani ujenzi wa madarasa ya shule, madawati na kadhalika lakini utakuta kwamba viongozi wa Halmashauri hawaongozi wala hawakai

na hii Kamati ya Ujenzi kwa kushirikiana nao kwa kuongoza katika Kata kwa ufanisi wa ujenzi. Miradi mingi inajengwa haileti ufanisi wala tija mfano ni maghorofa yale yanayoanguka na mashule halikadhalika hivyohivyo yanaezuliwa na baridi baadaye wanarudia tena kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie kwenye miradi, miradi mingi imeorodheshwa na *TASAF* lakini fedha zinafika ila miradi ni hewa. Kuna miradi ya kuku, kuna ng'ombe na miradi mingine. Je, Mheshimiwa Waziri huu ndiyo utawala bora? *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Moza Saidy, tunakushukuru sana kwa uchangiaji wako. Sasa kama nilivyosema ni zamu ya Mheshimiwa Vullu atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kujikita kwenye hoja ya msingi ambayo ndiyo imewekwa mezani. Naomba nianze na suala la watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya watumishi, ajira zimekuwa haba na tunashukuru Serikali kama ilivyosema imeongeza ajira kwa mfano Walimu, tumepata idadi ya Walimu 28,000. Naishukuru Serikali imesema hivi karibuni kunatarajiwa kuajiriwa watu zaidi 15,000 lakini je, watumishi hao watakaoajiriwa wameandaliwa namna gani? Kwa mfano, wanaopelekwa kwenye Kata, kwenye vijiji, hawana

nyumba za kuishi. Ni vyema basi bajeti ikaongezwa ili watu hawa waweze kupata nyumba bora za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika suala la mishahara. Kiwango cha mishahara ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya Mtanzania kwa sasa. Nauli za mabasi zinapanda kila kunapokucha, unga unapanda bei kila kunapokucha lakini bado kuna haja ya kuangalia ni vipi tunaweza tukawasaidia hawa watu wanaoajiriwa, ndiyo kwanza wametoka Chuoni, hana hata kitanda, hana hata sufuria, ni vyema tukaangalia ni vipi tunawasaidia. Wengi wanaokwenda vijijini wanakumbana na mazingira magumu, lakini ni vizuri tukaangalia ni vipi tunawasaidia katika kuwawekea mazingira yaliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata masikitiko makubwa sana, humu ndani sisi ndiyo viongozi na viongozi sisi ndio tunaotakiwa tukitoka hapa na hata tukiwa humu ndani tuzungumzie suala la amani lakini cha kushangaza wenyewe humu ndani hatuna amani, tutaishi vipi? Wananchi tunaowaongoza huko nje wanatuangalia vipi? Cha ajabu tukitoka hapo kwenye mlango, tunashikana, tunapeana mikono, mimi naomba tuwe na umakini kama tunataka kuzungumza amani**,** tulenge wananchi wetu tunataka tuwaambie kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sidhani kama nchi hii ina udini, sina uhakika. Mimi ni Muislam, ni kiongozi niliyechaguliwa na watu na walionichagua ni Wakristo na Wapagani, sasa mnaniambiaje kuna udini? Mimi hapo ndiyo ninashindwa kuelewa! Hakuna Mkristo humu ndani ambaye hajachaguliwa na Muislam. Hakuna Muislam aliyekuwa humu ndani ambaye hajachaguliwa na Mkristo. Niambieni Jimbo gani wanaishi Waislam watupu, niambieni Jimbo gani wanaishi Wapagani watupu, niambieni Jimboni gani wanaishi Wakristo watupu? Tukishalijua hilo, haya matatizo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tumeishi Tanzania hii, suala la kuchinja limetoka wapi, anachinja Muislam anayeuza ni Mkristo tatizo nini? Si wewe unayekula ndiyo unajua unakwenda kununua nini? Wewe unayepika, unapika unajua unakula na Wakristo, unakula na Waislam, unajua nani aje achinje ili uweze kushiriki naye katika kula. Sasa sioni kwa nini, tunavyozidi kupiga kelele jamani ndiyo tunazidi kuharibu hii amani yetu. Tusiharibu hii nchi, nchi hii ni kisiwa cha amani, cha kuigwa kwa Taifa nzima, Bara la Afrika hata Mabara ya Ulaya, hii ndiyo sehemu mojawapo ya kuigwa mfano. Sasa tuombe jamani, kuna Wachungaji humu ndani, kuna Masheikhe humu, bahati nzuri mpaka Wachungaji wanawake tunao humu ndani tunataka nini? Tunapofika humu ndani tuzungumze amani inayotuhusu sisi na wananchi wetu, tusizungumze amani itakayotubomoa huko nje. Tutengeneze mazingira ya kuwapooza wananchi wetu. Kama nyie mnaona Rais ana udini, Rais hana udini, Rais angekuwa na udini tunangeona kwenye idadi ya viongozi wake. Asingesimama jukwaani akahubiri yeye anaonewa na baadhi wa viongozi dini, tusipewe cheo kisicho chake. Tuzungumze yale ambayo tunayoona na tunayatenda kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba tuliangalie suala hili.

**MBUNGE FULANI:** Itikafu!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Eti watu hapa wananiambia Itikafu. Kweli Rais ni Muislam na Waislam walimsomea Itikafu kwa maelezo yake kwenye hotuba ya mwezi uliopita. Sasa yeye Muislam, Waislam wenzie wapo na sina hakika nalo, lakini mwenyewe Rais amelisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe, tupate siku maalum, waje viongozi wa dini zote waongee na sisi labda tukitoka hapa tutahubiri vizuri suala la amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapata semina za aina mbalimbali, juzi tulikuwa na semina ya Albino, tuliona

jinsi tulivyoguswa, tumekuwa sisi wanawake na semina ya akinamama tumeona tulivyoguswa. Sasa ni vyema katika suala hili la amani, mimi ninaliogopa sana kwa sababu ukiwa huna amani hata njia uliyokuwa unapita hupiti unageuza kwa sababu umeshaona pale kuna adui yako. Ukishakuwa huna amani, hata kama ulikuwa unakwenda hospitali unaogopa, nyie wenyewe mmesema hapa, maneno mengine mimi sitaki kuyanukuu. Sasa niombe utuweke utaratibu, waje viongozi wa dini tena kwa pamoja, waje waongee na sisi, watueleze amani inavyosema ili na sisi twende kwa mustakabali wa amani tuliyokabidhiwa na viongozi waliopita kabla yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye suala la utumishi. Askari wetu wanafanya kazi nzuri sana, kuanzia Kitengo cha Usalama wa Taifa, Usalama Barabarani na Usalama wa Raia lakini niombe Askari hao wanaofanya kazi za usalama watengenezewe mazingira mazuri ya kazi, wapewe posho zake kwa wakati, wapewe vyombo vya usafiri vinavyostahili, magari hayapo basi hata pikipiki, wapeni waweze kufukuzana na sisi. Wale wanaosimama barabarani na toshi, naomba suala hili liangaliwe, wanasimama katika maeneo ambayo siyo mazuri, wanategemea kivuli cha miti, hawana sehemu ya kujihifadhi. Kwa hiyo, ni muhimu Serikali ikaangalia hawa watu wakapatiwa vifaa na vitendea kazi na posho zinazostahili ili waweze kufanya kazi yao kwa umakini na uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vullu kwa kujielekeze kwenye hoja. Uchangiaji wa namna hii kwa kweli tunaukaribisha sana. Mheshimiwa Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Mabumba.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA***:* Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kukuomba mapema kwa sababu sisi wengine tuna bahati mbaya, tukishaanza kuongea wengine utakuta roho zinawaruka na tusiweze kufika mpaka mwisho, lakini niwaahidi tu mimi leo maneno yangu ni ya kawaida, ya taratibu ila nataka kufikisha ujumbe kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nitaomba unilinde mpaka mwisho, mwenye nia ya kufanya *interruption* asubiri mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hali ambayo inaendelea sasa hivi kwenye nchi hii ya kikundi cha watu wachache hususani wapinzani na hasa CHADEMA kuona kwamba kila jambo wanalolifikiria wao, kila jambo wanalolizungumza wao, kila jambo wanalolifikiria wao ni sawa basi Watanzania wote lazima tuseme hilo ndilo sawa. Ndiyo maana huwezi kushangaa kuona mtu akatamka kwamba Serikali haina weledi, Serikali inakosea na kwa kweli mtu ili aweze kufahamu uweledi, ni lazima mwenyewe kwanza awe mweledi. Huwezi kumchukua mtoto wa darasa la kwanza, halafu ukamwambia afanye mtihani wa *form four* au wa Chuo Kikuu. Kwa hiyo, inawezekana kwa sababu wao uwezo wao kuona yale tunayoyafikiria wenzao bado upo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo basi, utakuta hapa tunakaa tu, tunazungumza hili, linatokea lile lakini ni kwa sababu ya uelewe mdogo na hii ni kwa sababu bado wanakua kisiasa, ni sawasawa na tuna haki ya kuwavumilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashtushwa mimi sana, sasa hivi kuna hali ya kuwadanganya wananchi, kuwadanganya viongozi wa dini, sisi wanasiasa tunajaribu kuwagawa kwa sababu ya kufikiria mwaka 2015 tuweze kuwapata, tunatafuta huruma zao. Unaenda kwa viongozi wa dini kwa mfano ya Kikristo, unaenda kulia, unajua sisi wanatwambia ni Chama cha Kikristo ili kupata *sympathy* kutoka kwa Wakristo. Wanaenda kwa Waislam wanawaambia Wakristo wanasema hivi na hivi ili kupata *sympathy* kutoka kwa Waislam hapana, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, CHADEMA siyo Wakristo hata siku moja, CHADEMA siyo Chama cha Kikristo, CHADEMA ni chama...

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Kwa sababu kama ni Wakrsito hata mimi ni Mkristo kwa nini sipo CHADEMA nipo CCM? *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Kwa mazingira hayo, mimi najaribu kuona jinsi ambavyo tunatafuta mbinu kuwashawishi wananchi .... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya samahani kidogo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Nilijua ataruka huyu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip,* mimi ningekuomba sana pamoja na Wabunge wengine tusipokuwa na uvumilivu hata kidogo, hatuwezi kufika mwisho. Tangu tumeanza kipindi hiki, Mheshimiwa umeshasimama zaidi ya mara kumi, uwe na uvumilivu. Haya mpe taarifa Mheshimiwa Mbunge lakini ningewaomba uvumilivu itatusaidia sana. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa msemaji aliyekaa chini kwamba, ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi walioanzisha madai ya udini wakasema *CUF* ni chama cha Waislam wenyewe siasa kali, Ndugu Omar Mahita akaonyesha mapanga hadharani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu...

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa tu.

**NAIBU SPIKA:** *No, no*. Samahani kidogo, kaa tu kidogo ili twende vizuri. Alichosema Mheshimiwa Manyanya ni kwamba CHADEMA siyo Chama cha Kikristo na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, taarifa yako ijielekeze katika hilo maana wewe unaanza kuchangia vitu vingine na una dakika zako 10 utapata. Unaanza kuchangia mambo mengine ambayo wala yule hajasema. Ndiyo maana nasema kama unamsahihisha taarifa mpe katika lile alilosema.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa hicho hicho alichosema kwamba hii anayosema sasa hivi hailingani na matamshi ya viongozi wa Chama chake, haijawahi kulingana na matamshi ya Chama chake, CUF chama cha Waislam, CHADEMA chama cha Wakatoliki...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kweli unanivuruga tu bila sababu, anachozungumza Mbunge ni mawazo yake si mawazo ya Chama chake. Kwa hiyo, akosolewa kwa yale anayoyasema yeye. Endelea Mheshimiwa Manyanya. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilijua wataitetea kwa nguvu sana hoja hiyo, wanapenda kuitwa kwamba Chama chao ni cha Wakristo si kweli. Mimi ni Mkristo na nipo CCM na hili nawaomba wale ambao wana imani sawa na mimi, tusibaguliwe kwa kujidai Chama fulani ni Chama cha imani fulani. Hiyo ni kutafuta kura zao kiujanja ujanja. Hiyo ni kutafuta *sympathy*, kutafuta kuonewa huruma kiujanja ujanja, hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hili suala la kuchinja, niwaulize wenzangu mliopo humu ndani, hasa wale wenye imani sawa na mimi, kwani siku zote mimi mpaka leo nafikia umri huu wa nusu karne, hiyo imani ya nani kachinja

haikuwepo? Kwa nini tunakuja kuambiwa leo? Kwani watu wamekuwa hawachinji? Kwa nini leo ukitaka kuchinja mpaka umwambie mtu unaona sasa leo nachinja, *why*? Tunajaribu kutumia hali ya ndugu zangu, wananchi wenzetu kutokuelewa na sisi kuwachanganya hapana, hapana, hatuko *fair*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tukiwa kwenye kongomano la wanawake, kuna Mbunge mmoja, upande wa wenzetu CHADEMA, alidiriki kuwaambia wale akinamama kwamba sisi mle kazi yetu ni kuachilia uongo. Kwa mfano, leo tumeongea jengo limetoboka, wanataka kuchukua shilingi bilioni sita kukarabati ukumbi na ikawa ni *discussion* kwa wale wanawake, lakini wanauelewa, wanawake wakasema kwamba kwa nini...

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sasa hivi asipewe nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Nimemwomba Mheshimiwa Abwao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu ningekuomba tena kwa mara nyingine uwe na uvumilivu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Kwa nini huwi mvumilivu?

**NAIBU SPIKA:** Nimemwona Mheshimiwa Chiku Abwao amesimama.

**TAARIFA**

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mimi naomba kumpa taarifa msemaji anayesema hivi sasa. Kama hakifahamu vizuri Chama cha

Demokrasia na Maendeleo hana sababu ya kukitilia maneno hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Demokrasia na Maendeleo hakina udini na yeye mwenyewe anajua hilo. Mimi mwenyewe ni Muislam na tupo watu chungu nzima na Wapagani wapo kwenye chama, kwa nini anapenda kusema maneno ambayo hayana ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, sijawahi kukaa katika kikao chochote tukajadili mambo ya udini na hatujawahi kusema sisi chama chetu ni cha Kikristo ama cha Kiislam. Namwomba achangie hoja iliyopo Mezani. Asianze kuokota maneno na kukichafua Chama cha Demokrasia na Maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Chiku Abwao. Mheshimiwa Manyanya unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi namshukuru anaungana na maneno yangu kwamba CHADEMA sio chama cha Kikristo. Ndivyo nilivyosema. Kwa sababu nafahamu hata Mheshimiwa Chiku yuko huko na ni Muislam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachokataa ni maneno ambayo yanajaribu kuwavuta watu wa imani fulani ili waweze kuwahurumia na kuwapa upendo wa kiujanjaujanja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye masuala ya usalama yanayozungumzwa. Kuna wakati nilichangia ikaleta tatizo kubwa sana na ndiyo maana siku hizi huwa nanyamazanyamaza kidogo, unajua silaha ya msaada haitakiwi kutumika kila wakati. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa kwa sababu wenzetu wanajifanya wana taarifa nyingi sana za usalama, wana taarifa nyingi sana ndani ya Serikali, sijui limetoka hili Ikulu, nashindwa kuelewa kidogo. Kama ni ukweli,

basi Usalama wa Taifa wana haki ya kujilaumu wenyewe. Inawezekana wana mahusiano ya kiajabuajabu ambayo mengine yanatoa taarifa zisizo za kweli au kwa sababu ya kuchekacheka pamoja wanawaona kama wenzao, lakini ninavyofahamu, dola ina mihimili yake mikuu mitatu, Bunge, Serikali na Mahakama na kila mhimili utatenda kwa kuji-*balance,* hakuna mhimili utakaotaka kuzidi mihimili mwingine. Kwa misingi hiyo, nasema Serikali mchukue nafasi yenu. Serikali ichukue nafasi yake, ndiyo maana sasa hivi huwezi kushangaa mtu anakuja tu anasema hapa ondoa, unajua Mkuu wa Mkoa hafai, unajua Mkuu wa Wilaya hatakiwi kwa sababu watu hawajui mipaka yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naagiza, kwanza nimsifu sana na kumpongeza Mheshimiwa Mbowe alivyokuja Rukwa kwa sababu niliagiza vyombo, safari hii nikisikia tusi kwa Mheshimiwa Rais, nikisikia tusi kwangu mkamateni muwekeni ndani. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Kwa bahati nzuri hakufanya hivyo. Ameongea na wananchi aliokuwa ameenda kuongea nao kwa uzuri kama ambavyo chama chake kinavyotakiwa kifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa misingi hiyo, mimi mtazamo wangu nitasimamia hayo na kwa kweli wananchi wanatuelewa jinsi ambavyo tunajaribu kuwarubuni hapa kwa maneno yasiyo ya haki na ya ukweli kwa kujidai kuzuia hata vyombo vya usalama na ulinzi visichukue hatua. Kwa mfano, mtu anavyokimbia zake anaenda mpaka Kituo cha Polisi akatishia au maandamano yasiyopangwa kihalali halafu aseme Polisi wanatumia nguvu kubwa, unataka Polisi awe na kirungu halafu wakati wewe una watu ambao wana mawe na mambo mengine. Mimi nimesema hapana. Polisi wamepewa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, watumie madaraka na haki zao zote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya, nakushukuru sana na ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Sylivester Mabumba atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mchango wangu unaelekea katika mambo yafuatayo kwanza nitaongelea TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuambia TAKUKURU imeshughulikia tuhuma 2,936 lakini kati ya tuhuma hizo, ni tuhuma 165 tu ambazo zimefunguliwa majalada na kupelekwa Mahakamani. Sasa nauliza, kwa mwenendo huu wa kwamba watuhumiwa ni wengi lakini utendaji wa kazi unasuasua, mimi nina wasiwasi na umadhubuti wa Taasisi hii ama kuna tatizo Ofisi ya *DDP* ambayo haipeleki kesi hizi Mahakamani wakati TAKUKURU wao wameshafanya kazi yao. Napenda Mheshimiwa Waziri akija hapa aniambie, ni muda gani au wastani wa siku ngapi au miaka mingapi wanahitaji kufanya uchunguzi kwa tuhuma moja hata miaka yote hii wameweza kushughulikia tuhuma 165 tu kati ya 2,936. Kusuasua kwao kunapoteza imani kwa taasisi hizi ambazo zinatumia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine wametuambia kwamba TAKUKURU waliweza kuokoa shilingi 4,313,723,189.55. Kati ya hizo, shilingi 3,000,000,000 zilikuwa ni mishahara hewa. Sasa napenda kujua, Mheshimiwa Waziri atuambie, hawa ambao walifanya mchezo huu mchafu wa mshahara hewa shilingi bilioni 3.881, ni wangapi hasa walichukuliwa hatua na ni hatua zipi? Kutuambia tu kwamba uliokoa fedha na ukashindwa kutuambia wahusika wa mchezo huo mchafu, haisaidii. Bunge hili lingependa kuwajua hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie pia habari ya MKURABITA ambao tumeambiwa kwamba umeingia awamu ya tatu. Napenda niulize tu swali moja dogo la msingi sana. Mheshimiwa Waziri atuambie, ni mafanikio mangapi hata machache tu ambayo MKURABITA toka imeasisiwa imeweza kulipatia Taifa hili. Kwa sababu wanyonge bado mali zao hazitambuliki na kwa sababu hiyo hawawezi kukopesheka kwa sababu hawana dhamana yoyote. Tungetarajia MKURABITA iwasaidie kupata hati ambapo mali zao zingetambulika kisheria na hivyo kuweza kukopesheka. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie kwamba MKURABITA toka wameasisiwa wameleta mafanikio moja, mbili au tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda nizungumzie *TASAF* hasa Jimbo langu la Dole. *TASAF* kama tunavyojua ni mradi ambao unatekelezwa nchi nzima, Tanzania Bara na Visiwani. Kwenye Jimbo la Dole tumeambiwa sasa hivi wameingia awamu ya tatu iliyoanza Agosti, 2012 na wataendelea nayo kwa miaka 10. Ninavyojua Jimboni kwangu, ni mradi mmoja tu umeweza kutekelezwa katika Shehiya ya Bungusudi yenye thamani ya shilingi milioni 385 hivi lakini ninavyojua pia ni maombi mengi sana yamewasilishwa kwenye Ofisi ya *TASAF* kupitia kule Zanzibar lakini hadi leo hii majibu yake hayaeleweki. Kwa hiyo, ningependa kujua kama tuna lengo la kusaidia wananchi wetu kujikwamua na umaskini kutokana na mradi huu wa *TASAF* basi ni vyema maombi yanapopelekwa yashughulikiwe kwa haraka ili lile lengo lililokusudiwa la kuwasaidia wananchi wetu waondokane na umaskini liweze kufikiwa. Kwa sababu kila Waziri anayesimama hapa anasema bajeti yake imezingatia MKUKUTA, MDG, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano lakini tutafikiaje kama miradi hii iliyowekwa kusadia kutekeleza programu hizi, haiendi kwa kasi na haiwaangalii watu wote kwa wakati mmoja na hivyo hatuwezi kufikia malengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nijielekeze kwenye Sekretarieti ya Ajira. Hapa pia nina swali dogo la msingi. Tunajua tuna wahitimu wengi sana wanahitimu toka

Vyuo Vikuu vya Umma na vya binafsi hapa nchini lakini wanazurura mitaani kwa kukosa ajira wakati kuna watu wameajiriwa kwa mikataba. Naomba nijue, ni vigezo vipi ambavyo vinazingatiwa kwamba huyu ni muhimu sana hata apewe ajira ya mkataba na vijana wetu wakaendelea kuzunguka mitaani hawana ajira na mwisho tunawashawishi kujiingiza katika matendo mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie hii Dira ya Taifa. Dira ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, naona ni hadithi njema lakini bila kuwekeza katika utafiti, hatuwezi kutekeleza dira hii ya Taifa. Tutafika mwaka 2025 bila ya mafanikio makubwa ambayo mipango hii imejiwekea. Napenda kujua, Taifa letu limetenga kiwango gani cha asilimia ya bajeti ya Taifa kwenye utafiti? Kwa sababu Vyuo Vikuu vyetu, Vitengo vya Utafiti havina fedha za kutosha matokeo yake wasomi Maprofesa wanakaa bila kufanya utafiti ambao utafiti wao ungesaidia Taifa hili. Hatuwezi kuendelea bila ya kuwekeza katika utafiti. Tutatamani tu Mataifa ya Ulaya ambayo yamewekeza zaidi katika utafiti ndiyo maana yameweza kufahamu vipaumbele halisi vya Taifa katika Mataifa yao lakini vilevile wakaweza kushawishi fedha za Taifa kuelekezwa katika vipaumbele hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Taifa letu lione umuhimu wa sekta ya utafiti. Ni aibu leo Tanzania haiwezi kuwawezesha Watafiti wakarahisisha hata kilimo ambacho tunasema Kilimo Kwanza. Naweza kuungana na Mheshimiwa Kessy anayesema Kilimo Mwisho... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu unazalisha kisha unazuiliwa usiuze mazao yako nje ya nchi, yanabaki kuoza mashambani, huyu mkulima atafanya nini? Maeneo yanayolima mpunga hapa wamesema, mpunga wa mwaka jana upo, hauna masoko. Wananchi hawawezi kuuza mazao yao kwa sababu wafanyabiashara wameruhusiwa kuingiza vyakula kwa bei nafuu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabumba.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Kwa hiyo, nilikuwa naomba haya niliyoyasema nisaidiwe, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tundu Lissu atafuatiwa na Mheshimiwa Laizer. Mheshimiwa Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mambo mawili tu kwa sababu sitapata muda wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kulizungumzia linahusu mchakato wa kupatikana kwa Katiba Mpya na vilevile masuala yanayohusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wiki iliyopita, Wajumbe mbalimbali wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wamelalamikia utaratibu uliowekwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba wa kutengeneza Mwongozo wa uundaji wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ambao kwa kuuangalia tu, umetengenezwa kuhakikisha kwamba ni Wana-CCM peke yao ndio watakaoenda kwenye Mabaraza hayo ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wajumbe wengi wa CCM ambao wamehoji kauli zetu na wengine mpaka jana wamezungumzia mfano Mheshimiwa Makamba. Leo nimepata ushahidi unaothibitisha hicho ambacho tumekisema kwamba utaratibu wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, ni kuhakikisha kwamba Mabaraza haya yatakuwa ni Mabaraza ya CCM na kwa sababu yatakuwa ni Mabaraza ya CCM, Katiba itakayotokana na utaratibu huo itakuwa ni ya Ki-CCM, CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio tu kwamba Wajumbe waliochaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wamefutwa katika ngazi ya *Ward C* zinazodhibitiwa na CCM, hata wachache ambao wamefanikiwa kupita hilo chekecheke la *Ward C* za CCM, bado wanafuatwa huko waliko ili na wao waondolewe. Ushahidi ninaouzungumzia hapa, ni ushahidi uliotoka Arusha Mjini. Nina barua hapa iliyoandikwa na Katibu wa CCM wa Wilaya ya Arusha Mjini anaitwa Allan Kingazi. iliyoandikwa tarehe 8 Aprili, 2013 kama wiki moja iliyopita, kichwa chake cha habari kinasema 'Afisa Mtendaji wa Kata ya Sombetini kukiuka kanuni za Uchaguzi wa Muundo wa Mabaraza ya Kikatiba, amnyima Mwenyekiti wa Mtaa kupiga kura, pia amruhusu raia wa Burundi kuingia kwenye Baraza la Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayezungumziwa hapa anaitwa Beatus Kipea, anatoka Jimbo la Muhambwe, Jimbo la Mheshimiwa Mkosamali. Ni raia wa Tanzania, ameshinda kwa kura nyingi kuingia kwenye Baraza la Katiba la Wilaya ya Arusha Mjini. Baada ya hapo, Wana-CCM wa Kata ya Sombetini, wakiongozwa na mtu anaitwa Mussa Khamis Mkanga, tulimshinda kwenye kesi ya Mheshimiwa Lema, wamepeleka maneno ya uongo kwa Ma-CCM wenzao ikaandikwa barua hii na hii barua ameandikiwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha halafu walionakiliwa kuonyesha mchezo gani unaendelea, mtu wa kwanza kunakiliwa ni Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Bwana Abdrahman Kinana, wa pili Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, wa tatu Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Mjumbe wa vikao vyote vya CCM Mkoa wa Arusha, wa nne Afisa Usalama wa Taifa wa Wilaya ndio hawa tunaowalalamikia hapo wanateka watu nyara, mwingine Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Jiji, walee na wa mwisho Afisa Uhamiaji wa Mkoa wa Arusha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya barua hii, Afisa Uhamiaji wa Mkoa anaitwa Gowele amemwandikia Beatus Kipea barua inayomtaka kufika Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Arusha bila kukosa wala kutuma mwakilishi. Hii barua imenakiliwa moja, Afisa Mtendaji Kata ya Sombetini Arusha, Mwenyekiti wa Mtaa Kirika A Sombetini, Balozi wa Mtaa wa Zurich Sombetini na Balozi ni wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapozungumza kwamba utaratibu wa kupata Katiba Mpya ya nchi yetu umetekwa nyara kutokana na Mwongozo wa uundaji wa Mabaraza unaohakikisha Mabaraza yatakuwa ya CCM, hii ndiyo maana yake na watu wasiokuwa wana-CCM wameenguliwa nchi nzima, nchi nzima. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**NAIBU SPIKA:** Naomba tumsikilize.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya aina hii ndiyo yanayotumbukiza Mataifa kwenye maasi na kwenye machafuko. Uchakachuaji wa aina hii ndio unaleta vita. Ndiyo maana tumesema na naomba niurudie tena, kwa sababu Tume ya Katiba imeandaa mchakato utakaorudisha Katiba ya Ki-CCM, sisi hatumo na tutawaambia Watanzania wanaotusikilia wasiwemo. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa rafiki yangu Tundu Lissu anaposema kwamba wameenguliwa nchi nzima, naomba nimpe taarifa kwamba Kata ya Namsimo iliyoko Jimbo la Mwibara aliyekuwa mgombea wa Udiwani wakati wa uchaguzi ndugu Baltazar Meso, safari hii amegombea kuingia kwenye Baraza la Kata na wapiga kura walikuwa ni Wenyeviti wote wa CCM kwenye vijiji vyote na kwa kauli moja wamemchagua kuingia kwenye Baraza. Kwa hiyo, asiseme kwamba nchi nzima. *(Makofi)*

Nilikuwa nakupa taarifa tu rafiki yangu Tundu Lissu ili tusije tukapotosha umma. Anaitwa Baltazar Meso, ni wa CHADEMA na kura zote zile zilikuwa ni za Wenyeviti wanaotokana na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** CCM huyo!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Tundu Lissu umeikubali?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Siku zote huwa namshukuru Mheshimiwa Kangi Lugola kwa taarifa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba, taarifa ambazo tumepokea nchi nzima watu wetu na watu wasiokuwa wana-CCM wameenguliwa katika Mabaraza ya Wilaya kwenye *Ward C* pamoja na kwamba walichaguliwa na wananchi kwa kura nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili naomba Watanzania watuelewe na Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa zamani, Mheshimiwa Warioba ituelewe. Kwa sababu mchakato unavurugwa kiasi hiki tutawaambia wananchi wetu watuunge mkono, tusikubali Katiba mpya kuchakachuliwa namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye suala la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Sekretarieti hii iliundwa mwaka 1995, wakati Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilipotungwa na Bunge hili Tukufu. Leo hii Sekretarieti hii ina miaka karibu 30, kama hesabu zangu ziko sawasawa, ina miaka mingi tangu mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 1995, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haijawahi kupata viongozi wa umma hata mmoja na hatia ya kukiuka maadili ya viongozi wa umma. Walikuja kwenye Kamati yetu, nikawaambia tupeni jina hata moja la mtu ambaye amepatikana na hatia ya wizi wa mali ya umma ya uharibifu wa nchi, hawana hata mmoja. Maana yake ni kwamba, aidha, nchi hii haina tatizo la ukosefu wa maadili ya viongozi na kwa maana hiyo, sisi ni Taifa la watakatifu au vinginevyo Sekretarieti hii haina kazi, inatakiwa ivunjwe, tuache kuchezea fedha umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi ambacho Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haijapata kiongozi hata mmoja mwenye hatia, nchi hii imeshuhudia Waziri Mkuu akilazimishwa kujiuzulu Bungeni humu kwa tuhuma za ufisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki hiki kimeshuhudia Mawaziri kadhaa wakilazimishwa kujiuzulu kwa tuhuma za ufisadi. Bunge hili limeletewa ushahidi wa Rais akifanya biashara Ikulu, limeletewa taarifa ya Rais na marafiki zake Mawaziri wanakichukua mali ya Taifa mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira na kuutwaa kuwa mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili limeshuhudia uchafu mkubwa wa viongozi wa Serikali. Viongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wana utajiri wa kutisha. Wameficha mabilioni ya fedha Uswisi, lakini Sekretarieti ya Maadili ya Umma haijasikia wala kuona shetani yoyote. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Bahati mbaya umechelewa hiyo taarifa, ameshakaa chini.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa nilisimama tangu mwanzo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Rage ajiandae.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niseme machache na kwanza nakupa pole. Nakupa pole sana kwa sababu hicho Kiti kwa kweli kimewaka moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kusema machache, niseme kwamba, ndugu zangu Wabunge, Bunge hili tumegeuza kwamba sio Bunge tena ila umekuwa uwanja wa mapambano. Wala sio Chama kimoja ni sisi Wabunge wote na tumekiuka utaratibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni sio mahali pa kuzomeana, kwa sababu tukianza kuzomeana ni kwamba tutaanza kupandisha jazba, hata ule Uheshimiwa hatustahili tena kuitwa Waheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kukumbuka, hivi ni chombo kipi kinaweza kujadili au Bunge litajadiliwa na nani kama Wabunge wakikiuka utaratibu. Kanuni tumejiwekea lakini tunavunja. Hivi Mbunge mwenzako anaongea unaanza kumzomea unafikiria nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoanza Bunge la Vyama Vingi tulikuwa na Wabunge wa Vyama Vingi mahiri sana. Mheshimiwa Mbowe alikuwepo, alikuwepo Mheshimiwa Lamwai, alikuwepo Mheshimiwa Lyatonga Mrema, alikuwepo Marando, Mheshimiwa Mbatia, lakini hatujawahi kufikia kiwango hiki. Naomba ndugu zangu, kwa sababu tunazungumzia chombo fulani kivunjwe, hata hiki cha kwenu kinastahili kivunjwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumekikuka utaratibu na naomba...

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sugu, jamani nimewaombeni sana, tuwe na uvumilivu, kila mmoja apate haki ya kuchangia. Ikiwa kila anayechangia, taarifa, sijui nini.

Haya, Mheshimiwa Sugu (Mheshimiwa Joseph Mbilinyi) taarifa!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nampa taarifa tu kwamba, Bunge hilo analolizungumzia walilokuwepo akina Mheshimiwa Mbowe na wengine, halikuwa na watu pia kwa upande wa Chama cha Mapinduzi kama Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Nkamia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kwa vyovyote vile huku ni kupoteza muda na kutaka kuleta mifarakano ambayo haina sababu hata kidogo. Mheshimiwa Lekule Laizer endelea!

Mheshimiwa Nkamia, naomba sana msamehe bure Mheshimiwa Sugu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hizi taarifa tunazopeana ndizo zinapoteza muda na inafaa taarifa aikubali mtu anayezungumza. Hicho kipengele kiondolewe kabisa na sio kila mtu asimame akupe taarifa na kukutoa katika hotuba yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopenda kuzungumza ni kwamba, tumeichafua hali ya Bunge mpaka limedharaulika nchi nzima. Ndugu zangu tunakuja, tunakaa hapa tunatumia fedha za wapiga kura wetu bila kufanya chochote, tukicheza hapa, kitu ambacho hakina faida kwa mtu yoyote, tunakuja kusema chama fulani cha kidini, hivi wananchi ambao wako kwenye mkutano wa CHADEMA nchi nzima ni Wakristo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wananchi wote, hata hapa Bungeni tuko mchanganyiko. Kuna Wakristo, kuna Waislam kuna wengine ambao hawana dini humu. Kuna mwingine ambaye hajawahi kwenda Kanisani wala Msikitini, huyo ni wa wapi?

**MBUNGE FULANI:** Mpagani!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mko hapa hapa Bungeni. Naomba ndugu zangu na viongozi wa Vyama vyote, waendee kukaa na kujadili matatizo haya, wa CCM wakae watafute utaratibu ili turejee kwenye mstari mzuri. CHADEMA wakae, *CUF* wakae, tuje tuangalie, kama tutashindwa kuendelea Bunge hili livunjwe, imekuwa ni aibu tupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati mwingine Serikali inakaa kimya kwa sababu ya majukumu yake na wakati mwingine naona hata na ninyi mmeanza kuogopa ili watu wasipigane hapa ndani. Kwa sababu mwenzako akikuzomea na tunazomeana kwa mambo ambayo hayana msingi. Naomba Serikali wakati mwingine tukifanya mambo ambayo hayastahili msinyamaze kimya, mseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu kuwaambia wenzangu, turudi kwenye mstari, Bunge liheshimiwe, kwa sababu lisipoheshimiwa halitakuwa Bunge. Ni hayo tu niliyotaka kuyaongea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer. Kwa watu wowote au jamii yoyote yenye busara huwa ina wazee na Mheshimiwa Laizer ni miongoni mwa Wabunge *Veteran* ambao huwa tunawaita Ma-*senator,* maana kwa hakika kuna Wabunge wengine ni wapita njia, kwa maana kwamba amekuja hapa, lakini miaka mitano lazima aondoke tu. Sasa huyo utamwita ni Mbunge.

Uliza Mheshimiwa Lekule Laizer amekaa hapa miaka mingapi? Sasa wengine muwe mnakaa nao wazee kama hawa na kuongea nao, unapata kidogo. Akina Ndugai hapa tuna kipindi cha tatu, si haba!

Kwa hiyo, hili somo alilolitoa hapa ni *lecture* kwa Wabunge wote, yapo mambo ambayo mnafanya hapa 2015 baadhi yenu yatawagharimu kweli kweli. Mheshimiwa Mnyika atafuatiwa na Mheshimiwa Rage.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kuchangia kuhusiana na hotuba ya

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Uhusiano na Uratibu, hotuba ambayo inahusu ofisi nyeti katika nchi yetu kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu pamoja na ubovu wake, Ibara ya 33, inasema Rais ndiye Mkuu wa Nchi, kiongozi wa shughuli za Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Kwa hiyo, watumishi wote wa umma kwa Ibara ya 35 wanafanya kazi kwa niaba ya Rais. Kwa hiyo, mjadala huu ni mjadala nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na aya ya 14 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambapo sehemu ya tatu, taasisi hii imetoa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri taarifa ya kuwa imekwishakamilisha majadala yanayohusu tuhuma nne za rushwa kubwakubwa *(grand corruption)* na kwamba inafikishwa kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kupelekwa Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimechoka sana na hizi lugha zinazoandikwa kila mwaka kwenye hotuba zetu. Maneno yanajirudia yale yale, sijui majalada ya rushwa kubwa yameshachunguzwa, yatapelekwa Mahakamani lakini hakuna yanayopelekwa Mahakamani kwa hatua thabiti kuweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini TAKUKURU, Ofisi ya *DPP* na vyombo vingine, vinafikia hatua hii ya kushindwa kuchukua hatua ya rushwa kubwa kubwa kwa sababu ya udhaifu wa Ofisi ya Rais kwenye kusimamia vyombo hivi vya kiutendaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mingine iliyopita 15 Septemba, 2007, iliwahi kusomwa orodha ya mafisadi hapa nchini mwetu maarufu kama *list of shame*. Kishindo cha orodha ile ambayo ilisomwa nje ya Bunge kilihamia vile vile Bungeni ambako kuliundwa Tume mbalimbali na Kamati mbalimbali na maazimio mbalimbali yalisomwa Bungeni, lakini Waheshimiwa Wabunge tujiulize toka 2007 na 2009 yalipofanyika maamuzi mbalimbali ndani ya Bunge hili ni kwa nini mpaka leo watuhumiwa wa kashfa kubwa kama za

Kagoda, kama za Meremeta na kashfa mbalimbali hawajafikishwa Mahakamani mpaka leo. Asimame Mbunge mmoja au Waziri mmoja aseme kama hali hii haichangiwi na Ofisi ya Rais katika kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu miaka michache iliyopita Bunge hili liliwahi kuhutubiwa na hotuba iliyohusu masuala ya wizi wa *EPA* ile hotuba nimeingia Bungeni nimejaribu kuitafuta *Hansard* ya Kumbukumbu za Bunge ya Hotuba ile ya Rais ya wakati ule mpaka leo hotuba ile ilipelekwa Ikulu, sijui kwenda kukarabatiwa au kuchakachuliwa, mpaka leo hotuba haipo kwa sababu kuna mambo yalisemwa mle ambayo kimsingi yanajenga msingi wa kukwaza uwajibikaji kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu hatua zikachukuliwa na ni muhimu Idara ya Usalama wa Taifa na nasikitika kwa mujibu wa *instrument* ambayo Mheshimiwa Rais alitoa kwa Mawaziri, Idara ya Usalama wa Taifa, iko chini ya Wizara ya Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesoma kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Wassira, hakuna mahali popote amezungumza kuhusu utendaji wa Ofisi hii ya Idara ya Usalama wa Taifa. Mheshimiwa Lukuvi anatikisa kichwa, lakini hata kama ingekuwa chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma hakuna mahali popote ambapo Mheshimiwa Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma ameelezea kuhusu *role* ya Usalama wa Taifa kwenye kunusuru usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama haya si ajabu kuwa na usalama ambao umegawanyika vipande vipande. Kipande kimoja kinafanya kazi ya kulinda usalama wa mafisadi, kipande kingine kidogo kinabaki kikitetea usalama na kutoa hata taarifa kwa ajili ya kuisaidia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ni muhimu tukayajadili kama Watanzania na tukayajadili kwa uwazi sana kwa sababu wengine sisi ni wahanga wa huu mfumo. Matendo yanayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, hayawaathiri tu watu tunaowaona mtaani, iwe ni watu wanaondikwa kama akina Kibanda, Ulimboka na wengine. Matendo haya yanapanua wigo mpaka yanaingia kwenye kuwalenga Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna shaka Usalama wa Taifa ukiwa usalama wa nchi, kila mtu ataheshimu Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa unaolinda mafisadi, haupaswi kuheshimiwa na raia yoyote yule, Usalama wa Taifa unaolinda uhalifu, haupaswi kuheshimiwa na raia yoyote yule. Usalama wa Taifa ambao Mbunge akizungumza Bungeni, unapanga njama tumlenge yule, Usalama wa namna huo haupaswi kuheshimiwa na raia yoyote yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yanahitaji nchi yetu, tufungue ukurasa mpya. Ningekuwa kwenye kiti cha Mheshimiwa Waziri anayesimamia Usalama wa Taifa, badala ya kusikitika na uozo unaozungumzwa kuhusu Idara anayopaswa kuisimamia, hii ingekuwa nafasi ya kuufumua upya Usalama wetu wa Taifa ili ulinde maslahi ya nchi yetu, ulinde maslahi ya kiuchumi ya nchi yetu, ulinde maslahi ya kiusalama ya nchi yetu badala ya kuwa chombo cha kuifanya Serikali dhaifu inayoongozwa na CCM kuendelea kubaki madarakani hata baada ya kukataliwa na ridhaa ya wananchi wanaozidi kubadilika kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wana hasira, hasira ya wananchi ni kwamba, Ofisi hii ya Rais, unasema peke yako, Ofisi yako ya Utumishi wa Umma inakuja hapa Bungeni, inawaahidi Bungeni kwamba maslahi yenu yatashughulikiwa. Walimu wanakwenda Mahakamani, Mahakama inaamua, Serikali ikae pamoja na Walimu chini ya msuluhishi, Wizara inashindwa kusimamia huwezi jambo hili...

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika kuna taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa kifungu namba 68(7), lakini nikizungumzia kuomba ufafanuzi wako. CCM kingekuwa ni chama dhaifu kingekuwa kimeshinda kwa asilimia zaidi ya sabini? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Mnyika unaipokea.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, tuokoe muda. Endelea Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, CCM kingekuwa Chama chenye nguvu, kingeshinda Jimbo la Ubungo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yanahusu maisha ya wananchi, mambo haya yanahusu udhaifu wa CCM wa kusimamia hata ilani yake. CCM iliahidi maisha bora kwa kila Mtanzania, leo kuna ugumu wa maisha, gharama za maisha zinapanda, Ofisi ya Rais, chin ya Tume ya Mipango ndiyo ilipaswa inusuru nchi yetu na mgogoro ambao utatokea karibuni, hakuna kitu kibaya kwenye Taifa la watu maskini kama gharama za maisha ziko juu, mwananchi ana kipato kidogo, mishahara ya watumishi wa umma haiongezwi, halafu Serikali hiyo hiyo inaridhia leo waongezewe nauli, kesho waongezewe gharama hizi, halafu wananchi wakiamka, mnalaumu Wapinzani kwa mambo ambayo mnayasababisha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wenzetu mlioko upande wa pili, muinusuru nchi yetu kwenye miaka michache iliyobaki kwa nyinyi kuwa madarakani, msiende kukabidhi nchi ikiwa vipande vipande. Tunawaomba ndugu zetu

mtambue kuwa, nyoyo za Watanzania zinatarajia kuwa Bunge hili litakuwa chombo cha kusimama kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Nchi yetu, kuishauri na kuisimamia Serikali, yanapotoka mawazo yenye tija kwa Taifa letu, ni vizuri mawazo haya yakasimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais afikishe salamu kwa Rais, kwa matatizo madogo madogo kama haya ya wananchi, Rais alikuja Jimboni Ubungo kwenye suala la maji tarehe 20 mwezi Machi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais akaahidi tarehe 25, tunakutana Ikulu kwenye masuala ya ufumbuzi wa tatizo la maji. Sasa kama Ofisi ya Rais inashindwa kuratibu utekelezaji wa ahadi ndogo kama Kikao, itakuwaje utekelezaji wa ahadi nyingi zilizotolewa kwenye kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inahitaji mabadiliko na mabadiliko ya kweli, ni lazima yaanzie kwenye siyo tu kubadili utamaduni wa utendaji wa viongozi wetu, inahitajika vile vile kubadilisha mfumo wetu mzima wa utawala na ndiyo maana wengine tunaamini kuwa, Katiba mpya inaweza kuwa ufumbuzi wa kitaasisi wa uongozi katika nchi yetu, wa utamaduni wa uwajibikaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa bahati mbaya, wenzetu upande wa pili, mnafikiri kwamba, zoezi la mchakato wa Katiba mpya, ni suala la kiuchaguzi kwa upande mmoja, lakini la pili mnadhani ni njia vile vilem baada ya kuiteka agenda ya Katiba mpya ambayo haikuwepo kwenye Ilani ya Chama chenu, haikuwepo katika ahadi zenu mnafikiri kuwa ni njia ya kurudisha imani kidogo katika nyoyo za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati mbaya vile vile mnayatekeleza mambo haya mkiwa na dhamira ovu, ndiyo maana mpaka leo ahadi ambazo zimetolewa na Ofisi ya Rais, hazijatekelezwa na ahadi hizi zinahusu mambo mengi kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulipotokea mauaji yaliyotokea Iringa, Ikulu ilitoa kauli kuwa kwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ameunda Kamati, Waziri wa Mambo ya Ndani akikabidhi ripoti ya Kamati yake, Rais atachukua hatua na atatoa kauli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka sasa, Rais hajachukua hatua, Rais hajatoa kauli pamoja na kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeainisha ndani ya ripoti ya Idara ya Serikali yenyewe kwamba, Jeshi la Polisi limekiuka Sheria ya Vyama vya Siasa, Kamanda wa Polisi anaitwa Kamuhanda ambaye mpaka leo hajachukuliwa hatua amekiuka Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika. Sasa ni Mheshimiwa Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Nchemba.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ningependa kuanza kwa kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ukurasa wa 86...

**NAIBU SPIKA:** Jaribu kutumia *mic* nyingine.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** *Hallow, hallow*. Naona iko vizuri.

**WABUNGE FULANI:** Kuna mtu hajazima *mic* yake. Mheshimiwa Mnyika hajazima.

**NAIBU SPIKA:** Tumia *mic* nyingine tafadhali, fuata ushauri wangu tuokoe muda.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ni Mbunge kwani Bunge la Jamhuri ya Muungano lina sehemu mbili; ni Mbunge kwa sababu anashiriki katika kupitisha na kuidhinisha Sheria zilizopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika sana Mbunge mmoja wa Chama cha CHADEMA akimdhihaki Rais wa

Jamhuri ya Tanzania, tena amekwenda mbali kwa kusema kwamba, Rais wetu ni mdini. Huyu Rais nakupa mifano midogo ya kudhihirisha ili Watanzania waelewe kabisa kwamba, Rais hana udini, nitakutajia Baraza lake la Mawaziri; ana Mawaziri 22 Wakristo na Waislam wako tisa, ana udini gani hapo? *(Makofi)*

Ana Manaibu Mawaziri 16 Wakristo na tisa Waislamu, kuna udini gani hapo? Kuna Makatibu Wakuu 19 Wakristo na tisa Waislam kuna udini gani hapo? Kuna Wakuu wa Mikoa 15 Wakristo na 10 Waislam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Makatibu Tawala 16 Wakristoo na tisa Waislam. Kwa nini mnataka kumdhalilisha huyu Mzee wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Waafrika tunafurahi tunapoona tuna Wabunge vijana, lakini tuna mila na desturi zetu, tunawaheshimu watu waliotuzidi umri. Naanza kupata wasiwasi malezi yenu yamekuwa ya namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu huyu ambaye naambiwa kuwa ana udini, tarehe 31 Machi mwaka 2013, ameongea na Taifa hili akilalamika juu ya vurugu zinazotokea katika nchi yetu kwa kuhusiana na masuala ya udini. Jamani acheni unafiki na uzandiki katika masula ambayo hayawezi kuleta umoja katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumnukuu Waziri Mkuu jana, ameongea maneno ya hekima kwenye masuala ya udini anasema hivi: "Mkiwa mnataka kumchagua mtu kuwa kiongozi ama kwa sababu ya dini moja ama kwa Uislam au Ukristo, upande mwingine utakataa na nchi itakuwa haitawaliki". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mnapokuwa kila siku kukikucha nyinyi kazi yenu ni kusema na hakuna asiyejua kuwa mwaka 2010, mlitumia udini sana. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alionesha kuwa yeye ni Waziri Mkuu wa kweli, tangu nimeanza kumwona katika Bunge hili,

jana nimeona cheche zake, Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee kutoa cheche zake, tukiwaachia hawa watu watatuchezea. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshitushwa na ndugu yangu na shemeji yangu Tundu Lissu, huyu ni Mwanasheria na namheshimu kama Mwanasheria aliyebobea kabisa, lakini kuna kitu kinaitwa *natural justice*. Hivi utamhukumu mtu bila kumpeleka Mahakamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanaowatuhumu ni lini walipelekwa Mahakamani ikaonekana kuwa Serikali ya CCM imewaachia ikawatoa? Mbona Waziri Mramba yuko Mahakamani? Mbona Waziri Yona yuko Mahamakani? Mbona Katibu Mkuu Mgonja yuko Mahakamani? Sasa mnasemaje kwamba, Serikali ya CCM kuwa watu wanaofanya matatizo haiwapeleki Mahakamani? Hizi taarifa mnazitoa wapi? Acheni kudanganya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wameamka na nakubaliana na maneno aliyosema Waziri Mkuu, nadhani ninyi mnaanza kuwa na hofu ya mwaka 2015, ninachowaambia ni kuwa, *mmebugi men*. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** *Sharobaro*.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja kwenye sula la Usalama wa Taifa. Jamani wote tunafanya utafiti, someni muone, katika nchi inayoongoza watu wa Usalama wa Taifa wanaofanya kazi nzuri Tanzania ni mojawapo, lakini inasikitisha kuwa nyinyi wengine mko humu ndani ya Bunge awamu ya kwanza mlikuwa hamjazaliwa bila shaka. Tuliweza kupambana na kulikomboa Bara la Afrika kutokea Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo nataka kuwaambia ndugu zangu leo, siku zote Usalama wa Taifa wanakamata kambare, sijui dagaa kwenye Upinzani, juzi

wamekamata kapapa kadogo tu, basi wamehangaika, kila siku wanapiga kelele. Hebu acheni watu wa Usalama wa Taifa wafanye kazi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ilikuwa ni *bashrafu* ngoja nije katika hoja yangu. Pale Tabora tuna Chuo cha Utumishi na tuna wanafunzi zaidi ya 5000 sasa hivi pale, lakini hosteli hazitoshi, kwa hiyo, naomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** *Lahaula walakuwwata!*

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Aaa. Ninachoomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anamalizia hebu akikumbuke Chuo kile cha Utumishi cha Tabora, tuweze kupata hosteli za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza ametujengea *dispensary,* naweza kudiriki kutamka katika Bunge lako kwamba, sijawahi kuona popote katika Tanzania hii isipokuwa pale Chuo cha Utumishi Tabora. Lakini kinachosikitisha ni kwamba, hakuna madawa na hakuna Madaktari, tunaomba tupate Madaktari na madawa ili tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU wanafanya kazi nzuri sana, lakini iko haja ya kuwaongezea bajeti yao, safari hii tumewapunja sana tumewapa *only 15 billion shillings* na kazi wanaifanya ni ngumu sana. Nafikiri wakati umefika sasa ili TAKUKURU iweze kufanya kazi nzuri, hebu tuwape meno, badala ya kuwa kila wanapofanya kazi ya uchunguzi inabidi waende kwa *DPP* ili ndiyo waidhinishe watu kupelekwa Mahakamani. Kwa hiyo, hii inawavunja morari kidogo,nadhani iko haja sasa Takukuru wapewe ruksa na wao waweze kupeleka watu Mahakani kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuisihi Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, uhuru wa demokrasia unakwenda na wajibu, kama mtu hajui wajibu wake, basi achukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza katika Bunge lililopita mwaka jana na nikajibiwa ndani ya *Hansard* majibu hayo yapo, kwamba Mbunge yeyote atakayetafuta kwa ujanja wake nyaraka za Serikali bila kupitia utaratibu wa kuomba Bungeni, anakuja na kuzi- *present* hapa, hivi kwa nini watu kama hawa hawachukuliwi hatua?

**TAARIFA**

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa huyu Mheshimiwa wa Tabora Mjini kwamba, sababu pekee Wabunge hawachukuliwi hatua ni kwamba, Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inalinda uhuru wa majadiliano ndani ya Bunge, kama hakuwa anajua na amesema ana Katiba, asome. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rage, unaipokea taarifa?

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Kwanza kwa kuwa ni Mwanasheria naikataa taarifa yake na namwomba akarudie tena kusoma digrii yake ya Sheria. Nyaraka za Serikali ni mali ya Serikali, hakuna Mbunge anayeweza kuchukua, soma Kanuni, iko kwenye Kanuni vizuri kabisa, ukitaka nyaraka ya Serikali unamwomba Spika, anatoa maelekezo, utaletewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rage. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, kwa dakika 10!

**MHE. MWIGULU L.N.MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuwasihi Watanzania waelewe vizuri hili,

kwamba, sote tunakubaliana kwamba, jambo la udini kwa Tanzania ni jambo geni. Tanzania imeongozwa na Rais wa kwanza Mkristo alitoka CCM, akaja Muislamu alitoka CCM, akaja Mkristo alitoka CCM na akaja Muislamu ametoka CCM na ndiyo wamekuwa Wenyeviti wa CCM, lakini vilevile tumeendesha chaguzi tangu enzi ya chama kimoja mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna jambo geni limekuja lazima tujiulize nani kaja nalo? Leo hii watu wanasema kuwa Rais ni muasisi, ninachokumbuka sijui watu wengine wanakuwa na *hangover* gani? Kitu ninachokitambua ni kwamba, Rais amekuwa ni mtu wa kwanza kukemea jambo la udini na alilikemea kwa sababu kuna mgombea wa chama kimojawapo baada ya kutumia viongozi wa ofisi za Chama chake katika ngazi tofauti, alikuwa anakwenda anaongea na baadhi ya viongozi wa dini kama ndiyo viongozi wa mikutano ya ndani ya chama chake. Hicho ndicho Rais alichokikemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Slaa hakufanya mkutano wa hadhara Singida, alikusanya baadhi ya viongozi wa dini kama ndiyo mkutano wa ndani wa chama chake, hili linakubalika wapi? Wakati CCM inatumia Mabalozi, inatumia Wenyeviti wa matawi, yeye akatumia wale, ndicho Rais alichokemea na nchi hii ina Rais mmoja tu akishakemea jambo...

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba nimemwona Mheshimiwa Susan, wengine kaeni chini.

**WABUNGE FULANI:** *Chief Whip* amesimama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga!

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa muongeaji kuwa, mimi ndiye nilikuwa mratibu wa kampeni za mgombea Urais nchini

Tanzania na nilikuwa naandaa mikutano ya hadhara. Mkutano wa Singida tuliufanya kwenye hoteli na mimi ndiyo niliyeandaa, tulikutana na wadau na viongozi wa Chama chetu. Kwa hiyo, haya anayoyasema ni uongo, ni uongo, wa mchana kweupe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana huwa sikurupuki, wale walioingia kwenye kikao kile, viongozi wa kidini, walishaona kuwa ule ni upuuzi na unaipeleka nchi pabaya wako tayari kulisema hili na ndiyo maana huwa nasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeikataa hiyo taarifa.

**MHE. TUNDU A.M LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nafikiri sijui ni huu ugeni wa kuwa Bungeni…

**WABUNGE FULANI:** Aahh!

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo, lazima nitoe maoni yangu pia kama kiongozi. Lazima kuwa na uwezo wa kusikiliza watu wengine, umeongea dakika kumi, umesimama mara ngapi? Karibu mara ishirini unaongea wewe peke yako, siyo utaratibu ukiwa *Chief Whip* kuwa sehemu ya kufanya vurugu ndani ya Bunge.

Nasema hivi, askari mtoe nje Tundu Lissu, askari toa nje Tundu Lissu!

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani.

**NAIBU SPIKA:** Askari wako wapi, toa nje.

**MBUNGE FULANI:** Ubabe, huo ni ubabe.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa umeanza *double standard,* huo ni ubabe.

**NAIBU SPIKA:** Askari mtoe nje haraka sana.

**MBUNGE FULANI:** Huo ni ubabe, hatoki mtu, hatoki mtu.

**NAIBU SPIKA:** Nasema atolewe nje, askari toa nje huyo, nyinyi mnafanya nini huko? Wewe fanyeni hiyo kazi hapo atoke huyo.

*Ruling* yangu ni kwamba, kwa muda wa siku tano mfululizo hatakiwi kuwemo ndani ya Bunge, ninasema atolewe nje siku tano mfululizo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amefanya nini?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo ujinga wenu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Bunge zinakiukwa.

**NAIBU SPIKA:** Naagiza askari waongezwe mpaka atolewe nje.

**MBUNGE FULANI:** *AG* watu kwenye *TV* wanawacheka.

**MBUNGE FULANI:** Mjadala wa nini?

**NAIBU SPIKA:** Na *ruling* nyingine ambayo naongeza juu ya hao pamoja na Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye ametolewa kwa siku tano, Wabunge wafuatao kwa utovu wa nidhamu walioonesha na wenyewe ni siku tano

Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Mbilinyi, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Kiwia na Mheshimiwa Wenje, wote hawa ni siku tano. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, baada ya muda kwisha, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 18 Aprili, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*